ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.

14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34 .Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg. Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Saba – Tarehe 5 April, 2012

(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, *(Mahmoud Muhammed Mussa)* alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa Sita wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 18 Januari, 2012 hadi tarehe 27 Januari, 2012. Baraza lilipitisha Mswada mmoja wa Sheria ufuatao. Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Kama ilivyotakiwa chini ya Kifungu cha 90(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2011, naomba kutoa tarifa kwamba Mswada huo umekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 120
Dawa za Kurefusha Maisha Vyuo Vya Mafunzo Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-
Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na kampeni za kupambana na ugonjwa wa ukimwi.

(a) Kwa vile yamekuwepo malalamiko ya upungufu wa dawa hizo katika Vyuo vya Mafunzo na waathirika ni wafungwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka dawa za kutosha katika vyuo vya mafunzo.

(b) Matumizi ya dawa hizo yanahitaji lishe bora. Je, Serikali inazingatia vipi upatikanaji wa chakula kwa wafungwa kwa kuwapa milo mitatu kwa siku, badala ya mlo mmoja kwa wafungwa wakiwemo waathirika wa ukimwi.

(c) Je, Serikali imekuwa ikisaidia Vyuo vya Mafunzo kiasi gani cha mgao wa dawa kwa mwaka, kwa kuzingatia hospitali za vyuo hivyo zimekuwa zikisaidia matibabu kwa wananchi wasiofungwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako swali lake nambari 120 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Idara Maalum ya Vyuo vya Mafunzo inatumia jumla ya TZSh. 12 milioni kwa ajili ya kununulia dawa ambazo zinatumika katika vituo vyake vya afya. Mbali ya dawa hizo kuwahudumia Askari na wanafunzi pia zinatumika kwa ajili ya huduma za wananchi wanaofika katika vituo hivyo. Miaka inayokuja Serikali inategemea kuongeza bajeti ya dawa kutoka TZSh. 12 milioni hadi 20 milioni ambazo pia zitasaidia kununua dawa mbali mbali zikiwemo za Ukimwi.

Serikali itaendelea na juhudi zake za kuwapa chakula wanafunzi wa Vyuo vya Mafunzo milo mitatu (3). Tumeshaanza mpango huu kwa mwaka huu wa fedha, lakini hakukuwa na bajeti maalum, kwa hiyo bajeti maalum tutaitayarisha kwa mwaka ujao wa fedha. Hata hivyo, tumefanya mikakati ndani ya wizara na wanafunzi wanapata milo mitatu wakiwemo wanafunzi walioathirika na ukimwi ambao Mheshimiwa Mwakilishi ameuliza.

Aidha, vyuo vya Mafunzo vitaendeleza zao la mboga mboga na mazao mengine muhimu yenye virutubisho muhimu kwa wangonjwa hasa wagonjwa wa ukimwi, ambalo tunahisi kwa kiasi kikubwa watazidisha urefu wa maisha yao kwa kula vyakula hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Kwa vile suala la dawa za kurefusha maisha ni muhimu. Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha lishe bora kwa waathirika wa ukimwi inapatikana pamoja na dawa za kurefusha maisha.

(b) Kwa vile bajeti ya Chuo cha Mafunzo ni milioni 4 ambayo haikidhi hata kidogo, huoni kwamba ipo haja katika kipindi kinachokuja, kesho kutwa Mwenyezi Mungu akitupa Uhai na uzima kuwaongezea bajeti hiyo.

(c) Vile vile isitoshe, wanafunzi hivi sasa wanapelekwa mahakamani kwa miguu hilo unalijua kutokana na bajeti yao kuwa ni finyu.

(d) Vile vile chakula wanachokula hivi sasa ni cha aina moja ikiwemo ugali, uji na maharage ni kutokana na bajeti yao finyu. Kamati ya Wanawake na Watoto ilitembelea na kuona hali halisi ilivyo. Je, una wito gani kuhusu suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jawabu langu la msingi kwamba Serikali itajitahidi kuwapatia dawa ambazo zinarefusha maisha wale wanafunzi ambao wameathirika kwa ukimwi, na lishe bora ambao kwa idadi katika Chuo cha Mafunzo tunao 12. Wataalamu wa Afya wanatwambia, elimu ya Ukimwi inatwambia kwamba, wale walioathirika tusiwanyanyapae bali tuwape lishe nzuri. Imeonekana tu kwamba kweli wale wanaofuata masharti na miko na lishe nzuri basi wanaishi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili hatulifanyi peke yetu kama Chuo cha Mafunzo au Serikali au Wizara, kuna taasisi nyingi sana za kilimwengu za kimataifa na za kitaifa zinazoshughulikia suala hili. Kwa hiyo kwa Chuo cha Mafunzo hapa tuna NGO moja iliyokuwepo hapa Tanzania inaitwa *Pharma Access Foundation*. Wao wanatusaidia dawa za ukimwi, wanapita hata kuangalia wanavyoishi hao wanafunzi kuona kwamba wanapata zile huduma zipasazo.

Suala la mwisho lilikuwa refu mno naomba alirejee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kutokana na bajeti ya Chuo cha Mafunzo ni shilingi milioni 4 kwa mwaka na haikidhi hata kidogo. Je, ana mpango gani wa dharura wa kufikiria Chuo kile muhimu ikiwemo hivi sasa baadhi ya wanafunzi kupelekwa mahakamani kwa miguu, na kula mlo wa aina moja yakiwemo maharage na sembe kutokana na ufinyu wa Bajeti, kutokana na keshokutwa bajeti ana mpango wa kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ukweli kwamba suala la usafiri hili si tatizo, kwani tunashukuru wale ambao wanajiweza ni kama wanafanya mazoezi tu. Kwa sababu kukaa gerezani muda mrefu kule nako kunachosha. Kutembea kiinua miguu mpaka hospitali kwa mgonjwa anayejiweza, au kufika kortini kwa anayejiweza mbele ya ulinzi nafikiri ni zoezi zuri sana, na nchi yetu ni ya amani na wanafunzi wetu wana uelewa mzuri, hawana matatizo. Kwa hilo nafikiri sio tatizo.

Suala alilolizungumza la bajeti ni kweli kwamba kwa bajeti nakiri kwamba mahitaji yetu ni mengi lakini kiwango cha bajeti tulichowekewa kwa sababu serikali bado ina vipaumbele vingi. Lakini kubwa ninalotaka kusema kwamba Chuo cha Mafunzo kina kambi nyingi ambazo ziko nje ya mji, na wanajitahidi sana kuzalisha vyakula kwa matumizi yao. Kwa kweli nashukuru sana maafande wa kule na wanafunzi wenyewe wana ufahamu huo. Kwa hivyo wana vilimo kama muhogo, mpunga, mbaazi, kunde, wanalima sana na zinawatosheleza kwa chakula. Hilo tunashukuru sana na wanajitahidi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri suala moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali mara kwa mara ilikuwa ikihimiza kutowanyanyapaa waathirika wa ukimwi. Lakini leo nashangaa nasikia kuna waathirika wapo Chuo cha Mafunzo, bila shaka wamefungwa.

(a) Je, huku si kuwanyanyapaa.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanafunzi hawa wanawatoa Chuo cha Mafunzo na wanawaweka pahali pengine maalum, ambapo hapaitwi Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ile kuwatambua wakiwa kule gerezani kwamba wameathirika wana maradhi ya ukimwi sio kuwanyanyapaa. Ni imani yangu kwamba yale maradhi hawakuyapata wakiwa ndani ya Chuo cha Mafunzo. Kule wamekwenda nayo, kwa kuwa wanapimwa, wanashughulikiwa kimatibabu ndipo walipobainika kwamba wana maradhi yale. Nafikiri ni vizuri baada ya kubainika wapate uangalizi maalum, chakula, pamoja na dawa.

Chuo cha Mafunzo hakuoneshi kwamba kuna unyanyapaa, nafikiri wanachanganyika na wenzao, wanafanya kazi pamoja, kwa sababu tu wao wameugua. Lakini kama tulivyosema wao wanapata uangalizi maalum. Hilo tumeliona, tunajitahidi. Mimi nimewahi kwenda kuwatembelea, nimewaona na wanaendelea vizuri sana wala hawahisi kama wana maradhi.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Hawa wanafunzi kwa sababu tu za kibinaadamu na wao wameshaathirika, huoni Mhe. Waziri kuwaweka pamoja na ambao hawajaathirika kwa hofu zile za kibinaadamu ambazo huwa tunasikia huwa zinatokea, ni kusababisha madhara zaidi kwa wale ambao afya zao bado ni sahihi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema ikiwa kwa kweli tutawatenga hapo ndio tutaonesha huo unyanyapaa usiotakiwa. Nafikiri ni sera nzuri na wao wakapata zile shughuli za kawaida ndogo ndogo, kuna kazi nyingi kule, kwa hiyo wakichanganyika na wenzao wakifanya zile shughuli pamoja. Nafikiri hakuna haja ya kuwa na hofu ya kunyanyapaa.

Lakini suala alilosema la kufikiriwa basi hiyo ni rai nzuri tutaizingatia na kila mwaka Mhe. Rais huwa anatoa msamaha kwa wanafunzi kwa hiyo fikra yako tutaichukua na kuizingatia.

Nam. 121

Kituo Kikuu cha Daladala Darajani Kukosa
Sehemu ya Kujihifadhi Abiria

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Serikali imefanya kazi nzuri ya kutengeneza eneo la Kituo cha Daladala Darajani lakini tatizo kubwa ni kukosekana sehemu ya kujihifadhi abiria katika kituo hicho.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kujenga kituo cha kujihifadhi abiria katika kituo hicho.

(b) Mhe. Waziri kwa vile eneo hilo ni sura ya Mji, kwanini Serikali kwa muda mrefu haijajenga Kituo cha Kisasa na kuweka taa katika eneo hilo ambalo lina mkusanyiko wa watu hadi nyakati za usiku.

(c) Mhe. Waziri, Je, ujenzi huo utaanza lini tukizingatia kuwa Msimu wa Mvua za Masika unakaribia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako swali lake nambari 121 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa lina mpango wa kujenga jengo la kupumzikia abiria katika kituo cha dala dala cha Darajani. Mpango huu upo katika *Master Plan* ya uendelezaji wa Mji wa Zanzíbar, ikiwa ni pamoja na

eneo hilo la Darajani ambapo pana mpango wa kuweka kituo kikubwa cha gari za *private* na za abiria yaani kama *bus stand* kama ilivyo katika miji mikubwa unayoifahamu wewe ulimwenguni na hata katika Bara letu la Afrika.

Tatizo lililojitokeza ni nafasi kuvamiwa na wafanyabiashara wale wanaokwenda bila ya mpango maalum. Hili tunalifanyia kazi kwa pamoja kwa busara, kwa hekima ili tuone kwamba hili linafanikiwa, ili hiyo nafasi ipatikane ya kujenga hicho kituo. Michoro ya awali ya ujenzi huo tayari imetayarishwa na Baraza la Manispaa lina mpango wa kushirikisha Sekta binafsi katika ujenzi huo.

Nakumbuka Mhe. Jaku, utakubaliana na mimi kwamba utakuta *bus stand* nyingi kuna matangazo ya wafanyabiashara, na wao ndio wanasaidia kuzijenga vile. Kwa hivyo na wao tutashirikiana nao katika suala hilo. Ili ile karaha ya mvua za masika ikifika, tuweze kuondokana na usumbufu kwa abiria wetu. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kutokana na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Kutokana na umuhimu wa eneo lile, Serikali inachukua hatua gani za dharura kutokana na waathirika wakubwa wakiwemo wanafunzi na wagonjwa.

(b) Kwa hivi sasa kumeibuka vitendo vya wizi katika eneo lile kutokana na kuwepo kwa giza. Je, una mpango gani wa kuweka askari kulinda eneo lile, ili watu wasipate kuibiwa, wakati wizara yako imejitahidi kufunga gari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Ni kweli kwamba kuna watu wazima na kuna watoto ambao wanahitaji usaidizi. Tutajitahidi kufanya mpango wa dharura ili watu kama hawa wasitaabike wakati wanasubiri gari huku tukiwa tunakamilisha mipango yote ya kujenga vituo vya kudumu

(b) Kuhusu ulinzi hili nilitaka kusema kwa mujibu wa *master plan* yetu ya kuendeleza mji wetu, tuna mpango wa kuweka taa za barabarani kwa kutumia miyonzi ya jua. Tumeshazungumza na ndugu zetu na marafiki wetu wa Serikali ya Jamhuri ya watu wa China. Mpango huu tunatarajia kuanza mapema iwezekanavyo. Taa hizi za barabarani naamini zitatusaidia hata pale kwenye *stand* ya Darajani kupamurika ili pasiwe na maficho ya wahalifu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri kama ifuatavyo. Alipokuwa anajibu swali la Mhe. Jaku amesema kwamba sababu moja inayowafanya wasijenge banda la kupumzikia abiria, ni wafanyabiashara ambao wanafanya biashara pale chini ambao waliombwa kupelekwa Saateni.

Historia ya Baraza la Manispaa mara zote wamekuwa wakishindwa kuendeleza mji. Kwa mfano wameshindwa hata kuondosha uchafu pale Darajani unaotokana na matumbo ya samaki, wameshindwa kuendeleza ile *Pemba grass* ambayo imepigiwa debe sana na Mhe. Waziri kwamba ni kivutio cha watalii. Lakini pia wameshindwa hata kujenga vyoo.
Je, Mhe. Waziri, atakubaliana nami kwamba sababu ya kuwepo kwa wafanyabiashara siyo iliyosababisha wizara yake kujenga banda pale, bali ni uzembe na ubovu wa Manispaa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ukweli Mhe. Mwenyekiti, kama Baraza la Manispaa liache kufanya kazi yake siku moja tu pale Marikiti Mheshimiwa huwezi kupita pale, huo ndio ukweli lazima tukubaliane nao. Kwa kweli vijana wanajitahidi sana. Tatizo letu ni upungufu wa zana, lakini pia na tabia yetu sisi wenyewe wafanyabiashara kutupa taka ovyo. Jengine ni kufanya biashara mahali pasipotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na wafanyabiashara wa samaki, soko limeshafungwa jioni saa 10:30 au 11 wao ndio wanatoka nje sasa. Wanaacha kuuza samaki ndani wanapanga nje na wafanyabiashara wengine wanapanga chini, hata kupita kwa miguu utashindwa. Mimi nakuomba leo mimi na wewe jioni twende zetu tukashuhudie hiyo hali. Halafu utusaidie kuwaelimisha wafanyabiashara kwamba twende kwa mpango, hakuna mji wowote ambao hauna mpango. Kila mji ni lazima uwe na mpango na tufuate taratibu na sheria zilizowekwa.

Nam. 43

Nyongeza za Mishahara

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny Mhe. Rashid Seif Suleiman) - Aliuliza:

Mhe. Mwenyekiti, katika nyongeza za mishahara zilizotolewa Oktoba 2011, taaluma za vyeti vya wafanyakazi ndizo zilizozingatiwa zaidi.

(a) Je, wale wenye taaluma ndogo lakini wametumikia muda mrefu, malipo yao yanalipwa vipi.

(b) Kuna sababu zipi za msingi zilizofanya watumishi wenye taaluma sawa na miaka sawa ya kazi kuwa na tofauti kubwa sana ya viwango vya mishahara kwa sababu tu mmoja amepewa wadhifa wa kuteuliwa na Rais.

(c) Utaratibu wa kutathmini wafanyakazi (*appraisal*) unategemewa kuanza lini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika mabadiliko ya mishahara yaliyofanywa Oktoba 2011 vyeti vya taaluma vya wafanyakazi ndivyo vilivyozingatiwa zaidi. Hii haina maana kama muda wa utumishi haukuzingatiwa, kilichofanyika katika mabadiliko hayo ni kutilia mkazo zaidi taaluma. Kwa hivyo wale wote wenye taaluma ndogo lakini wametumikia muda mrefu nao pia walifanyiwa mabadiliko ya mishahara yao kulingana na taaluma walizonazo, na urefu wa muda wao wa kazi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, inapotokea kuna watumishi wenye taaluma na miaka sawa, lakini mmoja ni mteuliwa wa Rais au anashika nafasi ya uongozi wanaweza wakapitana katika mshahara, na sababu kubwa hapa sio muda wa kazi wala sio taaluma, bali ni majukumu ya ziada ya uongozi aliyopewa mfanyakazi mteuliwa.

(c) Zoezi la tathmini la wafanyakazi ni zoezi la kitaaluma ambalo kwa muda mrefu halikuwa likitekelezwa ipasavyo. Hivi sasa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendeleza taratibu za tathmini ya wafanyakazi na taaluma za kisasa zaidi, ili kupata ufanisi katika Utumishi wa Umma hapa Zanzibar. Kwa taarifa ya Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu, katika hatua mpya imeshaandaliwa Rasimu ya fomu ya tathmini ya utendaji wa wafanyakazi katika Utumishi wa Umma. Hatua inayofuata sasa ni kuiwasilisha rasimu hiyo kwa wadau mbali mbali kwa maoni na ushauri wao kabla ya kuanza kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa tarifa ya Baraza lako tukufu ni kwamba hatua hiyo ya wadau hivi sasa tayari imeshamalizika, kinachosubiriwa sasa ni fomu hiyo kuwasilishwa kwenye Kamati ya Uongozi wa Wizara ili iweze kuchukuliwa hatua.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Je, Serikali imetumia vigezo na sifa gani kwa mahakimu wa mahakama ya mwanzo kulipwa mishahara mikubwa ukilinganisha na kitengo cha muendesha mashtaka cha DPP wakati kazi zao wanazozifanya ni sawa sawa.

(b) Kwa vile Serikali imeamua kuimarisha uwajibikaji na kupiga vita rushwa, je, mpango huu utafanikiwa vipi kama Mahakama na Mahakimu wa mwanzo wanaendelea kulipwa mishahara duni wakati kesi za uhalifu zikiwa zinaendeshwa na wao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Suala hili la ufafanuzi wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Wanasheria wengine takriban tokea limeanza Baraza nimekuwa nikilitolea ufafanuzi. Ningemuomba Mhe. Jaku kama anataka maelezo zaidi ama asubiri kwa mujibu wa utaratibu wa Kanuni aulize swali lake tena, ili niweze kumfahamisha. Lakini kwa mujibu wa kanuni zetu suala hili nimelitolea ufafanuzi karibu hiki nzima sasa.

(b) Kwa sababu hiyo inawezekana Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wakapokea rushwa, kutokana na pengine kunyimwa fursa ya kuweza kupewa mshahara sawa pengine na wanasheria wengine.

Ninachotaka kumwambia Mhe. Jaku na hasa kwa taarifa ambayo leo Mhe. Mwenyekiti, umetupa tumepitisha sheria hii hapa ya kupambana na kudhibiti rushwa. Sheria ile haitatoa msamaha kwa mfanyakazi yoyote yule kwa sababu ya kisingizio cha kulipwa mafao madogo.

Hatua ya Serikali ni kuona ukweli kwamba kama Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wanastahiki kulipwa maslahi kwa mujibu wa kazi zao. Na hilo, Serikali kama ilivyokwisha kulitolea taarifa jana imeanza kulichukulia hatua baada ya kuona kwamba wao kwa mujibu wa viwango vyao vya mshahara wao hairuhusu kulipwa mshahara sawa na Mahakimu wa Wilaya na ngazi nyengine au wanasheria wengine. Wizara yangu imechukua hatua maalum ya kuwawekea posho maalum kwa ajili ya mazingira ambayo wanayafanyia kazi, mpaka hapo Serikali itakapokwisha kukamilisha taratibu za kufanyia kazi *scheme of service* ya Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo, basi nao maslahi yao yatazingatiwa ipasavyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeongeza mishahara kwa wafanyakazi ambao wana taaluma na wale wenye uzoefu kwa ajili ya kuboresha na kuwalinda wafanyakazi wetu ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi katika nchi yetu. Mhe. Waziri kuna wafanyakazi ambao hawana elimu, lakini wana uzoefu wa muda mrefu na wanafanyakazi katika mazingira magumu ambayo ni hatarishi kwa maisha yao. Kwa mfano, kama mafundi wa sehemu za umeme, na mafundi waliomo kwenye chelezo na sehemu nyengine ngumu.

Je, Mhe. Waziri watu hawa wanalalamika kama wao hawakufaidika na nyongeza hii ya mishahara, hivyo utakubaliana na mimi kama kuna haja ya kufanya utafiti wa kina na ukigundua kama kweli kuna watu ambao wamefanyiwa hivyo wakaongezewa mishahara yao ili na wao wafaidike. Na kama hukubaliani na hilo utafanya utafiti ukaangalie ikiwa wao hawafaidiki hatuoni kama kutakua na maonevu ndani yake.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakubaliana nae kama kuna mfanyakazi yeyote awe wa taasisi ya umma, awe wa sekta binafsi kama hapati mafao kwa mujibu wa taratibu zilizopo basi tutakua hatumtendei haki. Lakini nataka niseme kwamba mfano alioutoa ni wafanyakazi wa mashirika ya umma ambao maslahi yao yanashughulikiwa na bodi zao, wafanyakazi wa Shirika la Umeme na wafanyakazi wa Shirika la Bandari wanashughulikiwa na bodi zao. Sisi kama Serikali tunasimamia sera kwa jumla, mpaka sasa hivi hatujapata kesi hiyo kwenye ofisi yangu ya utumishi wa umma kwamba wafanyakazi wa mashirika hayo baadhi ya haki hawazipati. Lakini kwa taarifa ambayo nimeipokea hapa Wizara yangu itachukua hatua ya kuwasiliana na Waziri muhusika ili aweze kufuatilia hayo, kama ni kweli hali ni hiyo basi wataweza kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za mashirika yao ya kuwahudumia wafanyakazi wao.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, katika nyongeza za mishahara zilizotolewa kuanzia mwezi wa Oktoba, 2011 sasa hivi imetimia kama miezi sita hivi, na miongoni mwa wafanyakazi walioathirika na nyongeza hizi ni wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ambao zaidi ya wafanyakazi 80 hawajafaidika kabisa na nyongeza hii. Je, Mhe. Waziri ni lini wafanyakazi hawa wa Baraza la Wawakilishi watapata nyongeza yao.

(b) Katika nyongeza yao itazingatia pia na *arrears* ambazo kwa kipindi chote hiki wamekosa ongezeko hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, wako wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi ambao hawakufaidika na nyongeza hii ya mishahara mipya, ni wale wafanyakazi ambao walikua hawana vigezo vya taaluma ya kazi zao. Wakati Serikali inafanya mabadiliko ya mishahara, wafanyakazi hawa tayari walishavuka kiwango cha mishahara kile kilichoongezwa na Serikali. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba kama kuna mmoja amepata kile ambacho anaongezewa mwengine, ina maana atapata yule ambaye hajaongezewa. Mhe. Mwenyekiti, Serikali ililiona suala hili na mambo haya yaliletwa kwenye ofisi yetu, lakini kutokana na utaratibu ambao Serikali iliamua, hawa wafanyakazi walishavuka kiwango cha kima ambacho kimeongezwa na Serikali. Hivyo, wafanyakazi hawa katika mwaka huu wa fedha ujao watazingatiwa kupandishwa mishahara kulingana na viwango ambavyo vitaongezwa na Serikali kwa mujibu wa taaluma zao.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kua watalipwa *arrears* au hawatalipwa ni kwa sababu Serikali haikuamua kuwaongezea mishahara yao kwa kipindi cha Oktoba tabaan wafanyakazi hawatastahiki kulipwa *arrears* kwa sababu walikua hawapo katika wafanyakazi ambao walikuwa na stahiki kupata hiyo *arrears*.

Nam. 13

Ujenzi wa Maabara ya Chake-Chake

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Kny: Mohammed Said Mohammed) – Aliuliza:-

Serikali kwa kuona umuhimu wa maabara katika hospitali zake hapa Zanzibar imeifanyia ukarabati mkubwa maabara ya Hospitali ya Chake Chake Pemba.

(a) Je, ujenzi huo umegharamiwa na taasisi au shirika gani;
(b) Je, ni kiasi gani kimetumika kwa ajili ya ujenzi huo.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa maabara ya uchunguzi wa maradhi ya Hospitali ya Chake Chake Pemba umegharamiwa na *Internation Centre for AIDS Care and Treatment Programme (ICAP)* na Chuo Kikuu cha Columbia Marekani ambacho husaidia matibabu ya ukimwi, kutoa huduma kwa makundi hatarishi kwa ukimwi hasa wale wanaojidunga sindano. Jinsi ya kutoa ushauri nasaha, kusambaza vipeperushi na kutoa huduma za matibabu kwa kuwafuata wahusika pale ambapo vituo vya afya viko mbali na wananchi.

b) Kiasi kilichotumika katika ujenzi huo ni dola za Marekani 85, 157 sawa na 140, 000,000 shilingi za Kitanzania.

Nam. 76

Mradi wa Umeme Vijijini

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Mhe. Waziri katika kuwasilisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2011-2012 kuhusu Mradi wa Umeme Vijijini alisema kua atahakikisha kua anakamilisha kuwapelekea umeme wananchi wa vijiji vilivyobakia.

a) Mhe. Waziri utekelezaji wa tamko hilo umefikia hatua gani.

b) Unawaambia nini wananchi walio katika vijiji amabvyo bado havijapata umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa tamko hilo ni kwamba hadi sasa hivi vijiji 14 kwa Unguja na Pemba vimeshapelekewa umeme. Aidha, Wizara yangu iko mbioni katika kukamilisha kazi za ujenzi wa njia ya kupelekea umeme katika vijiji 6 vya Unguja na Pemba.

b) Mhe. Mwenyekiti, nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yangu ni kuhakikisha kua vijiji vyote ambavyo havijapata huduma hiyo, basi vinapelekewa huduma hiyo ya umeme.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata jibu zuri la Mhe. Naibu Waziri hivyo naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, iliposomwa bajeti hii vijiji vyote vilivyomo katika Jimbo la Mtambwe ambavyo vilikua havijapata umeme kwa mfano, Mtambwe Kaskazini, Chanjaani, Chekea, Mtambwe Mkuu. Mtambwe Kusini, Kivumoni, Mitambuuni, Kinazini. Shehia ya Kisiwani, Tondooni, Machuga, Shehia ya Piki, Matuuni, na kadhalika. Mhe. Mwenyekiti, vijiji hivyo mpaka leo havijapatiwa hata kijiji kimoja wakati anasema kazi inaendelea.

Je, vijiji hivi vilivyomo katika Jimbo la Mtambwe ikiwa ni moja kati ya majimbo ya Zanzibar vinakosa nini mpaka leo havijapata huduma hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba vijiji hivyo vitapatiwa huduma hiyo kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yangu nia yake ni kuhakikisha kusambaza umeme katika vijiji vyote ambavyo havijapta umeme. Mhe. Mwenyekiti, vijiji hivyo namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba hali itakaporuhusu tutavipelekea umeme vijiji hivyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alisema kuna vijiji 10 vya Unguja na Pemba tayari vimeshapatiwa huduma hiyo, nilikua nataka kuvijua vijiji hivyo ni vipi na sita viko njiani kupatiwa vya Unguja na Pemba navyo pia nilikua nataka kujua ni vipi.

b) Vile vile nilikua nataka kujua baadhi ya vijiji vya Jimbo la Mkwajuni ni lini navyo vitapatiwa huduma hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Mwakilishi vijiji vilivyopatiwa huduma hiyo baada ya kutoka tamko la Mhe. Rais ni vijiji 10 ikiwemo kijiji cha Uswisi Makunduchi, Kijiji cha Fuoni Kidarajani, na vyenginevyo. Lakini vyengine dhidi ya hivyo nitakupatia kwa maandishi. Mhe. Mwenyekiti, vijiji ambavyo tutakavyovisambazia tutatoa taarifa rasmi baada ya kuvipanga, lakini kila kile ambacho kimekosa basi tutakitia kwenye orodha ili kuvipelekea umeme.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri katika kikao kilichopita nilimuuliza suala na akaniambia kwamba kijiji cha Muuka tukishirikiana mimi na yeye tutakwenda huko ili kwenda kuona sehemu ambayo haijapata umeme. Je, Mhe. Naibu Waziri mpaka hii leo ahadi hiyo imefikia wapi au Serikali bado iko mbioni.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nimemwambia Mhe. Mwakilishi kwamba tushirikiane na twende tukaone pamoja, na nilisubiri taarifa yake ili anipe taarifa rasmi kwamba tuondoke. Lakini kama ningekwenda mimi tu ingekua sawa na mzigo usiokua na mwenyewe, nisingejua wapi pakuanzia na wapi pakumalizia. Kwa hivyo, niseme kwamba Mhe. Mwakilishi kama uko tayari sasa hivi basi mimi niko tayari twende tukaangalie ili tujue nini cha kukifanya na tuweze kukupelekea umeme kijijini kwako.

UTARATIBU

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mwakilishi na yeye ni mwakilishi, lakini yeye ni Naibu Waziri yeye ndiye mwenye mamlaka ya kuniambia mimi ni lini twende na mimi nimsubiri ili twende tukaone hicho kijiji chenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri hiyo ilikua ni nafasi ya upendeleo kwako, ungeliniamulia wewe basi ingekua bora zaidi.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku ya leo kufika katika hali ya usalama katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri kajibu majibu mengi sana, lakini kwa kua huko nyuma kulikua na *phase IV* ya umeme. Je, anataka kutwambia hii *phase IV* ya umeme inaendelea au kuna *phase V* na *VI.*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikueleze kwamba ile miradi ya mwanzo yote ile imeshamalizika muda wake, imefanya vizuri, imetekeleza nafikiria mimi na wewe ni mashahidi ambao tumeona. Kwa hivyo, tunataka kuingia katika phase nyengine ambayo itakayomalizia kusambaza umeme katika vijiji vyetu vya Zanzibar.

UTARATIBU

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kanuni ya 41 inaeleza utaratibu wa maswali ya nyongeza sijaona kanuni inayosema maswali ya nyongeza ni matatu. Nilipotaka kumuuliza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, alijenga hoja kwamba maswali matatu yamepita. Lakini mwenzangu tayari amepata maswali manne. Naomba unisaidie utaratibu ni upi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwakilishi kwa mujibu wa kifungu cha 41 cha kanuni mwenye maamuzi ya mwisho juu ya maswali yawe mangapi ni yule anayekaa katika kiti kinachohusika. Kwa hivyo, Mhe. Waziri inawezekana wakati alipokua akizungumza hilo ilikua kuna kipengele labda kimempita kidogo. Kwa hivyo, naomba tustahamiliane katika hilo, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na taarifa yako kama mwenye maamuzi ya mwisho ni kiti na sio Waziri muhusika. Kwa hivyo, Waziri muhusika alijenga hoja na wewe ukamkubalia kwa hiyo nataka kuweka sawa kama mwenye maamuzi ya kuamua ni aliyekalia kiti sio Waziri husika.

Nam. 17

Utalii Haramu Pemba

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Kny: Mohammed Said Mohammed) - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu Serikali imekua ikielezwa kuhusu tatizo la Watalii kutoka Kenya kufika kwenye Hoteli za Kitalii Kaskazini Pemba bila ya kupitia kwenye bandari halali na bila ya kufuata taratibu za uhamiaji na taratibu za kulipa kodi.

Mhe. Waziri, baada ya kushauriwa sana kuhusu hatua za kuondoa tatizo hilo, hatua gani zimechukuliwa na sasa suala hilo likoje.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hizi zimekua zikitolewa mara kwa mara na kwa muda mrefu ambapo Serikali kupitia vyombo mbali mbali imekua ikilifanyia kazi suala hili na kulipatia ufumbuzi muafaka. Hoteli ambayo imekua ikilalamikiwa juu ya suala hili ni *Manta Reef* ambayo sasa inajulikana kwa jina *Manta Resort* iliyoko Panga la Watoro Makangale Mkoa wa Kaskazini Pemba. Takwimu zinaonesha kwamba hoteli hii haijapokea mtalii yeyote moja kwa moja kutoka nchini Kenya kwa njia ya baharini tangu mwaka 2008. Kwa kipindi chote hicho (2008 –

2012) wageni wa hoteli hii wanafika Pemba kwa kupitia Bandari ya Mkoani na Uwanja wa Ndege wa Chake Chake Pemba. Hata hivyo, kwa wale waliokua wakija moja kwa moja kutoka nchini Kenya kabla ya mwaka 2008 walilazimika kufuata taratibu zote za kuingia nchini kisheria.
Mhe. Mwenyekiti, naomba nilieleze Baraza lako tukufu kua mtindo wa kuleta watalii kutoka Kenya kupitia njia za panya ulikua ukifanyika kutokana na ukweli kua kampuni ya *One Earth* iliyokua ikiendesha Hoteli ya *Manta Reef* wakati huo ilikua inamilikiwa na kuendesha hoteli za *Reef* na Shimoni Reef Mombasa, hivyo ilikua ni tija kwao. Hata hivyo, Kampuni hiyo imeondoka na inamilikiwa na Kampuni ya *Manta Ltd* ambapo jina la Hoteli hiyo sasa ni *Manta Resort* ambao sasa wanafuata utaratibu kama nilivyoeleza kabla.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada zote hizo Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi mbali mbali katika kuhakikisha sheria na taratibu za nchi zinafuatwa ili kuimarisha mapato yanayotokana na biashara ya utalii hapa Zanzibar.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, ni wa Kenya wangapi wanaofanya kazi katika mahoteli ya hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nitakupatia takwimu hii kwa maandishi.

Nam. 68
Tabu ya Usafiri Kati ya Unguja na Pemba

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza:-
Baada ya kutengenezwa M.V. Maendeleo na kuanza kazi ya kusafiri baina ya Unguja na Pemba limejitokeza wimbi la mapapasi kuipigia kampeni mbaya meli hiyo kua ni mbovu na haifai kusafirisha abiria.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili limefika Wizarani kwako na mnalichukuliaje.

(b) Kuna taarifa kiwango cha abiria katika Meli ya MV Maendeleo ni 400 tu. Ukilinganisha na ukubwa wa meli hiyo na boti nyengine za kawaida, abiria hao ni wachache. Kuna sababu gani za msingi kuwekwa idadi hiyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano haina taarifa juu ya suala la mapapasi kuipigia Kampeni mbaya meli ya MV Maendeleo baada ya kutengenezwa. Mhe. Mwenyekiti, meli ya MV. Maendeleo ilinunuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1980 na wakati huo ilikua inachukua abiria 484 na mizigo isiyozidi tani 700. Meli hii sasa ina umri wa miaka 32, kiwango au idadi ya abiria wanaoruhusiwa katika meli ya abiria inatolewa baada ya meli husika kufanyiwa *inclinations test* au *inclining experiment.* Matokeo ya hatua hii yanaambatanishwa pamoja na taarifa nyengine, na yanahifadhiwa katika kitabu maalumu kinachoitwa *stability book*. Katika *stability book* ya M.V. Maendeleo inaoneshwa kwamba meli hiyo sasa ina uwezo wa kubeba abiria wasiozidi 454. Hivyo basi, Mamlaka ya Usafiri imetoa ruhusa kwa M.V. Maendeleo kubeba abiria 454.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri aniambie meli hiyo imerudi lini matengenezo na inategemewa kwenda lini matengenezo ili kuondosha uovu wa mapapasi hao.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Meli ya M.V. Maendeleo mara ya mwisho ilipofanyiwa matengenezo imerejea hapa Mwezi wa Januari, 2012, sasa hivi meli hiyo imeharibika, tunaangalia uwezekano wa kupata fedha ili ikatengenezwe tena.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika kujibu swali hili amesema kuwa meli hii hivi sasa ina umri wa miaka 32, kwa vyovyote meli hii ni mbovu. Kwa nini Mhe. Waziri haoni kuwa ni bora hii meli kuiuza zikapatikana pesa za kutafuta meli nyengine kuliko kusubiri ikatokea kama ilivyotokea kwa M.V. Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Meli ya M.V. Maendeleo ina miaka 32 ni chakavu na kweli inafanyiwa matengenezo mara kwa mara. Nalichukua wazo lake kutafakari ili tuone kama Serikali itafanya maamuzi ya kuuza meli hiyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amekiri kwamba meli hii imekuwa ikienda matengenezo mara kwa mara. Je, anaweza akatwambia kwamba ndani ya miaka mitatu meli hii imekwenda Mombasa mara ngapi na imetumia shilingi ngapi.

Lakini pili, haoni kwamba ubovu huo unaoendelea umesababishwa na wizara yake kukaidi maelekezo ya bodi ya shirika kwamba iuzwe itafutwe meli nyengine.
Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Aprili hii tukirudi nyuma (Aprili iliyopita mpaka hii tuliyonayo) meli hii imekwenda matengenezoni mara tatu.

Mhe. Mwenyekiti, miaka 32 kwa chombo ambacho kilikuwa kinafanya kazi usiku na mchana ni muda mrefu, na ni kichakavu kama nilivyosema, ndio maana sasa hivi tunatunga kanuni na tunataka kuleta marekebisho ya sheria ili meli zitakazoingia nchi hii zisizidi miaka 20. Kwa hivyo, nakubali kabisa kwamba meli hii ni chakavu na inahitaji matengenezo ya mara kwa mara, serikali haimudu gharama hizo. Kwa hivyo, ni wakati muafaka kwa serikali kutafakari namna ya kufanya, ama kuuza au kufanya vyengine kama ambavyo ilifanywa Meli ya M.V. Mapinduzi.

Nam. 78
Ununuzi wa Karafuu

Mhe. Salim Abdulla Hamad - Aliuliza :-

(a) Katika msimu huu wizara imenunua tani ngapi za karafuu na matarajio yalikuwa kununua tani ngapi.

(b) Ni jimbo gani lililouza karafuu serikalini kwa wingi zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 22/03/2012, serikali ilishanunua jumla ya tani 4,739.412 zenye thamani ya fedha za Kitanzania Bilioni 70, milioni 848, laki 6 na 37 elfu, sawa na asilimia 157.98 ya lengo ililojiwekea.

Aidha Mhe. Mwenyekiti, katika msimu wa uvunaji karafuu wa mwaka 2011-2012 serikali iliweka lengo la kununua tani 3000 kwa mchanganuo ufuatao;

Wilaya	**Tani**
Mkoani	1,025
Chake Chake	622
Wete	738
Micheweni	385
Unguja (wilaya zote)	230

b) Mhe. Mwenyekiti, takwimu za makadirio ya uzalishaji na ununuzi wa karafuu zimetayarishwa kiwilaya. Kadhalika ili kufuatilia utekelezaji wa lengo hilo takwimu nazo za uvunaji zimewekwa kiwilaya, hivyo takwimu zilizoandaliwa ziko kwa ngazi ya wilaya na sio kijimbo. Wilaya ya Wete ndio iliuza karafuu kama nilivyotangulia kusema Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tunaweka kiwilaya

basi Wilaya ya Wete inaongoza ambapo jumla ya tani 1 577.267 zenye thamani ya 23, 624, 119,760 zimenunuliwa, ikifuatiwa na Wilaya ya Mkoani tani 1262.340 zenye thamani ya fedha za Kitanzania 18, 792, 674,750.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa jibu lake ambalo ni la kuridhisha na la kutosheleza kabisa. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa inaonesha wazi kuwa safari hii Shirika la Biashara limenunua zaidi ya karafuu kuliko walivyowakifikiria au kuliko kiwango walichojiwekea.

a) Je, Mhe. Waziri anaweza akanieleza ni sababu zipi hasa zilizosababisha karafuu kuweza kununua kwa wingi kiasi hicho.

b) Kwa sababu wizara hii na naipongeza ilifanya kila juhudi ya kuona kuwa karafuu popote zilipo zinafika katika vituo kwa kununuliwa, ikiwa ni pamoja na kutengeneza barabara kwa njia ya kufanya *grading*, na kwa sababu ununuzi wa karafuu utakuwa kila mwaka ukiendelea. Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na kwa sababu wizara hii imeshatumia pesa nyingi sana kwa utengenezaji wa barabara. Je, wana mpango gani wa kuona zile barabara ambazo wameshazitengeneza zinatiwa angalau kifusi ili kwa msimu ujao ziweze kufanya kazi vizuri na kushughulikia nyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli lengo tulilojiwekea limepitiliza na limepitiliza kwa sababu kama nilivyokwisha kujibu katika swali lililoulizwa Nam. 22, ni mashirikiano makubwa tuliyoyapata kutokana na wakulima wetu, lakini pia mikakati iliyowekwa na serikali katika kuhakikisha kwamba safari hii tunanyanyua hadhi ya zao la karafuu.Lakini zaidi Mhe. Mwenyekiti, ni kupambana na magendo ya karafuu.Sababu hizi zimepelekea kuongezeka kwa manunuzi ya karafuu hapa nchini.

Mhe.Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba uchumi wa nchi yetu unategemea zaidi pamoja na mambo mengine, lakini karafuu. Sasa kuelekeza fedha zote zinazotokana na zao la karafuu katika kuimarisha peke yake, itakuwa sekta nyengine hazijatendewa haki. Kwa kuwa serikali inafahamu sekta nyengine nazo pia zinahitaji kufanyiwa kazi Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Mawasiliano amesikia na nina hakika atapigania barabara hizo kwa sababu wakati wizara yake itakapowasilisha bajeti, na ni Baraza hili ambalo linapitisha bajeti hiyo, basi tutategemea mashirikiano na Wajumbe wa Baraza lako katika kuelekeza serikali ni vipi fedha zigaiwe katika mgawanyo wa kisekta ili kuendeleza sekta zote kwa pamoja na isiwe barabara peke yake.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe.Mwenyekiti, kunipa fursa kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa naipongeza sana wizara hii kwa kununua karafuu nyingi na kuongeza bei kwa wananchi ili kufaidisha walimaji wa karafuu. Sasa kwa kuwa karafuu zilizonunuliwa ni nyingi sana na zimepindukia matarajio yaliyokusudiwa zimezidi zaidi, na kwa kuwa fedha zimetumika nyingi zaidi, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri ni tani ngapi za karafuu sasa hivi zimeshauzwa na serikali, na kiasi gani cha fedha kimeshapatikana baada ya mauzo ya karafuu hizo. Vile vile je, wanatarajia kuongeza tena bei kwa kiwango kikubwa zaidi kipindi kinachofuata.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nipokee pongezi za dhati alizotuletea ndani ya wizara kufuatia kununua karafuu nyingi. Ni kweli kufuatia ununuzi wa karafuu hizo, ni pesa nyingi serikali imetumia na ziko mikononi mwa wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya fedha zilizotumika katika ununuzi wa karafuu nimuombe Mhe. Mwakilishi afanye hesabu za haraka haraka jumla ya tani ambazo tumezinunua na kuziuza nje ya nchi kwa kiwango cha wastani. Ununuzi Mhe. Mwenyekiti, ulikuwa ukipanda na kushuka kulingana na mahitaji ya soko la dunia la ununuzi wa karafuu. Lakini wastani kwa kila tani dola 12 elfu basi afanye kwa tani hizo Mhe. Mwakilishi atapata jumla ya fedha ambazo serikali imeweza kupata kwa kuuza nje ya nchi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja lenye sehemu *a* na *b*. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

a) Baada ya hilo sasa naomba nimuulize kwamba, katika majibu yake alisema kuwa karafuu pamoja na mambo mengine lakini ni tegemeo katika uchumi wa nchi yetu. Kama hivyo ndivyo, je, kwa sasa shirika linachangia kiasi gani kama kodi katika serikali.
b) Je, kwa sasa karafuu kwa ujumla inachangia kiasi gani katika pato letu la taifa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Kwanza ningeomba niwafahamishe Wawakilishi na wananchi wote kwamba tumenunua tani 4,726 za karafuu ambazo tumetumia kiasi cha shilingi bilioni 71.6. Vile vile tumenunua makonyo yenye thamani ya shilingi bilioni 1 na milioni 300 kama tani 990, manunuzi yote kwa jumla yanakaribia shilingi bilioni 73 karafuu na makonyo.

Lakini vile vile tumeuza nchi za nje karafuu tani 3700 zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 48 sawa na shilingi bilioni 70 za Kitanzania. Vile vile tunasema kwamba mchango wa zao hili kwa mwaka huu 2011/2012 utakuwa mkubwa lakini bado haujafanywa tathmini yake, tathmini yake hutolewa na Benki Kuu ya Tanzania na tunatarajia katika kipindi kifupi kijacho Benki hiyo itatupa tathmini, lakini mimi nataka niwape tu *indication*.

Kwa mwaka uliopita kulikuwa na nakisi kubwa baina ya uagiziaji na usafirishaji, ilikuwa tumenunua bidhaa kutoka nje zenye thamani ya shilingi bilioni 137, lakini tulisafirisha vitu kutoka Lamu vyenye thamani ya shilingi bilioni 27-28. Kwa mwaka huu nakisi hii itapungua, tunaamini kwamba kwa mara hii baina ya uagiziaji na usafirishaji nakisi itakuwa ndogo sana, lakini takwimu hasa ya kiasi gani itatoka kutoka Benki Kuu na tunaingojea sote ili tuweze kueleza katika vikao vyetu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 41
Ujenzi wa Sekondari za Kisasa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Rashid Seif Suleiman) – Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ujumla kwa ujenzi wa sekondari za kisasa.

(a) Je, skuli hizi zinategemewa kufunguliwa lini.
(b) Walimu watatoka wapi kwa ajili ya kufundisha skuli hizo, na sifa gani za msingi zinazohitajika kwa walimu wa kufundishia skuli hizo..
(c) Kila skuli miongoni mwa skuli hizo ina maabara ngapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 41 lenye kifungu (a) na (b) na kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi kwa heshima yako, naomba kumkaribisha waziri wangu mpya na kumuahidi kwa niaba ya wenzangu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kumpa mashirikiano ya hali ya juu kama ambavyo tulikuwa tukimpa Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban.

Mhe. Mwenyekiti, nia ya Serikali yetu ya Awamu ya Saba ni kuleta maendeleo kwa wananchi wetu wote, na bila ya ushirikiano na umoja maendeleo hayo yatakuwa ni ndoto katika nchi yetu. Sisi Wizara ya Elimu tuna nia na lengo la kuwafundisha watoto wetu au kuwajengea mazingira mazuri kufika katika hilo lengo la serikali. Kwa ushirikiano wa pamoja na nia zetu njema basi tutafikia huko. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Rashid Seif Suleiman swali lake Nam. 41 lenye vifungu a na b.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imejenga Skuli za Sekondari 19 katika Wilaya zetu zote za Unguja na Pemba. Vile vile skuli 6 za sekondari kwa skuli tatu za Unguja na tatu Pemba zimefanyiwa ukarabati mkubwa. Aidha, kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatarajia kujenga skuli mbili za kisasa; moja katika Wilaya ya Kusini Unguja na nyengine Wilaya ya Mkoani Pemba. Ujenzi wa skuli 13, kati ya hizo skuli 8 za Pemba na skuli tano za Unguja umemalizika kwa asilimia 98, na kazi za uchongaji wa samani na kuingiza mitungi ya gesi kwa ajili ya maabara zinaendelea.

Ukarabati wa skuli nne, mbili Unguja na mbili Pemba unaendelea vile vile. Pia, kazi za ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Paje Mtule, Tunguu na Dimani unaendelea vizuri. Utiaji wa saini wa mkataba wa ujenzi wa skuli tatu za ghorofa katika Mkoa wa Mjini Magharibi umefanyika tarehe 14 Machi, 2012 na wakandarasi watakabidhiwa rasmi maeneo ya ujenzi mwezi mmoja tokea kutiliana saini mkataba huo. Zabuni zilizotangazwa upya za ukarabati

wa Skuli za Sekondari za Uweleni, Pemba na Hamamni Unguja hivi sasa ziko katika hatua ya kufanyiwa tathmini, na mkandarasi atapatikana baada ya kukamilika kwa tathmini hiyo.

Kuhusu skuli 2 za sekondari zinazogharamiwa na *BADEA*, tathmini ya zabuni imeshawasilishwa *BADEA* na kupatiwa maamuzi ya mwisho, na ni mategemeo yetu kuwa mkataba wa ujenzi wa skuli hizo utatiwa saini katika mwezi wa Aprili 2012. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali kama hivi ifuatavyo :-

(a) Skuli za Sekondari 13 mpya za Uzini, Dole, Chaani, Matemwe na Mwanda kwa Unguja na Pandani, Chwaka, Tumbe, Utaani, Konde, Shamiani, Wawi, Kiwani na Ngwachani kwa Pemba zinategemewa kufunguliwa katika mwezi wa Aprili, 2012 mara samani za skuli hizo zitakapokamilika.

(b) Hivi sasa, kibali cha uajiri wa walimu wapya wenye shahada na stashahada 240 kimeshapatikana kutoka Tume ya Utumishi Serikalini. Hatua za kuwaajiri walimu hao hivi sasa zinaendelea. Baadhi ya walimu hao watapangiwa kusomesha katika skuli mpya, pia wizara inatarajia kupata walimu 10 wa masomo ya sayansi na hesabati kutoka Nigeria. Walimu hao nao pia watapangiwa kusomesha katika baadhi ya skuli za sekodnari hizi mpya. Pamoja na walimu hao wapya, wizara pia itawapangia baadhi ya walimu wenye uzoefu kufundisha katika skuli hizo mpya. Hata hivyo, naomba kukiri kuwa pamoja na kupatikana kwa walimu hao, bado mahitaji ya walimu ni makubwa sana.

(c) Mhe. Mwenyekiti, skuli zote zina maabara tatu za masomo ya sayansi, Fizikia, Kemia, na Biolojia na chumba cha mafunzo ya kompyuta. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub : Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza vile vile nimpongeze Naibu Waziri kwa kupata bosi mpya. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali alitaja Skuli ya Mtule na skuli hiyo iko katika Jimbo la Muyuni, na hivi sasa karibu mwaka mmoja na nusu hakuna kinachoendelea. Ni sababu zipi za msingi zilizosababisha ujenzi ule kusimama na haoni kuwa ni hasara kwa walinzi kukaa pale kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Menyekiti, sikumsikia vizuri Mhe. Mjumbe, naomba aniulize tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa kupata bosi mpya. Pili, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali alitaja Skuli ya Mtule na skuli hiyo iko katika Jimbo la Muyuni, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha jengo lile kusimama karibu mwaka mmoja na nusu hakuna kinachoendelea na kuwepo walinzi tu kwa muda mrefu kupoteza pesa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba skuli ya Mtule, Tunguu na Dimani ujenzi wake ulizorota. Ijapokuwa Mhe. Mwenyekiti, mjengaji huyu ndie mjengaji wa kwanza ambaye tulitiliana nae saini, lakini ujengaji wake kidogo umekuwa ni wa taratibu mno.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alikuwa na ziara ya kutembelea hizi skuli zetu na tulifika kule Mtule tukaona namna ujengaji ule unavyokwenda. Tumekubaliana na mjenzi na tumewekeana tarehe ya mwisho, iwapo itafika tarehe hiyo atakuwa hajamaliza kwa sababu alisema matatizo aliyokuwanayo ni ule uongozi wa ujenzi uliokuwepo pale.

Hivi sasa kaweka msimamizi mwengine wa ujenzi na akataka tumpe muda, kwa hivyo tumempa muda ule na utakapofika muda ule ikawa mjenzi yule hakumaliza kazi zake basi tutavunja mkataba na yeye na hatua za kisheria nyengine zitafuata.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita Mhe. Waziri aliwahi kutueleza kuwa skuli hizi zitakuwa za wilaya, ni kusema kuwa zitachukua wanafunzi wa wilaya nzima. Je, ni skuli ngapi ambazo tayari zina dakhalia kwa ajili ya wanafunzi wa kulala.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mhe. Suleiman Hemed Khamis kwamba nia ya skuli zile ni skuli za wilaya na wanafunzi wote ambao watatoka wilaya husika basi watakuwa wanasoma skuli zile.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, tulikusudia wale wanafunzi *cream* ambao wanatoka katika wilaya husika ndio tuwapeleke katika skuli zile kwa sababu ni skuli za kisasa ambazo pia zitakuwa zinachukua wanafunzi wachache kwa darasa hawatozidi wanafunzi 40. Lakini zaidi ya hilo ni kuwa huduma zote za usomeshaji na maabara zitakuwepo pale.

Lakini wakati tulipotia saini yetu ya mwanzo na watu wetu hawa wa *World Bank* na mpaka tulipoanza kujenga tulichelewa sana. Kwa hivyo, ikabidi hizi gharama za ujengaji zizidi, ikabidi kuna mambo tuyatoe kwanza tuyaweke pembeni.

Mhe. Mwenyekiti, mpaka hivi sasa katika skuli ambazo tunajenga hakuna skuli zenye dakhalia, lakini nia ya wizara yetu ni kuziwekea skuli hizo dakhalia mbili moja ya wanawake na moja ya wanaume.

Hivi sasa tayari tumefanya mazungumzo na wenzetu wa *World Bank* na wametuahidi katika awamu hii ya pili basi skuli zote zile ambazo tulikusudia kujenga dakhalia tutazijenga dakhalia ili wanafunzi wetu ambao wako mbali katika wilaya ile wafaidike na matunda ya skuli hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii Nam. 6 ya 2009
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru muumba wetu Mwenyezi Mungu mtukufu kwa asubuhi hii kutupa fursa ya kukutana tena hapa na kuendelea na mkutano wetu huu. Pili nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa mswada huu asubuhi hii baada ya wenzangu ambao walichangia jana.

Mhe. Mwenyekiti, tatu niipongeze serikali kwa kuona haja ya kuleta mswada huu wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Utalii ya mwaka 2009. Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaingia katika mswada wenyewe kama wanavyofanya wenzangu wengi kutokana na umuhimu wa sekta hii kwa Zanzibar nilikuwa naomba uniruhusu nizungumzie mambo ya ujumla ili yaisaidie wizara. Hivi sasa imepata waziri mpya bila shaka kuna changamoto mpya iyatazame haya kwa makini sana ili tupate tija iliyokusudiwa kutokana na sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, la kwanza katika mambo haya ya jumla nilikuwa nadhani ni muhimu kuwa serikali na sisi sote kama nchi kwa ujumla kutambua umuhimu ambao tumeipa sekta hii ya utalii. Tumesema sote kwamba kama kuna sekta ambayo tumeipa umuhimu mkubwa sana katika kukuza uchumi wetu basi mojawapo ni sekta ya utalii na kwa hivyo imekuwa ni mchangiaji mkubwa katika pato la taifa.

Lakini kama hivyo ndivyo Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni muhimu sana kuona kwamba tunaipa sekta hii umuhimu mkubwa na tunaikuza na kuiendeleza na isibakie kama ilivyo leo kwamba takriban miaka 20 sasa au zaidi tangu tumefungua milango ya utalii lakini bado tukitazama utekelezaji wake ni wa kiwango cha chini mno ambacho hakilengi kule ambako dira 2020 ya nchi yetu iliyokusudia kwamba kuifanya Zanzibar kuwa ni kituo kikuu cha biashara ya utalii ambayo inalenga katika daraja la kwanza la sekta hii. Hilo bado ni mtihani mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo basi, niiombe serikali ichukue hatua za makusudi kuona vipi inabadilisha utalii wetu kutoka katika utalii ambao unategemea mno watalii wa daraja la chini ambao pamoja na kuambiwa kwamba wanachangia sana kwa sababu ndio wanaotumia sana mitaani na hivyo kuchangia uchumi wa wananchi wetu wa kawaida, lakini ukweli kwamba kiwango chao cha matumizi ni cha chini kwa hivyo hakuna matumizi makubwa ya fedha za kigeni katika nchi yetu yanayofanya kuongeza katika pato la taifa.

Lakini kama ni hivyo Mhe. Mwenyekiti, kama tunataka kuzungumzia kuendeleza utalii wetu kuwa katika hali ya juu ni lazima tuchukue hatua za kuhakikisha nchi yetu inakuwa na vivutio ambavyo vitawafanya watalii wa daraja la juu waweze kuja. Hata haya maadili na mambo mengine ambayo nitayazungumza baadae, haya tutakuta kwamba katika

utalii wa daraja la juu mara nyingi hayaathiriki sana kwa sababu watalii wa daraja la juu wanapoingia katika nchi wanakuwa ni wale ambao wenyewe wanaotoka katika nchi zao. Ni watunzaji wa maadili, wanaheshimu utamaduni wa nchi wanayokwenda, wanakuwa na misingi ya kuja kujionea zaidi maisha ya watu wengine yalivyo duniani na kwa hivyo wakiondoka hawana athari kubwa ambazo wanaziacha kama hawa watalii wa daraja la chini ambao mara nyingi ndio wanaoingia kwa maelfu lakini mapato wanayoyaacha katika nchi ni machache sana.

Mhe. Mwenyekiti, tunayo mifano ya kutazama wala tusiende katika dunia za mbali hapa hapa Afrika katika Bahari ya Hindi. Jirani zetu Seychelles, Mauritius wamefikia hatua kubwa sana katika kukuza utalii wao kufika katika kiwango cha juu. Tutazame basi wenzetu hawa wamechukua hatua zipi zilizowafikisha pale ambazo Zanzibar leo zaidi ya miaka 20 tangu tumefungua milango ya utalii tumeshindwa sisi kuzichukua.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika hili niseme kuna huduma za msingi ambazo watalii wa daraja la juu wanazitazama katika nchi. Kwa mfano, watalii wa aina hii wanategemea kuwe na michezo ya kisasa, wakija wataangalia katika nchi je, kuna maeneo ya kucheza *golf*, kuna maeneo ya kucheza *tennis* katika kiwango cha kimataifa, kuna maeneo ya viwanja vya michezo vya kisasa yanayotoa fursa za watu kuifanya michezo kama ya kuogelea katika *swimming pool* za nchi hiyo. Hayo ndio mambo ambayo yanatazamwa sio *swimming pool* zetu hizi za mitaani katika mahoteli haya madogo madogo ambayo yanajengwa.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, utalii ambao unaongeza mapato ni ule utalii pia unawafanya watalii wa daraja la juu wakiingia waweze kufanya manunuzi makubwa ya bidhaa, yaani kufanya eneo letu kuwa ni *shopping centre*. Dubai imekuwa ni kituo kikubwa sana cha utalii wa aina hii kwa sababu watalii wengi duniani kutoka nchi za magharibi wakiamini ni pahala ambapo unaweza kufanya *shopping*.

Je, Zanzibar imejipanga kiasi gani kuwa na *shopping* mall, *shopping centre* za kisasa na bidhaa za kiwango cha juu ambazo watalii wa daraja hili wakija sio tu kwamba wataishia kwenye mahoteli lakini wataweza kufanya manunuzi makubwa ya bidhaa na kwa hivyo kuongeza biashara katika nchi yetu, lakini pia kuongeza pato linalotokana na kodi ya bidhaa zile ambazo wanazinunua.

Ndio kusema Mhe. Mwenyekiti, yale ambayo nilikuwa nikiyapigia kelele sana serikali iachane na huu mdorongo ilionao katika kupasisha vitega uchumi vingi ambavyo vimeletewa maombi yao ambavyo vitabadilisha na kuweka haya ninayoyazungumza hapa lakini vimekwama mpaka leo kutokana na urasimu mkubwa ambao upo serikali katika ku-*process* na kupitisha miradi hii ambayo imeombwa. Nadhani Mhe. Mwenyekiti, hili ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo juzi alitwambia hapa kwamba kuna miradi mikubwa sana ambayo ipo katika nchi yetu imeombwa lakini sasa ni takriban mwaka mmoja na nusu tangu niingie serikali hii bado mpaka leo tunasuasua katika kuidhinishwa. Kwa hivyo, nadhani hilo ni muhimu sana.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, ni chombo hichi ambacho tunakibadilishia sheria yake Kamisheni ya Utalii inapaswa ibadilike ifanye kazi iliyowekewa ambayo ni kukuza utalii na kuuendeleza. Isifike pahala ikawa Kamisheni ya Utalii ni kamisheni ya wakubwa kugombania safari mpaka wakafika kununiana katika kamisheni kwa sababu kila mmoja anataka kusafiri yeye kwenda nje, ikawa hizi safari sio za kukuza utalii lakini za kuingiza posho mifukoni kwa gharama ya walipa kodi bila ya kuleta tija yoyote iliyokusudiwa. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, niliache hilo moja la jumla kuzungumzia sekta hii ya utalii. Lakini niseme vile vile umuhimu wa sekta hii tutauona tu ikiwa kutakuwa na kitu ambacho katika hayo mabadiliko yake kimeguswa *(link sector).* Vipi tunaiunganisha sekta ya utalii na sekta nyengine za uchumi katika nchi yetu, hapa inaweza kuleta tija katika nchi yetu na kuwafaidisha wananchi.

Kwa mfano, inajulikana sekta ya utalii inatumia bidhaa nyingi sana, lakini leo tutakuta bidhaa nyingi ambazo sekta ya utalii inazitumia zinaagizwa kutoka nje ya nchi. Hata vyakula, mambo kama maziwa, nyama, samaki, hata kuku hawa wote wanaagiziwa kutoka nje. Sasa hawa Wazanzibari ambao wanajishughulisha na uzalishaji katika sekta hizi za mifugo, uvuvi, kilimo, usafirishaji, kuna *link* gani baina ya sekta ya utalii na sekta hizi. Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala kubwa sana katika uchumi, wenzetu wote ambao wanakuwa na sekta moja tu wanayoitegemea wanafanya kuiunganisha sekta ile na sekta nyengine ili tija yake ifikie watu wengi katika nchi.

Hivi sasa tunavyofanya sekta hii inaendelea kuwanufaisha wawekezaji wa nje kuliko kuwanufaisha Wazanzibari wenyewe ambao wako ndani waliokusudiwa. Kwa hivyo, nataka na hili serikali katika mipango yake ya maendeleo ilitazame na juzi tumepitisha Sheria ya Tume ya Mipango moja katika kazi yake ilitazame hilo.
Mhe. Mwenyekiti, hili haliwezi kuwa ni jukumu la Kamati za Utalii za Wilaya, hizi kwa *level* yetu ziko chini sana inahitajika huku kamisheni juu katika mipango ya kitaifa kupitia hii Tume ya Mipango ilione hilo na ilifanye, Kamati za Wilaya zitakapokuja zifanye kazi ya kutekeleza tu yale ambayo yamepangwa katika wilaya zao. Hilo ni muhimu sana Mhe. Mwenyekiti.

La tatu la jumla Mhe. Mwenyekiti, linahusu ajira katika sekta hii. Mhe. Mwenyekiti, kwa vyovyote vile kama nilivyosema sekta hii inategemewa kwa hivyo moja ambalo ilikuwa tulitazame sana ni vipi ajira za sekta hii zinawanufaisha Wazanzibari. Leo ni ukweli usiopingika ninahakika kama tukifanya tathmini ya kikweli kweli zaidi ya asilimia 80 ya walioajiriwa katika sekta ya utalii sana utakuta ni wageni. Mimi ninahakika na hilo Mhe. Mwenyekiti, fanya utafiti. Tunasingiziwa mara nyengine tunaambiwa kwamba kuna kazi Wazanzibari hawazitaki ni kweli, lakini kazi hizi ni asilimia ngapi katika kazi zote za utalii. Ziko kazi nyengine ambazo haziingiliani na hayo maadili hata ya kidini ikibidi je, hizi pia Wazanzibari wanazipata.

Lakini vile vile tusifike pahala pia ikawa kazi hizi kwamba Mzanzibari kazi yake ni zile kazi ndogo ndogo tu, hata katika sehemu ya *management* ya mahoteli haya na mambo mengine yanayohusiana na utalii kiasi gani vijana wetu ambao wamesoma. Leo tuna vyuo vikuu hapa vinatoa wasomi kila siku, kiasi gani wanaajiriwa katika nafasi hizi, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inachukua jukumu gani kusimamia sheria za kazi kuona kwamba hawa watu walioajiriwa ni Wazanzibari katika sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, niseme katika hilo ni muhimu mno kwa hii Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kutobakia ofisini tu ifuatilie mambo haya katika sehemu hizi hasa katika sekta kama hizi za utalii ambazo ni sekta moja kubwa sana ya uchumi wa nchi yetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ajira pia tunapiga kelele hivyo hivyo tukiisikia serikali kuona kwamba inaweka umuhimu mkubwa katika mafunzo. Leo tuna Chuo cha Utalii cha Maruhubi lakini ukenda kukitembelea pale hakitoi hadhi ya wafanyakazi ambao wanategemewa kuweza kuajiriwa katika nafasi kama hizi. Bado kiwango chake ni cha chini mno, hata wewe ukenda kuhudumiwa tu pale Mhe. Mwenyekiti, unaona kwamba kwa huduma hii hata mimi siridhiki seuze mtalii wa daraja la kwanza ambaye tunataka aje katika nchi yetu.

Kwa hivyo, tunahitaji serikali kama kweli inaikubali sekta ya utalii kama ni sekta kubwa isingojee kukusanya mapato katika mahoteli kule lakini ijenge utaratibu wa kuwaandaa vijana wetu kuweza kuingia katika sekta hii na moja ni katika suala hili la mafunzo. Tukichambua haya Mhe. Mwenyekiti, uchumi wetu sisi wa kisiwa ni *service oriented* sio *resource oriented,* sasa kama ni uchumi unategemea huduma moja katika huduma ni sekta kama za utalii mafunzo kiasi gani wanajikita. Lakini katika hilo ajira vile vile isemwe Mhe. Mwenyekiti, sheria zetu na kanuni zake za utalii ziko wazi kwamba kazi za kusafirisha na kutembeza watalii *(travel and tours)* hizi ni faida ya Wazanzibari. Lakini leo tunajua kuna makampuni kwa wingi hapa, kuna mahoteli ambayo hairuhusiki kisheria yamefungua makampuni yake ndani ya makampuni ya hoteli yanayofanya kazi ya *travel* na *tours* kwa hivyo yanawapunguzia nafasi ya kazi zile kuwafikia Wazanzibari wanaofungua makampuni yale. Kwa sababu wao wameshajipanga huko chini ya mfumo wa *package tours* wanakuta Wazanzibari wanashindwa kushindana nao.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, serikali iisimamie sheria hii katika hili kuhakikisha kwamba wenye mahoteli wote ambao wameanzisha huduma ya *travel and tours* huduma hizi zinafungwa mara moja na serikali ili Wazanzibari wenyewe waliokuwa wameanza huduma hii wapate kazi hizi, wapate biashara hizi, wapate kipato kutokana na biashara hii.

Mhe. Mwenyekiti, niseme hapa hapa katika suala la ajira haya mambo ya kuajiri wageni ndio matokeo yake mara nyengine yanatuathiri katika kushindwa kusimamia maadili. Limezungumzwa suala jana na wenzangu hapa na mimi nataka kulisisitiza. Nchi yetu imefedheheka mno kwa kitendo kilichofanyika katika hoteli ya *The Residence* iliyoko Kizimkazi. Mtoto wa kike wa Kizanzibari kufika kuvuliwa nguo zake zote na mkuu anayesimamia mambo ya ulinzi ambaye vyombo vya habari vimeripoti kwamba ni raia wa kigeni ni Mkenya halafu serikali mpaka leo hatujasikia ikisema lolote katika suala hili. Mhe. Mwenyekiti, hii inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, juzi baadhi ya wawakilishi tulipokea ujumbe kutoka Chwaka kuhusiana na masuala tofauti na mambo ya magomvi yao haya kati ya Marumbi na Chwaka. Mmoja alitwambia anasema miaka 10 ya serikali ya awamu ya sita kulikuwa hakuna tatizo lile, lakini wanashangaa tangu ianzishwe Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo ndio walitegemea itoe mfano magomvi yale yameripuka upya na kila siku watu wanaingiliana mwilini. Sasa nilitaka kusema hili nataka kuliunganisha hapa na serikali hii pia ionekane katika kusimamia sheria vile vile.

Hapa katika miaka ya 80 Mhe. Abubakary Khamis Bakary atawakumbuka waliokuwa mawaziri wakati ule ilitokezea kashfa moja katika hoteli ya Bwawani wakati inaongozwa na wale wenye kampuni ya kutoka nadhani Italy. Wakati ule Mhe. Ali Haji Pandu alikuwa ni Waziri wa Utalii alimpiga mtu masaa 24 ikatoka amri kuhamishwa pale pale kuwa ahame Zanzibar aliyefanya kitendo kama kile cha udhalilishaji. Leo mtu kama huyu anafanya vitu kama hivi vinaripotiwa katika vyombo vya habari hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Hii tunapokuwa hatuchukui hatua inapelekea kutoa ujumbe kama vile watu waendelee kufanya mambo kama haya kwa sababu wenyewe wenye nchi tumelala. Sasa kama katika miaka ya 80 Mhe. Mwenyekiti, tumeweza kufanya kwa nini leo tushindwe kusimamia sheria zetu kama hizi. Kwa hivyo, nataka serikali katika hili ichukue hatua kali dhidi ya Mkenya huyu kutoa fundisho kwa wengine kuwa mambo kama haya hatuwezi kuyavumilia.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba taarifa iliyokuwepo ni kwamba huyu mfanyakazi aliyefanya kitendo hichi ile siku ya tukio aliyodaiwa kwamba kulitokezea hivi yeye alikuwa *off* hata hakuwepo kazini siku hiyo. Kwa hivyo, pengine kuna mambo yao huko katika mahoteli watu wanatumia fursa kama hizi kuwaadhibu watu na kuwadhalilisha namna kama hii katika nchi ambayo asilimia 99 ya wananchi wake ni waislam mambo haya hayakubaliki. Lakini hata katika hizo dini nyengine mambo wanayofanyiwa hayakubaliki kwa hivyo nataka serikali ichukue hatua kali.

La mwisho kabisa katika ya jumla Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la mapato ya utalii. Kama tutakubali kwamba sekta ya utalii ni sekta muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu kiasi gani tunayachunga mapato yanayotokana na utalii. Mswada huu umegusa na nitakuja Mhe. Mwenyekiti. Mimi mara nyengine naona hili tatizo la kuwa na vyombo vingi ambavyo vinasimamia mapato nalo ni tatizo.

Kama tumeunda Bodi ya Mapato Zanzibar na tumeipa jukumu la kusimamia suala la mapato basi nadhani tungekuwa na utaratibu ambapo kila penye mapato hasa yale mapato makubwa basi yakawa yanasimamiwa na bodi hii. Lakini ikiwa kuna kamisheni nyengine inakusanya mapato haya, kuna mamlaka haya inakusanya mapato, haya mapato tutaweka mianya ya kuchukuliwa yakenda yakafaidiwa na wachache badala ya kuingia katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika hilo niseme kuna malalamiko mengi sana kwamba kuna uvujaji mkubwa sana wa mapato kutokana na wawekezaji hasa hawa tunaowaamini sana wa kimataifa hawa ndio wanaoongoza katika kukwepa kulipa mapato kwa serikali. Matokeo yake Wazanzibari wanaojenga vijihoteli vidogo vidogo ambao wao ndio tungepaswa tuwape upendeleo na kuwakuza waje waishike sekta hii wao ndio wanaokamuliwa kila siku. Utakuta *inspection* hazishi katika hoteli hizi zilizokuwepo kwa Wazanzibari, lakini ukenda kwa wawekezaji wa kimataifa kunamalizwa mambo huko huko kimya kimya kunafanywa taratibu za aina ya ajabu kabisa katika kukwepa mapato na serikali inafumbia macho.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nadhani hili tulitazame sana tuone haja ya kuwakuza wawekezaji wetu wa ndani na kubana hawa wa nje ambao wanachukua mapato wakenda wakanufaisha katika nchi zao yabakie ndani yahudumie walipa kodi wa nchi hii. Lakini Mhe. Mwenyekiti, vile vile niseme kwamba pia wapo wawekezaji tunawatambua wanatumia mianya hii kuomba misamaha ya kodi kwa wingi sana, wanaleta vitu ambavyo baadae hata havitumiki Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nina mfano wa hoteli ambazo wana hoteli hapa na wana hoteli upande wa pili wa bahari kwa ndugu zetu wa damu. Wanatumia maombi ya *exemption* kwa Zanzibar kuleta vifaa ambavyo unaona kwa idadi yake kwamba hivi haviwezi vikatumika vyote katika hoteli ya Zanzibar, lakini baadae kumeundwa mpaka bandari bubu hapa hapa karibu ya tulipo katika jengo hili kuna hoteli ambayo ina bandari yake pale kabisa, vinatolewa *exemption* vikifika vinapakiwa pale vinamalizikia Kunduchi Dar es Salaam na kuteremshwa pia katika kupitia bandari ambayo si ya kawaida. Serikali itupie macho masuala haya isiwe kuna wakubwa fulani wanafaidika na wenye mahoteli haya wanatumika kuja kuhalalisha kuinyima mapato nchi yetu hili halikubaliki.

Mhe. Mwenyekiti, hayo yalikuwa ya jumla sasa naomba niende katika mswada. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema napongeza marekebisho haya ambayo yameletwa lakini yako maeneo machache ambayo nilikuwa naomba tuyafanyie marekebisho. Niipongeze kamati vile vile kwa kufanya kazi nzuri lakini kama kawaida tunachangia na mawazo zaidi ya hayo.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja naomba niende katika kifungu cha 5 cha mswada hichi kinazungumzia Muundo wa Kamisheni na hili naomba niliseme kabisa kwa ujumla wake. Mimi naona kama vile kuna kujizonga zonga katika suala la muundo wa hii kamisheni.

Mhe. Mwenyekiti, kama tumeiita kamisheni basi kamisheni ni wale makamishna. Sasa huku mbele utakuja kuona kuna kukwepa kutumia neno hili kamisheni kwa ule ujumla wa makamishna.

Hilo kwa mtazamo wangu limetokana kwa sababu tu tumejizonga mno, kuna Mwenyekiti ambaye unasema si mtendaji na unamuwekea kazi ambazo zinaonekana kama vile hayo madaraka pia ya kiutendaji, halafu kuna Katibu Mtendaji, halafu kuna Makamishna. Sasa kuna kama mgongano na mkorogano katika sheria hii, nataka hili suala liwekwe wazi katika hii sheria kwa ujumla.

Lakini nikija katika sheria kifungu cha 5 jana pamezungumzwa maoni hapa kwamba katika makamishna wale (b) (1) na (2) ni watu wamoja kwamba Wadau wa Utalii na Jumuiya ya Watembezaji na Kusafirisha Watalii ni wale kwa wale. Mhe. Mwenyekiti, sio sahihi na nadhani katika marekebisho ambayo kamati imeleta katika kifungu hichi imependekeza pale kwamba kifungu cha 5 (1) (b) (i) isomeke Jumuiya ya wenye Mahoteli.

Mimi nilikuwa naomba tuifanyie marekebisho zaidi tuseme Jumuiya ya wenye Mahoteli. Hawa wana jumuiya yao maana nafikiri Mhe. Waziri analijua ni *Zanzibar Association of Tourism Investors (ZATI),* kuna *ZATI* na *ZATO, ZATI* ni ya wale wawekezaji wa utalii na *ZATO* ni jumuiya ya wanaofanya biashara ya kusafirisha na kutembeza watalii. Kwa hivyo, nadhani ile (i) isomeke jumuiya ya wawekezaji wa sekta ya utalii watoe ile wadau wa utalii iondoke. Kwa maana kutakuwa na wale wawekezaji wenye mahoteli halafu namba (ii) kutakuwa na jumuiya ya watembezaji na wasafirishaji watalii.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, *roman (iv)* mimi naona haikukaa vizuri, huku juu inasomeka "Kamisheni itakuwa na: (a) Mwenyekiti atakayekuwa Mkuu wa Kamisheni kwa muda wote na ambaye atateuliwa na Rais. (b) Makamishna wengine wasiozidi 6 watakaoteuliwa na Waziri." Sasa ukija hapo (iv) inasomeka Mkurugenzi Mipango ya Sera na Utafiti wa Wizara yenye dhamana na Utalii."

Sasa huyu Mhe. Mwenyekiti, hata hateuliwi na Waziri, huyu ni mteuliwa wa Rais. Pili hawezi akaingia katika kundi la kutoka kwa sababu huyu ni Mkurugenzi kishatajwa kwa ajili ya nafasi yake. Nilikuwa nadhani tutofautishe baina ya wale wanaoteuliwa na yule ambaye anaingia kwa nafasi yake, lakini mara nyingi katika kuandika tunakuwa tunafanya makosa kama haya ya kuyajumuisha kwa pamoja. Kwa hivyo, nadhani huyu angewekwa mbali akatajwa kwamba huyu anaingia kwa nafasi yake wale wengine wakatajwa kwamba wanatoka katika zile mamlaka mbali mbali.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikubaliane na waliosema kwamba kile kijifungu kidogo cha *roman (vi)* Mjumbe mwengine yeyote ambaye atakuwa ni mwanamke hata mimi kimenikwaza namna kilivyoandikwa. Maana yake kimefanya hata ile nafasi ya mwanamke ni kwa mtu yeyote tu tena hawa wengine tume-*define* wanatoka wapi. Mimi nilikuwa nadhani hichi kingeondoka badala yake kingekuja kifungu cha jumla ambacho kitasema kwamba katika uteuzi wa hawa watu wote kwa jumla Waziri atazingatia uwiano wa kijinsia bila ya kutaja idadi. Jana walipendekeza watu idadi mimi nadhani tusiseme idadi tuseme tu atakapoteua wote hawa Waziri azingatie uwiano wa kijinsia. Kwa hivyo, atatazama katika jumuiya yake wangapi wawe wanawake wangapi wawe wanaume.

Sasa badala ya huyu mjumbe mmoja mwanamke ambaye katajwa *specifical* ambaye nyinyi mnasema kwamba hatutaji kwa jumla mimi nilikuwa naomba namba (vi) tuongeze mtu mwengine.
Mhe. Mwenyekiti, ukenda katika kifungu cha 23 A kinachozungumzia Kamati za Utalii za Wilaya mle katajwa mtu anayewakilisha taasisi za kidini lakini huku kwenye kamisheni yenyewe mtu wa taasisi za dini hayumo. Sote tunajua kwamba kutokana na mjengeko wa jamii yetu ambayo kwa asilimia 99 ni waislam watu wanapiga kelele mno juu ya namna tunavyotekeleza sera na sekta ya utalii tunavyoiendesha kwa ujumla wake. Sasa nilikuwa nadhani katika hichi chombo cha juu kinachosimamia sera hii ingekuwa ni muhimu kuwa na mtu anayewakilisha taasisi za kidini

kwa upande wa Zanzibar. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani Mhe. Mwenyekiti, hichi cha (vi) yule mjumbe mwanamke tungeweza tukaweka hivyo halafu tukaweka kifungu cha jumla ninachosema katika kuteua wote hao Waziri atazingatia uwiano wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 5 (2) naomba pia katika maoni yangu pengine nitachanganya na kijifungu cha 6 kinachohusu Mwenyekiti. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, mimi napata matatizo makubwa, naona kama vile tunataka kutengeneza utaratibu ambao si wa kawaida. Hii kama ni kamisheni Mhe. Mwenyekiti, mtendaji wake mkuu imeshasemwa ni Katibu Mtendaji na ndio maana tukabadilisha mfumo kutoka kuwa na bodi katika kile chombo tutakapokuwa na makamishna ndio kamisheni yenyewe. Sasa huu utaratibu wa kuja Mwenyekiti ambaye kawekewa utaratibu kama vile Mwenyekiti huyu ni mahsusi, tofauti na wenyeviti wengine wa vyombo vyengine kama hivi, mimi hili siliungi mkono. Naona tunakaribisha kabisa mgongano wa kiutendaji.

Mhe. Mwenyekiti, naona tunakaribisha kabisa mgongano wa kiutendaji. Katika hili tusidanganyane sio jipya hili. Mhe. Mwenyekiti, tusidanganyane, kamisheni hii hii sitaki kutaja majina ya watu palikua na wakati kazi zilikua hazifanyiki kwa mivutano kati ya aliyekua Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa Kamisheni, kila mmoja anajiona yeye mtendaji, kama nilivyosema kubwa utakuta watu wanagombaniana safari tu na maposho. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kuondosha mgongano huu na kuondosha hivi vishawishi na kila mmoja kufanyakazi haziendi badala yake hawaishi ugomvi kwa sababu kila mmoja anataka kupata fursa kutokana na nafasi yake, tuweke mtendaji mmoja tu na ifafanuliwe vyema. Haidhuru katika kuandika imeandikwa mwenyekiti hatokua mtendaji, lakini ukisoma vifungu Mhe. Mwenyekiti, inaonekana kama vile hatujaamua hasa.

Nitatoa mifano Mhe. Mwenyekiti, kwanza *specifically* au kwa mchango mahususi kijifungu cha 5(2) hii mwenyekiti atakua madarakani kwa muda wa miaka 4 kuanzia tarehe ya kuteuliwa. Hapa mimi najiuliza kwa nini miaka 4. Utaratibu mara nyingi tunaambiwa miaka 3, hata katika sheria tulioanza kuzipitisha katika kikao hiki kimeanza, uteuzi mwengi unafanywa kwa miaka 3, kwa nini huyu akapewa miaka 4. Kwa hivyo, nilikua nasema na huyu apewe vile vile miaka 3.
Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 5(3) (2) katika zile sifa za mtu kuteuliwa kua mwenyekiti imeandikwa awe na ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo. Nimeangalia ya Kiingereza inazungumzia *advocacies skills.* Mimi nadhani *advocacies* sio kupigania ni kutetea. Kwa hivyo, tungebadilisha lile neno pale. Kuna mjumbe mmoja aliuliza ni mambo gani. Ilivyokusudiwa ni ule uwezo wa jumla wa ku-*push* au kutetea vitu ili viweze kutekelezwa. Kwa hivyo, nadhani tukitumia neno hilo kutetea itakaa vizuri.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia nitahadharishe, katika kijifungu cha 5(3)(4) ambacho kiko kwenye ukurasa wa 43 juu pale, kwamba katika sifa zake imaandikwa awe na taaluma nyengine inayoendana na hiyo ambayo ni muhimu katika sekta ya utalii Zanzibar. Tukitizama katika mswada wa Kiingereza kifungu hiki kimeachwa hakimo. Kwa hivyo, niwatanabahishe tu, watakapokuja ku- *synchronize* waone haja ya kuja kukiingiza katika Kiingereza hiki kifungu cha *roman IV* kule katika Kiingereza kimeachwa kabisa hakimo.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kifungu cha 6, tunasema mwenyekiti sio mtendaji, lakini hebu tukisome namna kilivyoandikwa hiki kifungu. Kwanza kifungu cha 6(1) (a) kazi za mwenyekiti hizi, kinasema kutoa maelekezo ya mikakati kwa uongozi katika kuendeleza na kukuza biashara ya utalii. Ukishamfanya mwenyekiti kwa nafasi yake, sio kama sehemu ya chombo cha kamisheni, lakini kwa nafasi yake kwamba ana uwezo wa kutoa maelekezo, basi Mhe. Mwenyekiti huyu mwenyekiti atampa maelekezo mpaka katibu mtendaji. Kwa hivyo, wewe unaposema kwamba sio mtendaji unayapangua mwenyewe hapa katika kifungu hiki.

Vile vile twende katika kifungu cha 6(1) (c), kinasema kusimamia utekelezaji wa sera ya utalii na kutoa miongozo kwa uongozi juu ya utekelezaji wa sera hii. Pale pale tunarudi Mhe. Mwenyekiti, akitoa miongozo tunampa madaraka ya kiutendaji. Tuondoke hapo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo kwenye kifungu cha 6(1) (e) kinasema, kushauri na kuchukua hatua za kuanzisha mikakati kwa lengo la kuwashajihisha wananchi katika kujihusisha na biashara ya utalii ili waweze kujipatia manufaa kutokana na utalii. Mhe. Mwenyekiti, vifungu hivi vilivyowekwa vitasababisha mgongano wa moja kwa moja, ingekua maamuzi haya ni kazi za jumla za kamisheni ambapo yeye ni mwenyekiti wake kama chombo, sawa. Lakini ukimtaja yeye ambapo katika vyombo vyengine hakuna utaratibu kama huu wa mwenyekiti kupangiwa kazi kama hivi, basi unakaribisha migongano ya wazi na katibu mtendaji.

Pia Mhe. Mwenyekiti, katika kile kifungu cha mwisho cha 6(1) (f) kile ndio balaa zaidi, kinasema, kufanya jambo jengine lolote ambalo linakwenda sambamba au linaendana na majukumu yake ya jumla. Hapa Mhe. Mwenyekiti, ukitoa mwamvuli kama huu, basi unakaribisha kabisa kwamba atajitwika jukumu lolote na atasema hili linaendana sambamba na majukumu yangu. Kwa hivyo, nilikua nasema Mhe.Mwenyekiti, hiki kifungu kwa mtazamo wangu kiondoke, kiwe kifungu cha jumla ambacho kinazungumza kazi zake za kwamba kama ataongoza vikao na kuna lile jukumu linalosema pale kwamba ataongoza mkutano wa kamisheni na wadau wa sekta ya utalii. Yale ni majukumu ya kawaida ni *ceremonial* ni *amoral* kuliko majukumu ya kiutendaji ambayo yametajwa katika kifungu cha 6 cha mswada huu. Kwa hivyo naona hiki kifungu cha 6 tukiangalie sana ili tusikaribishe mgongano.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hiyo hiyo kifungu cha 6(4) kinazungumzia mshahara na mafao ya mwenyekiti baada ya kumaliza kazi yatakua kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma nambari 2 ya mwaka 2011 kulingana na masharti ya uteuzi wake. Ukishasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, tayari unaainisha kwamba huyu sio mwenyekiti kama wenyeviti wengine. Mimi nadhani hatupaswi kumlipa mshahara mwenyekiti wa kamisheni hii, huyu ni mwenyekiti wa kamisheni ambaye anahudhuria vikao alipwe posho kama wanavyolipwa watu wengine. Lakini suala la kuwapa mshahara tena kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma, huyu tunamfanya anakua sawa sawa na mtumishi mwengine yeyote wa umma. Suala hili silikubali Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa suala hili namuomba Mhe.Waziri kabisa, ili asije akatupitisha akataka tuliondoshe kwa kura, naomba akija aturidhie kwamba hili tuliondoshe kabisa kwamba mwenyekiti huyu aje awe mwenyekiti kama mwenyekiti wa vyombo vyengine vyote kama hivi ilivyo ili kuondosha mgongano huu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye kifungu cha 7 ambacho kinazungumzia makamishna, lakini kinazungumzia makamishna kwa nafasi yao, hakizungumzi makamishna kama kwa umoja wao wanaunda chombo sasa cha kamisheni wanakuwa kamisheni. Hiyo nadhani ni kwa sababu ile tuliyosema mwanzo kwamba tumemuweka mwenyekiti na madaraka yake katibu mtendaji, tukiwatambua hawa wote na mwenyekiti wao kwa pamoja ndio kamisheni, basi tungeweka vizuri zaidi kwamba haya majukumu ni ya kamisheni. Kwa hivyo, itakua ni majukumu yao kwa ujumla na pia majukumu yao kama kamishna mmoja mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, nilikua nasema pamoja na marekebisho hayo na ya lugha ambayo ningependa yafanyike ili isomeke kua hii ni kamisheni, lakini pia uandishi. Kifungu cha 7(1) (a) kinasema, washauri wa wakuu wa serikali na uongozi wa kamisheni, hii inachanganya mno. Nilikua nadhani hawa ni kua washauri wakuu wa serikali na uongozi wa kamisheni, lile neno ‘wa’ pale liondoke. Vile vile katika kijifungu cha 7(1) (d) kilichoko katika ukurasa wa 44 kimeandikwa pale, kutoa miongozo kwa ujumla katika uongozi wa kamisheni na wadau wa utalii. Pia haikai vizuri. Kwa hivyo, isomeke kutoa miongozo ya ujumla kwa uongozi wa kamisheni na wadau wa utalii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika kifungu cha 8, kinachohusu vikao vya makamishna. Kifungu cha 8 kinafutwa na kukiandika upya kifungu cha 8 cha sheria hiyo mama. Hapa hoja yangu moja kwanza hatujasema popote kwamba nani anaitisha vikao hivi vya kamishna, panazungumzwa vikao, lakini nani anaitisha haijasemwa na hata ukiangalia kule mbele katibu mtendaji haijasemwa katika madaraka yake ni pamoja na kuitisha vikao vya kamisheni, nilikua nadhani lingewekwa wazi kabisa.

Pili Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema, nadhani kwa ujumla wake ingetajwa sio vikao vya makamishna ni vikao vya kamisheni kwamba hawa makamishna kwa ujumla wao na katibu mtendaji ambaye keshatajwa kule mbele anashiriki vikao hivi na mwenyekiti wanaunda kamisheni, kwa hivyo vikao ni vya kamisheni sio vya makamishna kama vile wana vikao vyao kama makamishna ni kikao cha taasisi sio cha wao kama *individuals*. Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye kifungu cha 9, hoja yangu ni ile ile, tunaandika uamuzi wa makamishna. Mhe. Mwenyekiti, huu ni uamuzi wa kamisheni, hawa wakikaa ndio kamisheni sio makamishna. Nadhani iandikwe vizuri isomeke hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika kifungu cha 12 cha mswada ambacho kinarekebisha kifungu cha 11 cha sheria mama, kina kifuta na kukiandika upya kifungu cha 11. Kifungu cha 11(2) (a) mimi nilikua nataka nitahadharishe tu katika sifa zilizotajwa za mtu kua katibu mtendaji zilitajwa awe na angalau shahada ya kwanza ilivyoandikwa hapa, au elimu inayolindana na hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, hii au elimu inayolingana na hiyo ni jambo linalokubalika kokote, lakini mara nyengine hua tunatumia mianya kama hii kuchagua watu wasiokua na sifa. Kwa hivyo, nilikua nataka kutahadharisha sana hili,

kwamba ama tuiondoshe au kama inawekwa basi iandikwe katika lugha ya kwamba elimu inayolingana na elimu ya chuo kikuu. Kwa sababu mara nyengine inasema tunateua watu kwa mapenzi fulani tuliyonayo au pengine usuhuba fulani halafu tunasema kwamba kutokana na uzoefu wake alionao huu ujuzi wake unalingana na elimu ya shahada, mimi hilo silikubali. Vile vile kifungu cha (b) pale kwenye mstari wa 3, awe na taaluma ya kutosha na uzoefu katika masuala ya utalii au usimamizi wa biashara, au uchumi au masuala ya sheria na awe mweledi na mambo ya uongozi. Nadhani hapa awe mweledi wa mambo ya uongozi.

Mhe. Mwenyekiti, pia kifungu cha 11(3) (a) kimesema, katibu mtendaji atakua mkuu wa sekretarieti ya kamisheni. Inaendelea mpaka kijifungu cha (f). Kwa hivyo, nilikua naomba tuongeze pale mmoja wapo atakua ndio mwenye dhamana ya kuitisha vikao vya kamisheni ili ikae wazi kabisa kwamba huyu ndiye atapewa dhamana hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye kifungu cha 13 cha mswada ambacho kinarekebisha sheria mama kwa kuongeza kifungu kipya cha 11(A) (4) kinasema, "kwa kufuata kanuni zitakazotungwa na waziri kuhusiana na utaratibu wa kufanyakazi wa mkutano wa wadau, mkutano huo unaweza kujipangia taratibu zake wenyewe".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikua najiuliza tuamue moja, ama tunampa waziri jukumu la kuweka kanuni za mkutano huu wa wadau wa utalii au tuupe mkutano madaraka ya kutunga hizo kanuni. Lakini tukianza kuyagawa katika sehemu mbili basi tutakua tunasababisha mgongano ambao hauna sababu yoyote.

Naondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nakwenda katika kifungu cha 16 cha mswada. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinarekebisha kifungu cha 14 cha sheria mama, kwa kufuta neno 'bodi' na badala yake kuweka neno'mwenyekiti'. Ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, katika hili jadweli ambalo tumepewa linaloonesha vifungu vilivyorekebishwa na namna vitakavyokua. Kifungu hiki cha 14 kinazungumzia, mwanzo kilikua kinasema hivi, bodi sio zaidi ya miezi 3 kabla ya kufungwa mwaka wa fedha, itawasilisha kwa waziri taarifa ya mwaka juu ya kazi za kamisheni na taarifa ya ukaguzi kwa mwaka huu wa fedha.

Sasa hivi marekebisho yanaondoa bodi yanaweka mwenyekiti. Ndio nasema ukiweka hivyo unarudi kule kule unampa mamlaka mwenyekiti kua na madaraka ya kiutendaji. Mimi nadhani nikatae marekebisho haya yanayosema, badala ya neno 'bodi' tusiweke neno 'mwenyekiti' ila tuweke neno 'kamisheni'. Yaani sio zaidi ya miaka 3 kabla ya kufungwa mwaka wa fedha, itawasilisha kwa waziri taarifa ya mwaka juu ya kazi za kamisheni na taarifa ya ukaguzi kwa mwaka huu wa fedha. Tukisema hivyo, tutakua tumeipa kazi hiki chombo cha kamisheni na sio mtu mmoja ambaye anaweza akajitolewa madaraka ya kiutendaji.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 17 cha mswada kinachorekebisha kifungu cha 15. Hapa nataka kutoa indhari tu ambayo nimeshaisema katika mchango wangu wa jumla pale mapema. Mhe. Mwenyekiti, tunapotoa nafasi kwamba kamisheni ndio inayotoa leseni ya biashara, basi tunatoa mwanya wa mapato haya kusimamiwa na vyombo vingi. Mimi nadhani tungekua na mamlaka moja ambayo inasimamia hii. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hizi sheria kila inayokuja inanyang'anya mamlaka ya kutoa leseni ya biashara kutoka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaipeleka kwenye sekta husika, matokeo yake tumefikisha pale idara ya biashara haina mamlaka ya kutoa leseni yoyote sasa. Kila leseni zimeshachukuliwa zimepelekwa katika chombo kingine. Sasa najiuliza hii Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inasimamia nini. Nadhani na suala hili serikali iliangalie sana.

Kwa hoja hiyo hiyo Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 18 cha mswada ambacho pia kinazungumzia mambo hayo ya leseni, nadhani ingefaa serikali ituambie kwa nini masuala ya kusimamia mambo haya ya leseni yasisimamiwe na chombo kimoja na mapato yake yakakusunywa kupitia mamlaka ya mapato ya Zanzibar, ambapo kila siku tunaipongeza kwa kufanya kazi nzuri ya kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika kifungu cha 21 cha mswada ambacho kinarekebisha sheria mama kwa kuongeza kifungu kipya cha 19(A). Mhe. Mwenyekiti, kifungu hicho, maoni yangu yako hapa. Kifungu hiki cha 19(A) (1) kinasema, mtu aliyeruhusiwa kufanya biashara ya utalii, hatofanya mabadiliko katika ofisi yake au jengo, wanahisa, au wakurugenzi, jina la biashara au huduma wanayoitoa mpaka wawasilishe kwa kamisheni maelezo ya mapendekezo ya mabadiliko au marekebisho yaliyokusudiwa kwa maandishi. Sasa mimi hapa nimepata tabu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyojua mambo haya, ikiwa kuna mabadiliko katika ofisi au jengo kuna wizara ya majenzi inayoshughulika na masuala haya, ambayo inapaswa kusimamia mambo haya, kwa nini tuipe kamisheni. Lakini kama ni masuala ambayo yanahusu wanahisa wakurugenzi mambo haya yanasimamiwa na sheria za makampuni au sheria za kampuni na Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ina sehemu yake ambayo inashughulikia na kusajili makampuni. Sasa kama kuna mabadiliko ya wanahisa wakurugenzi, kwa nini mpaka irudishiwe ile kamisheni isisimamiwe kule kule na Ofisi ya Mrajis Mkuu ambayo ndio inayosimamia masuala ya kusajili makampuni. Suala hili mimi sikubaliani nalo, naona kama tunachukua madaraka mengi tunapeleka katika kamisheni, badala ya kuyabakisha katika sehemu zake ambazo zinahusika.

Mhe. Mwenyekiti: Tunadakika mbili zimebaki Mhe. Mjumbe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, naomba niende haraka nitumie hizo dakika zako ulizonipa niende kwenye kifungu cha 23(A) ambacho kimeongezwa na kifungu cha 22 cha mswada, kiko katika ukurasa wa 48 wa mswada. Kifungu hiki kinahusu kamati za utalii za wilaya. Mhe. Mwenyekiti, katika wajumbe wa kamati za wilaya, mkuu wa wilaya hakutajwa. Lakini huku mbele tunasema mkuu wa wilaya ndio atakayeviongoza vikao hivi. Pia katika marekebisho ya kamati yamependekeza kwamba hawa wajumbe wateuliwe na waziri kwa kushauriana na mkuu wa wilaya. Sasa nilikua nasema katika orodha ya wajumbe mkuu wa wilaya pia aorodheshwe.

Pia niseme suala moja vile vile. Hivi vijifungu vidogo (d) na (c) vimeandikwa tu, mfanyabiashara katika wilaya, mkulima katika wilaya. Nilikua najiuliza kwamba kwa nini hatuelezi kama kule kwengine kwamba ni mfanyabiashara mmoja katika wilaya, mkulima mmoja katika wilaya, kama ilivyotajwa kule kwengine.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri akija aje anisaidie kuanzia kijifungu cha (g) na (h) hawa waliotoka katika wizara, mtu mmoja kutoka wizara ya ardhi. Je, kutoka makao makuu ya wizara au kutoka katika wilaya na katika wilaya je wako maafisa wa wizara hizi ambao wako katika ofisi ya wilaya ambao ndio wataingia katika kamati hizi, nilikua naomba hili liwekwe wazi kabisa. Hayo ndio niliyaona muhimu Mhe. Mwenyekiti.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika kijifungu (j) imeandikwa viongozi wa dini katika wilaya, huku juu kote kumeelezwa kua ni mmoja mmoja. Nadhani hapa pia ingeandikwa kiongozi mmoja wa dini katika wilaya, ili tusije tukatoa mwanya wakawa ni wengi, hii kamati ikawa imepanuka sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika kijifungu pia kilichoongezwa cha 23(B) ambacho kinaanza kwenye ukurasa wa 48 na kumalizia ukurasa wa 49. Maoni yangu yako katika kijifungu cha 23(B)(1)(c) kiko ukurasa wa 49 juu pale, kinazungumzia kuanzisha mfuko wa fedha wa wananchi kwa njia ya michango ya hiyari, ambazo zitatumika kwa maendeleo ya vijiji. Mhe. Mwenyekiti, hili neno 'hiyari' linanikwaza. Katika nchi za wenzetu ambazo kuna madini, kuna matakwa kwamba yale maeneo ambapo wawekezaji wa madini wananufaika nayo, basi watenge kiasi fulani cha fedha kwa maendeleo ya maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, sasa sisi kwetu hatuna madini, tunasubiri mafuta *Inshaallah* mpaka ndugu zetu wa damu watakapoamua kuturuhusu tutachimba. Lakini kwa sasa sekta ya utalii tunasema ndio sekta kubwa, nilidhani yale maeneo ambayo kuna sekta ya utalii na ambayo yameathirika mno kwa kufanyiwa biashara ile, basi inapaswa wale wawekezaji pale sio kwa hiyari, watakiwe na sheria hasa kutenga kiasi fulani cha mapato na mimi nilisema angalau pengine asilimia 3 ya mapato hayo yachangie katika maendeleo ya maeneo yale ambayo wanafanyia biashara ya utalii.
Mhe. Mwenyekiti, nimalizie haraka kijifungu (f) cha kifungu hicho hicho. Hapa imeandikwa kulinda sifa ya kimaadili katika wilaya. Mimi nadhani ili kingeandikika vizuri, basi kisomeke, "kulinda maadili katika wilaya halafu tuongeze maneno kwa kuweka taratibu zitakazo hakikisha biashara ya utalii haitumiki kuharibu maadili hayo"

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kijifungu cha (g) kimeandikwa kwamba 'kamati itakua kama kiungo baina ya utalii na sekta nyenginezo, ndio ile *link sector* niliyoitaja. Mimi nilikua napendekeza isomeke, kwamba 'kupendekeza hatua zitakazo unganisha sekta ya utalii na sekta nyenginezo za kiuchumi'.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa katika mchango wangu ni kifungu cha 23 cha mswada. Kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti, katika kijifungu cha (b) kinasema, tunafuta kijifungu cha 3 na badala yake kuweka kifuatacho, naomba

nikisome, ‘mtu yeyote anayefanya biashara ya utalii aliyeajiri mtu ambaye sio Mtanzania kutoa huduma iliyoelezwa chini ya kijifungu cha (1) cha kijifungu hiki, ni lazima apate ruhusa ya maandishi kutoka kwa waziri, baada ya kumthibitishia waziri kua hakuna mtu wa ndani wa kujaza nafasi hiyo’. Kamati ilifanya marekebisho kwa kubadilisha badala ya waziri imependekeza iwe kamisheni.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kufanya marekebisho kwamba hili neno ‘Mtanzania’ liondoke hapo. Ajira Mhe. Mwenyekiti, ni haki ya Wazanzibari ndani ya Zanzibar. Kwa hivyo, tuseme wazi, ‘mtu yeyote anayefanya biashara ya utalii aliyeajiri mtu ambaye sio Mzanzibari, kutoa huduma iliyoelezwa chini ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, ni lazima apate ruhusa ya maandishi kutoka kwa kamisheni baada ya kuithibitishia kamisheni, kua hakuna mtu wa ndani wa kujaza nafasi hiyo’

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu katiba yetu kifungu cha 21(3) kinazungumzia katika haki za binadamu kwa Zanzibar ni pamoja na haki ya kufanya kazi. Sasa kama tumeweka haki ya kufanyakazi kwa Mzanzibari, lakini halafu huku kwenye fursa tuwe na fursa kwa watu wengine. Mimi nadhani hii imeshapitwa na wakati. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba mimi napendekeza hii iondoke ili kuwalindia Wazanzibari ajira zao na vile vile Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono mapendekezo ya kamati kwamba kile kifungu cha kufuta neno ‘*bar’* au nyumba ya kuuzia ulevi katika kifungu cha 25(b). Nakubaliana na kamati kwamba tulibakishe neno ‘*bar*’ kwamba iwemo katika maeneo ambayo kamisheni ina uwezo wa kuyafunga ikiwa itaridhika kwamba amekiuka taratibu.

Baada ya kuyasema hayo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunivumilia. Najua umenivumilika kwa sababu ulikua ukiamini kua nilikua nautendea haki mswada. Niseme kua nauunga mkono mswada baada ya marekebisho ambayo nimeyatoa ikiwa yatazingatiwa. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuchangia mswada wa marekebisho ya sheria ya utalii. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwa kutuletea marekebisho haya ya mswada ya sheria ya utalii.

Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri katika hali hii ya kutuletea mswada huu, mimi nasema hapa ni mahala pake kabisa. Wazanzibari waliowengi wanatuangalia na hii ndio nusra ya marekebisho haya katika mambo ya utalii. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hakuna hata mmoja aliyekua haupendi utalii, kwa sababu unatupatia kipato, lakini tuzungumze tu ni utalii wa aina gani tunaoutaka Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, tunaukaribisha utalii lakini tuelewe kua ni utalii wa aina gani tunaoutaka Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja kwenye mswada wenyewe. Katika kifungu hiki cha 23(b) (1), kuna kamati za utalii na wilaya zinatekeleza majukumu. Kifungu cha 23(a) kinasema kuendeleza dhana ya utalii kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, kuendeleza dhana ya utalii kwa wote ni kwamba wote tuliokua katika sehemu hizo tuupe nguvu utalii, ni sawa tutafanya hivyo. Lakini ni utalii wa namna gani. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa imekithiri kabisa, mimi naamini kwamba watalii huko nchini kwao wanavaa vizuri, tena wanavaa suti za kupendeza kabisa, lakini wanapoingia hapa basi wanatutukanisha Wazanzibari ambao sio silka na utamaduni wetu Wazanzibar.

Wazanzibari ni watu wenye kuheshimika, ni watu wastaarabu na ni watu wenye kujali utamaduni wao. Lakini hao watalii wanapofika hapa wanasababisha kuiga silka na utamaduni uliokua sio wetu. Mtu mwenye kuiga akifuzu basi atamshinda yule mwalimu wake aliyemuigiza. Kwa hivyo, Wazanzibari tumefuzu kuiga mila ambazo sio zetu na sasa hivi tunatembea uchi bila ya kua na ukomo, tutafika hatua Mwenyezi Mungu atunusuru na kufika tukaletewa sunami, kwa hali hii tunayokwenda, Mwenyezi Mungu atunusuru tusifike huko.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu za msingi, katika sehemu tunazotembelea tunaona hakuna hata mmoja. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu hili pamoja na wewe mwenyewe unaona hiyo hali. Wakati tunatembea tunawaona watalii wanatembea kila sehemu mjini na mashamba. Hiyo haitoshi, hapa katiba ya Zanzibar inampa fursa na haki Mzanzibari ya kufanya shughuli zake kama Mzanzibari, lakini katika haya mambo ya utalii basi wageni ndio wanaofaidika zaidi kuliko Wazanzibari wenyewe. Jambo hili sio zuri na wala hatuwatendei haki Wazanzibari.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kazungumza sasa hivi kwamba mpaka leo kule Marumbi na Chwaka kuna matatizo na Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa umeletwa angalau ugomvi ule usijitokeze tena, lakini umejitokeza. Hii ni kwa sababu ya kunyimwa haki Wazanzibari. Tumeukaribisha utalii, lakini Mzanzibari anakosa ile fursa ya kufanya shughuli zake, hasa wavuvi wamekosa fursa bahari yote inaweza kutoa hifadhi na Mzanzibari akakosa hapa pa kupita, iko siku tutakosa hata kupita hizi meli zetu ikawa hakuna hifadhi, meli haziruhusiwi kupita kwa tunavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, kama wenzetu wa Kenya wanapata watalii kushinda sisi. Lakini kule kuna maeneo yametengwa ya watalii na kuna maeneo ya wananchi kufanya shughuli zao. watu wanatumia boti kila siku kwa kuwapeleka watalii kwenda kuangalia sehemu zao za utalii. Lakini sisi maeneo yote tumesema kwamba ni maeneo ya hifadhi. Je, kama yote tukifanya ni maeneo ya hifadhi tutapita wapi Wazanzibari. Ni kweli hifadhi ni nzuri, lakini yatengwe maeneo na maeneo mengine inabidi yabakie kwa ajili ya Wazanzibari wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia katika kifungu hiki cha 23(1) kinasema, kulinda usalama na amani kwa wageni na jamii katika maeneo ya utalii. Ni sawa tulinde, lakini hao wanaoongoza watalii wanawaelekeza vizuri, wanawaelekeza katika sehemu hatarishi ambazo mtalii akipita anaweza akakwama. Mhe. Mwenyekiti, unamkuta mtalii saa 4:00 za usiku yuko sehemu za Jang'ombe, je huyo ana usalama. Ni lazima tuzingatie hilo, kuwaelekeza sehemu na kuwapa vipeperushi, ni namna gani ya utalii tunaoutaka. Wale wanataka kuelekezwa tu. Mhe. Mwenyekiti, tumezungumza hapa kwamba watalii kule kwao wanavaa vizuri, isipokua wakifika katika sehemu za bahari kule ndiko sehemu zao wanazoweza kufanya mambo yao ya utalii, lakini sisi hapa kwetu tunakwenda tu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho kijifungu kidogo cha (e) kulinda, kuendeleza na kukuza utamaduni wa kiasili ya Zanzibar kama ni sehemu ya bidhaa ya utalii. Ni sawa, lakini tunalindaje, tutalinda sehemu hiyo kwa kuleta vivutio ambavyo vinawavutia watalii, lakini sisi tukiangalia tumeacha silka na utamaduni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie hawa watalii wanafuata taratibu za utalii, sehemu za bahari, fukwe na pia wanakuja katika mji. Sasa wakati wanapokuja katika mji, yaani sehemu ya Darajani ni kubwa kwa watalii na wasiokua watalii wanatembea.

Lakini Wallahi kuna Mkahawa unaoitwa *Marikiti Cafe*, basi watalii wameshawahi kutengewa sehemu nyengine kwa ajili ya kupata chakula, hawa watalii tulionao kutokana na harufu mbaya ya jaa liliopo pale Darajani mkabala ya marikiti. Kwa kweli jaa lile linanuka harufu mbaya sana, sijui kwa sababu ya kucheleweshe kuondoa zile taka au vipi, sasa utawaita watalii namna gani.

Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti wanatuambia waliokwenda China wanatuambia karatasi huioni pale chini, lakini ukizunguka mji mzima wa Zanzibar umeoza kabisa hatuleti usafi, je hicho kitakua ni kivutio. Mhe. Mwenyeiti, lazima tuweke mazingira mazuri ya mji wetu, kwani tukiweka mazingira mazuri ya mji wetu itakua ni vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala ya utamaduni, basi utamaduni wetu uwe wa Wazanzibari. Kwa mfano, mavazi Wazanzibari tunavaa vipi, kwa kweli mavazi yetu Wazanzibari tunayovaa hivi sasa tunaelekea kubaya sana na namuomba Mwenyezi Mungu aturushe tunakoelekea na turudi kwenye utamaduni wetu wa mavazi.

Tukiangalia enzi za wazee wetu walikotoka. Kwa mfano, mwaname alikua anapiga kanzu yake nzuri, koti, kofia pamoja na bakora yake na huyu ni mwanamme halisi anatembea vizuri na akinamama pia nao wanavaa vizuri, yaani wanavaa mabaibui ambayo yenye stara, lakini hivi sasa hayo mabaibui yenyewe ni mipacho mitupu, hivi tunaelekea wapi?

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ukiona baibui limetoka kutengenezwa basi ni hatari, kwa sababu mtu atavaa baibui kwa ajili ya kujistiri, lakini baibui limepasuliwa mbele na kote kukowazi, hivi ni utamaduni gani wa Wazanzibari? Kwa kweli ni jambo la kusikitisha katika masuala ya Wazanzibari tunaelekea kubaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, mtu yeyote anayekwenda nchi ya watu, basi lazima afuate sheria za nchi anayokwenda. Kwa mfano, mimi sitokwenda Kenya au nchi nyengine na kutunga sheria zangu, isipokua nitafuata sheria za nchi ninayokwenda. Kwa hivyo, na sisi kama tutakaa vizuri na kutunga sheria zetu hizi basi wageni wote watafuata utaratibu wa sheria zetu tulizozitunga. Kwa mfano, tukiangalia nyumba za starehe hizi ni ufuska mtupu unaofanywa.

Sasa mtoto wa Kizanzibari atajifundisha nini. Kutokana na hali hiyo, naomba tutoke huko na tuelekee kwenye maadili yetu tuliyotoka pamoja na utamaduni wetu tena, ambao ni mzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika fursa hizi ndio maana hata Wazanzibari wenyewe wanakua hawapati hadhi zao za kazi. Kwa mfano, hapa mtu ananyimwa Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi na sheria inasema mtu yeyote aliyetimia umri wa miaka 18 anayo haki ya kupata kitambulisho hicho, lakini ukiangalia wageni wanapata vitambulisho na Mzanzibari hapati. Kwa kweli hivi sasa wapo Wamasai Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi wanavyo, lakini Mzanzibari halisi hapati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, masikini wa Mungu kule Kojani kisiwani ndani ya Jimbo langu kuna wazee hawajatoka hata siku moja, yaani hawapajui hata pale Wete sasa huyo utamwambia kwamba si mkaazi, tokea azaliwe na wazee wake yupo pale. Lakini mwanawe ananyimwa haki kwa sababu hana cheti cha kuzaliwa, je ni wangapi wenye vyeti vya kuzaliwa? Kwa hivyo, nadhani kama kuna mabadiliko ya sheria, basi sheria hii iletwe mara moja kwa ajili ya kurekebishwa. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu, tukiangalia kwenye masuala ya utamaduni ni mambo yaliyotuletea sifa kubwa Zanzibar, yaani yametuletea sifa kwa utamaduni tulionao. Lakini hivi sasa utamaduni tulionao ni utamaduni wa kuiba, ambao ni mbaya. Kwa nini niseme hivyo. Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo, kwa sababu hapa tulikua na ngoma zetu za asili.

Kwa mfano, Ngoma ya Msewe popote ilipokua ikipigwa, basi ilikua ikifurahisha, tena yenye hadhi, lakini hivi sasa ngoma zile zote zimepotea na wala hazitambuliki. Vile vile tulikua na ngoma ya beni, yaani ni ngoma za kivutiio katika nchi yetu, lakini hivi sasa hazitambuliki na siku hadi siku zinaendelea kufa. Mhe. Mwenyekiti, mambo haya ndio kivutio cha mji wetu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Ngoma ya Kibati pia nayo ilileta heshima kubwa sana. Kwa mfano, kule Mkoani Mzee Jumbe alikua akiimba kibati na kila mtu alikua akifurahi. Lakini mambo hayo yote tumeyaacha na tunaelekea katika mambo ambayo hayatuhusu. *(Makofi)*

Katika mambo ya michezo, hata mchezo wa Ng'ombe ulituletea sifa sana. Mhe. Mwenyekiti, katika mambo haya ya utalii ni juzi tu na wala sikumbuki ile tarehe wazungu wapatao 90 walifika ndani ya Jimbo langu sehemu ya Chwale na kwenda kuangalia Mchezo wa Ng'ombe na hiki ni kivutio tena haya ndio mambo yanayotakiwa. Sasa wakipata habari kama hizi, basi watalii wanapata moyo wa kuja kuangalia Wazanzibari wanafanya nini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala haya ya michezo pia ni utamaduni wetu Ngoma ya Msondo ilikuwepo. Lakini hivi sasa kuna mipasho, yaani ni kuvaa mavazi ya uchi kwenda mbele tu. Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache naunga mkono pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kojani kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii leo kwa ajili ya kuweza kutoa mchango wangu katika mswada huu muhimu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kwa kusema kwamba kwa kweli mswada huu ni muhimu sana kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala zima la utalii kwa Zanzibar ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu. Sasa nadhani Mhe. Mwenyekiti, utuvumilie kidogo, ili tuweze kuishauri vizuri serikali katika suala zima la kuhakikisha kwamba tunausimamia utalii, lakini na faida inayopatikana na utalii wenyewe.

Nianze na kusema kwamba kwanza tulikosea, yaani nakusudia kusema kua tunafunga banda wakati farasi ameshatoka. Kwa nini nikasema hivi, Mhe. Mwenyekiti, tulipoanzisha utalii Zanzibar viongozi wetu wakuu wa nchi walielezea kua tunaleta utalii, ili kuweza kutoa ajira kwa vijana wetu wa Kizanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka kipindi hicho kabla ya hoteli nyingi za kitalii hazijaanza Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar wa awamu ya tano Dkt. Salmin Amour Juma aliwahi kuzungumza maneno haya katika Kijiji cha Marumbi. Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu. "Tunataka kuwafanya vijana badala ya kuondoka vijijini na kuhamia mijini, tunataka sasa vijana tuwahamishe mjini na kuwapeleka vijijini".

Kwa kweli nilikua nikijiuliza maswali mengi sana, kwa sababu leo kila mtu au sisi sote tunatoka makwetu shamba waliokua hawatoki shamba kwa hapa mjini, basi ni wageni. Lakini hapa mjini wengi wetu tunatoka mashamba au kwa lugha ya wenzetu vijijini.

Sasa mimi nilikua nikijiuliza kwa nini vijana walitoka mashamba, yaani wazee wetu mpaka wakatuzaa sisi, inamaana kulikua na vitu ambavyo viliwavutia ni kufuata ajira kwa ajili ya kuweza kupata maslahi. Kwa hivyo, leo viongozi wetu watafanya miujiza gani kuwahamisha watoto tunaowazaa sisi ambao watakua ni vijana kuwarudisha vijijini, basi alisema tunataka kuanzisha utalii.

Mhe. Mwenyekiti, pale mwanzo tulikua tunahisi kama ndoto, lakini baadaye tuliona kweli vijana wengi inapofika kuanzia mwezi wa Juni, basi wengi hawakai vijiweni wanakwenda vijijini kwenye maeneo ya hoteli.

Lakini hatukujipanga vizuri wakati tulipoanzisha biashara hii. Mhe. Mwenyekiti, nchi za wenzetu nadhani ilikua kabla ya mswada huu kuja, basi hii Kamati ya Baraza la Wawakilishi ambayo inayoshughulikia masuala ya utalii, ni vyema ungeipa nafasi ya kutembelea katika nchi hizi za visiwa vinavyolingana na mazingira kama haya ya kwetu kama vile Seychelles na Mauritius. Kwa hivyo, kule wangelikwenda kujifunza wenzetu ni namna gani wanavyoutumia utalii na unawafaidisha vipi wananchi wao. *(Makofi)*

Lakini tatizo lako Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wako wa baraza la Wawakilishi huwapi nafasi za kwenda kujifunza. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nadhani tubadilike na uwape nafasi. *(Makofi)*

Kwa mfano, hii Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ungeliwapa nafasi wakenda Seychelles na Mauritius, basi mswada huu Mhe. Mwenyekiti usingekuja hivi, isipokua ungekuja na marekebisho mazuri ambayo yangeweza kutufanya tukauchangia vizuri mswada na ukaleta manufaa kwa Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa nini nikasema hivyo, Mhe. Mwenyekiti wenzetu Mauritius wakati wa Mhe. Rais wa Zanzibar wa Awamu ya Kwanza Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, waliwahi kuja kutuomba na tuliwasaidia. Mhe. Mwenyekiti, Kiongozi wetu muasisi alikua ni mtu mwenye imani sana, yaani tuliwasaidia wenzetu, lakini baadaye wakaona kwa nini tupite kuomba omba, basi walijipanga na kuangalia nchi yao na kuamua kuanzisha biashara hii ya utalii. Kwa kweli wenzetu tukiangalia uchumi wao nadhani hawana mafuta, isipokua ni vitu viwili tu ndio *priority* kwao wao, kuna masuala ya utalii pamoja na biashara yao ya miwa ambayo ni moja ya vianzio vyao vya uchumi na inawaendesha vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu ile nchi yao ya visiwa kwa hiyo kitu kimoja walichoweza kui-*control* nchi yao, ni uingiaji wa watu holela katika nchi yao. Mhe. Mwenyekiti, nchi yoyote ya visiwa huwezi kuachia watu kuingia kama wanaingia chooni. Kwa kweli leo Zanzibar tutaanzisha uwekezaji wa kila aina, bado vijana wetu wataendelea kulalamika kwa kukosa ajili, kwa sababu hatuna udhibiti wa ku-*control* kwanza uingiaji wa watu, lakini kudhibiti hata zile ajira tunazozikaribisha katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa mfano mmoja ambao ni hai. Mhe. Mbunge wa Jimbo la Kiembe Samaki, ambaye huko nyuma alikua Mkurugenzi katika Idara ya Maafa, huyo alisoma Mauritius.

Sasa wakati alipokua akisoma kama tunavyojua vijana wanapopata muda wa likizo hua mtu anaomba kufanya kazi japo ya *part time*, kwa ajili ya kupata riziki kidogo. Mhe. Mwenyekiti alihangaika mwisho aligonga ukuta, yaani mpaka ile kazi ya kulea watoto nyumbani hupati kama mgeni na hivyo ndivyo nchi zinavyokwenda. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, sisi Marais wetu wakati wanapokwenda kwenye kampeni wanawaahidi vijana kwamba tutakupatieni ajira, maisha mazuri. Kwa kweli baada ya kupata serikali kama hukuweza kudhibiti zile ajira wakapata wananchi wako, basi wananchi wako kila siku wataendelea kukulaumu, kwa sababu uwekezaji Zanzibar upo lakini hauna udhibiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hili suala la utalii na ndio maana nilisema tunafunga banda farasi ameshatoka. Kwa kweli kwanza ilikua ule uwekezaji, yaani Mwekezaji yeyote anayekuja katika nchi yetu sheria hii ndio inayompa muongozo, kwamba ajira yako watu wowote utakaowajiri basi lazima wawe Wazanzibari, isipokua kwa zile nafasi ambazo Wazanzibari watakua hawana sifa.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo sisi Zanzibar hatukijui hasa tunachokitaka, mimi nataka niseme hivyo. Kwa mfano, leo tukiangalia uchumi wetu mkubwa ni utalii, hebu tukiangalie Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar, hivi kweli kinalingana kwamba utalii ndio nguzo kuu ya uchumi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka kutoa mfano mmoja, serikali sio kama haina fedha, lakini hatuna mipango mizuri ya kuweza kusema kwamba hii ndio Mipango Mikakati ya Kitaifa. Mhe. Mwenyekiti, tumeweza kutenga fedha shilingi bilioni moja na nusu kwa ajili ya kujenga jengo la Wizara ya Fedha Pemba leo nyumba inaning'inia. *(Makofi)*

Lakini je, bilioni moja na nusu zile tungezipeleka na kukijenga Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar, ili hawa vijana wetu tuweze kuwaandaa kwa ajili ya kuingia katika soko la utalii, hivi leo tungekua wapi? Ndipo pale nilisema kwamba hatukijui tunachokitaka, yaani ule uti wa mgongo wa uchumi sisi wenyewe ndio tunaoudharau. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie hali ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar akesha kutoka pale mtu anakwenda kufanyakazi Hoteli ya Lagema au Kempinski akifika kule ile wiki ya mwanzo kazi hawezi kufanya, yaani yale mazingira ya alikosoma na kule anakokwenda kufanya kazi hayalingani hata kidogo. *(Makofi)*

Nadhani wakati umefika serikali itafute fedha na ijenge Chuo cha Maendeleoo ya Utalii Zanzibar tena kiwe na *facilities* zote tena za kutosha, ili hata wale wawekezaji wanaokuja wasema ah! Hawa kweli wanataka kuimarisha utalii wao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, natoa angalizo Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Sita Dkt. Amani Abeid Karume, walikuja Wairain na katika mambo aliyozungumza nao aliwambia ah! Tunahitaji mambo mengi kwa ajili ya kusaidiwa, basi Iran walisema jiandaeni tafuteni kitu chochote, walisema sisi tutaleta dola milioni moja mtaangalia nini cha kufanya. Mhe. Mwenyekiti, Dkt. Karume aliagiza dola milioni moja zilizotoka katika Serikali ya Iran zipelekwe kwa ajili ya kuimarisha Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze kwamba hili analijua na kama halijui, basi alifuatilie na nadhani akilifuatilia vizuri atakuta, ili kuweza kufuatilia fedha hizo zilipo kwa ajili ya kuimarisha Chuo chetu cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar. Kwa kweli hatuwezi kuendelea kuzungumza kwamba uti wa mgongo wa nchi yetu ni utalii, lakini bado sisi wenyewe hatujajiandaa katika kuupokea huu utalii wenyewe.

Nikiendelea na mchango na ndipo pale niliposema kwamba tunafunga banda, lakini farasi ameshatoka. Hivi sasa ajira ya utalii na yale malengo ya viongozi wetu kuanzisha utalii Zanzibar yamepotea, takribani asilimia karibu 70 ya ajira ya soko la utalii wapo wageni kuanzia *managers* mpaka wale wafyagiaji.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili lazima tuliwekee mikakati, yaani lazima tuwe na muda maalum. Kwanza tuhakikishe kwamba tujue hoteli zako ngapi pamoja na wafanyakazi wangapi.

Mhe. Mwenyekiti, siridhiki kwamba Kamisheni ya Kazi wao ndio wawe wanaoshughulikia masuala ya kazi zote katika *Private Sector* pamoja na Sekta ya hoteli.

Kwa hivyo, nadhani wizara yenyewe inayoshughulikia masuala ya utalii kungekua na kitengo maalum ambacho kinashughulikia kujua wawekezaji wanaokuja katika *Sector* ya Utalii pamoja na ajira kwa wale watu watakaowaajiri. Kutokana na hali hiyo, hivi sasa lazima tuwe na *percentage*, haiwezekani tukaachia watu kuajiri watu wakaajiriwa tu kiholela.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti hata mikataba, kwa kweli hoteli nyingi hivi sasa zimeajiri vijana hawana hata mikataba ya kazi, yaani watu wanafukuzwa kama kuku. Kwa mfano, leo wafanyakazi baada ya miezi sita anafukuzwa na anapofukuzwa hakuna hata ule utatu, kwa sababu kuna Kikao kinachoitwa Tripolarity. Mhe. Mwenyekiti, kikao hicho kinamhusisha yule mwekezaji, Chama cha Wafanyakazi pamoja na yule mwenyewe kwa ajili ya kujitetea. Lakini leo Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi katika hoteli wanafukuzwa kama kuku hawana mikataba na wala hawakijui wanachokifanya**.**

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, wanaajiriwa wageni katika hoteli kama *expertise*, lakini unapokwenda na kuzungumza na vijana wetu hasa katika maeneo ya upishi pamoja na maeneo mengine.

Kwa kweli utakuta yule mgeni taaluma yake inakua ndogo kuliko huyu kijana wetu, lakini yule mgeni analipwa kama ni *expert*, yaani analipwa mshahara wa *expert*, wakati yule kijana wetu wa hapa ambaye amesoma vizuri pamoja na *CV* nzuri pengine katika mambo ya upishi, unamkuta yeye analipwa kiwango kidogo na yule mgeni analipwa kwa fedha za kigeni na kiwango kikubwa.

Hali hii inatokana na nini? Mhe. Mwenyekiti, hatuna udhibiti mpaka kwenye ajira za utalii, ndio maana ninaposema kwamba tumefunga banda farasi ameshatoka, kwa sababu haya yanafanyika kwenye hoteli, lakini pamoja na kwamba farasi ameshatoka, bado tunaweza kumpiga shemere farasi na kumrudisha bandani.

Kwa hivyo, lazima zifuatiliwe tena ajira zote katika mahoteli yetu na tuangalie kwenye maeneo ambayo vijana wetu wao wenye ujuzi pamoja na taaluma, basi nafasi zile wachukue wao na wale wageni watusamehe, kwa sababu zipo nchi nyengine wanaweza kwenda kufanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe msemo wa Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Siku moja aliulizwa katika masuala ya ardhi, kwa nini watu wa Tanganyika au Tanzania Bara wao hawaruhusiwi kumiliki ardhi Zanzibar, kwa sababu kwa mujibu wa Sheria ya Zanzibar, maana aliambiwa mbona Sheria ya Zanzibar inakua kama ya ubaguzi.

Sasa mwenyewe Mwalimu Nyerere na sio kama alikua ni Mzanzibari, kwa sababu Mwalimu Nyerere alikua ni Mtanzania *pure*, ambaye ni *original* kutoka Tanzania Bara na wala hajahusu Zanzibar hata mjukuu, alizungumza vipi?

Kwa hivyo, alisema Zanzibar kuunda ile Sheria ya Ardhi inayowa-*protect* Wazanzibari kwamba wao ndio waweze kumiliki ardhi hii ndio hali halisi ya nchi za visiwa. Kwa mfano, alisema kama tutawaruhusu watu wa Bara watoke huku na kila mmoja aende akanunue ardhi Zanzibar, basi watu wa Wilaya ya Kinondoni tu wote wakihamia Zanzibar, Wazanzibari wenyewe watakua hawana pa kukaa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, maneno hayo si ya Mzanzibari, isipokua ni ya Mwalimu Nyerere na alizungumza vile kutokana na *geography* ya visiwa kwamba havipanuki, isipokua watu wanaongezeka.

Kwa maana hiyo, tunaposema suala la udhibiti wa uingiaji wa watu Zanzibar. Kwa kweli hili sio suala la ubaguzi, kwa sababu watu wengine wanaweza kusema kwamba wanataka kuwabagua watu wa Bara, hakuna kuwabagua watu wa Bara.

Kwa mfano, wenzetu katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki Mhe. Mwenyekiti sura zetu zinafanana, labda mimi leo nikiingia Uganda, basi huwezi kusema kama huyu ni Mzanzibari, kwanza tukiangalia sura yangu nyeusi, bara, nadhani mimi ukinikuta Uganda huwezi kunibagua. Kwa hiyo, utakuta na wale wakija wanaingia kama vile Hamza anaingia Zanzibar hakuna hata kizuizi, ndipo pale tuliposema kwamba mtu anaingia kwenye kucheza *pool*. Kutokana na hali hii, ni lazima nchi yetu tuweze kuilinda.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Ulaya wanao Muungano wao wa *European Union*, kwa mfano ukitaka kwenda Italy, Germany, France au sehemu nyengine, sasa ukienda Ubalozini kwao basi unapata *Visa* moja tu unagongewa *Visa* ya Ulaya na unatembea nchi zote na ukienda kwenye ile mipaka wameondoa zile *block* na unapita kwa miguu na kurudi.

Lakini Uingereza hata kama unayo Visa ya Ulaya huwezi kuingia Uingereza, kwa sababu gani? *Geography* yao ni visiwa tofauti na zile nchi nyengine za Ulaya na yale ni mabara, nchi za visiwa lazima zilindwe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ndipo pale nilipokwambia kwamba hii Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari hebu ipeleke Mauritius pamoja na Seychelles kwa ajili ya kwenda kujifunza ni namna gani wenzetu wanavyoendesha utalii wao na unawafaidisha wao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tulivyokua tumeshindwa ku-*control* masuala ya uingiaji nchini pamoja na kuweka taratibu nzuri za ajira Zanzibar. Kwa mfano, leo Mhe. Mwenyekiti mpaka Kampuni za Ulinzi nyengine si za Zanzibar, hivi tunakwenda wapi. Kwa kweli tumekua kama tunatawaliwa, yaani tunalindwa na kampuni za nje, hivi tutegemee kweli kutakua na ulinzi na usalama katika hoteli zetu.

Nadhani lazima tubadilike, ndio maana niliposema kwamba huyu farasi tunaweza kumpiga shemere akarudi tena bandani, yaani ajira zirudi kwetu kwa Wazanzibari, ili vijana wetu Wakizanzibari waweze kupata ajira.

Nikiendelea sasa naomba nitoe mfano wa bidhaa. Mhe. Mwenyekiti, ilipokaribishwa biashara ya uwekezaji wa utalii imekusudia kutoa ajira na kuinua uchumi kwa wananchi. Kwa kweli hawa wawekezaji, yaani wenye hoteli wanaagiza bidhaa moja kwa moja kutoka nje ya nchi, wakati bidhaa zile walikua wafanyabiashara wa Zanzibar wao ndio waagize bidhaa zile na wenye hoteli wanunue. Lakini leo mwenye hoteli anaagizia nyama, maziwa ya makopo, yaani mpaka dawa za kusafishia wanaagiza kutoka nje na sisi wenyewe tupo wapi? Hivi ni ajira gani watakayopata Wazanzibari? Kwa hivyo, nafikiri haya mambo ndio maana mwekezaji anaambiwa wewe ekeza kwenye hoteli, lakini bidhaa zote katika hoteli yako ununue, sasa kama zile bidhaa atanunua, basi atanunua kutoka kwenye kampuni au wafanyabiashara wa Kizanzibari.

Kwa maana hiyo, wafanyabiashara wa Kizanzibari wakiweza kufanya biashara nyingi, yaani wakiwauzia wenye hoteli ya kitalii, basi na wao wataweza kutanua biashara zao na kutoa ajira kwa vijana wetu na kuondoka vijiweni na kwenda kuajiriwa kwa wafanyabiashara. Mhe. Mwenyekiti, matokeo yake leo kila kitu tumewaachia huru na kila mtu anafanya anavyotaka utafikiri hii nchi yetu tumehama haina wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala ambalo limejitokeza hivi karibuni, baada ya serikali kutangaza mishahara mipya. Kwa kweli kuna unyanyasaji mkubwa unaofanywa kwenye hoteli baada ya kutangazwa kwa mishahara mipya. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, alitoa Tamko kwa Wawekezaji wote katika *Sector* ya Utalii kwamba hivi sasa kiwango cha chini cha mshahara kama walikua wakilipwa shilingi 80,000/= basi hivi sasa walipe kama inavyolipa serikali kuanzia 150,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, wawekezaji hao wamechukua fursa hii kwa kuwanyanyasa wafanyakazi, yaani wanawapunguza wafanyakazi na hili ni kosa na wala serikali haiwezi kukaa kimya na huu ndio udhalilishaji. Kwa kweli hawa waliotupigia kura hivi sasa wamo mitaani hawana kazi.

Kwa mfano, mtu ameoa kwa sababu anafanyakazi kwenye hoteli, sasa leo amefukuzwa kinyume na utaratibu, basi vijana wale wataendelea kutupiga virungu na watatumaliza. Mhe. Mwenyekiti, watatumaliza lakini wenzetu wanaendelea kutengeneza faida na suala hili haliwezekani.

Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Waziri mwenye kushughulikia masuala ya utalii kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba awaite wawekezaji wote akae nao upya na hili suala la kufukuzwa wafanyakazi kiholela sisi hatulitaki na kama uwekezaji tumuuita sisi, sasa kwa nini uwekezaji, maana yake baada ya uwekezaji unatukalia juu na wala hatuna pumzi kama vijana hawana, hivi sisi pumzi tutaipata wapi? Mhe. Mwenyekiti, tunaiomba serikali suala hili ilishughulikie tena kwa haraka sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niende moja kwa moja kuuchangia huu mswada na hii yote ilikua ni dibaji tu.

Nianze moja kwa moja kwenye kifungu cha 5 cha mswada Mhe. Mwenyekiti, lakini kabla ya kifungu cha 5 nakuja kwenye kifungu cha tatu. Kifungu cha tatu kinarekebisha kifungu cha pili kuna maneno haya ambayo yamefanyiwa marekebisho ikiwemo tafsiri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe una dakika tano za ziada.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hii, kifungu hichi kina tafsiri ya mtalii sasa hii tafsiri ya mtalii nilikuwa naomba Mhe. Waziri aje anisaidia zaidi hii tafsiri kakusudia nini, inasema mtalii maana yake ni mtu ambae yupo katika sehemu ambayo sio makazi yake lakini yupo kwa ajili ya kazi, mapumziko au starehe. Sasa Mheshimiwa kuna wafanyakazi wengi humu wengine wanafanya kazi majumbani, wengine wanafanya kazi sehemu nyengine nyengine ambazo sio za utalii sasa je na hawa ni watalii, hii tafsiri kidogo naona haijakaa vizuri nilikuwa naomba ije kuwekwa sawa. Kwa sababu ukisema kwamba maana yake ni mtu ambae yuko katika sehemu ambayo sio makaazi yake unaposema sio

makaazi yake ina maana ni mgeni hapa Zanzibar, lakini yupo kwa ajili ya kazi au mapumziko au starehe sasa hili kidogo tutahitaji ufafanuzi kwa sababu wamo wengine wanafanya kazi nyengine ambazo sio za utalii lakini hapa sio kwao.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kifungu cha tano kinasema muundo wa kamisheni, kwanza inasema kamisheni itakuwa na mwenyekiti atakayekuwa mkuu wa kamisheni kwa muda wote na ambae atateuliwa na rais, nikija hiki kifungu cha tano lakini vilevile nimejaribu kuangalia katika madhumuni ya mswada, katika madhumuni ya mswada hii tafsiri kidogo imenichanganya ndio maana nikasema nije kupata na ufafanuzi. Katika madhumuni ya mswada ina sababu ya mswada lakini haya maelezo yana *refer* kile kifungu cha tano.

Kinasema: "marekebisho yanayopendekeza kuwepo kwa mwenyekiti wa kamisheni ambae atakuwa anafanya kazi kwa muda wote na kufutwa kwa bodi ya wakurugenzi na kueleza uteuzi wa makamishna, wakamisheni vile vile marekebisho haya yanapendekeza kufutwa kwa nafasi ya Mkurugenzi Mkuu bdala yake kuwekwa katibu Mtendaji wa Kamisheni ambae atakuwa msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku za kamisheni".

Sasa huyu Katibu Mtendaji wa Kamisheni yeye atakuwa ndio miongoni mwa hao wajumbe wa Kamisheni, sasa huku kwa kuwa kuna Mwenyekiti sasa huyu Katibu Mtendaji anaambiwa yeye ndio atakuwa msimamizi mkuu, wakati Mkurugenzi Mtendaji yeye ndio anakuwa mtendaji mkuu sio msimamizi mkuu, msimamizi mkuu hapa atakuwa huyu Mwenyekiti. Sasa hii naona kama itakuwa *vise vaser* au labda Mhe. Waziri aje anitolee ufafanuzi uliokuwa mzuri.
Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki hiki cha 5(3) kinasema "Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti mpaka awe na utaalam wa kipekee katika fani inayofanana na utalii, uongozi wa wadau wa utalii au uhusiano wa kimataifa".

Mhe. Mwenyekiti hapa hatujataja sifa hii ndio sekta kiongozi huwezi ukatamka mtu awe na uzoefu awe na nini bila ya kutaja kiwango chake cha elimu, sasa hivi kwa karne tunayokwenda wajomba tuwasamehe tutafute watu wenye taaluma ambao wana sifa za kuweza kushika nafasi na kuweza kusaidia utalii kuondoka hapa tulipo kwenda kule ambako tunakutaka, sasa huku lakini katika uteuzi wa Mkurugenzi huku alitakiwa kwamba awe na stashahada ya kwanza, sasa leo utakapomuweka Katibu Mtendaji kama huku atakuwa na stashahada ya kwanza ambapo mwenyekiti anatakiwa mtu mwenye uzoefu tu. Kwa maana hiyo bosi atakuwa taaluma yake ndogo lakini yule ambae anamtwika majukumu ya kuweza kutekeleza anakuwa taaluma yake kubwa, hii kidogo naona itakuwa haifanani fanani.

Sasa mimi napendekeza kwamba basi ile sifa ambayo alitakiwa awe nayo yule Mkurugenzi au Katibu Mtendaji wa kamisheni basi ni vizuri na huku ile sifa, basi huku angalau angeambiwa akawa na shahada ya kwanza katika masuala ya utalii au uchumi au japo masuala ya uhusiano wa kimataifa. Kwa sababu ni mambo ambayo yanalingana lingana na mambo mengine ya uzoefu yatafuata baadae, lakini suala la shahada hapa Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri akija ajaribu kututolea ufafanuzi wa kutosha.

Halafu vile vile (2) kinasema ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo, sasa kupigania mambo gani hayo mambo yapo mengi, sasa asiwe ana ujuzi wa kupigania mambo mengine akaja kuwekwa kwamba ana sifa ya huyu mtu ambae ndio atakuwa mwenyekiti.

Halafu mahusiano mazuri na watu vipi hapa tunazungumzia suala la uchumi huu utalii, kuna watu wana mahusiano mazuri na watu lakini hamna kitu sasa mimi nadhani hizi sifa hizi kwanza tuangalie katika zile shahada kwanza halafu haya mambo mengine yatafuata baadae, hizi ziwe kama ni sifa za ziada lakini ile taaluma iwe ndio kitu cha mwanzo ingawa kidogo nne inasaidia, na taaluma nyengine ambayo inaendana na hiyo ambayo ni muhimu katika sekta ya utalii Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika suala zima la muundo wa Kamisheni, hapa sheria inasema kwamba kamisheni itakuwa na makamishna wengine wasiozidi sita watakaoteuliwa na waziri, mimi nadhani kama kutakuwa hakuna *loop hole* ya kumpachika basi tupendekeze iwe saba tumemuacha mtu muhimu sana katika hii kamisheni. Mkurugenzi wa Mazingira kama nilivyosema jana uwekezaji wowote Zanzibar ujenzi wowote Zanzibar lazima kwanza ufuate utaratibu au masharti ya mazingira, sasa hivi hii sheria tunayoitunga au huu ujenzi wa mahoteli yetu ya kitalii takriban karibu yote yamekiuka uhifadhi wa mazingira. Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa naomba

Mkurugenzi wa Mazingira hapa huyu ndiye chumvi hapa katika eneo hili, kwa sababu chochote kinachotaka kufanyika yeye atakuwa anatoa ile taaluma na uzoefu wake katika masuala mazima ya uhifadhi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 6(4) naomba nikinukuu. "Mshahara na mafao Mwenyekiti wa Kamisheni baada ya kumaliza itakuwa kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma Nam. 2 ya mwaka 2011 kulingana na masharti ya uteuzi wake".

Mhe. Mwenyekiti, hii nafasi aliyopewa huyu hailingani na hii sheria ambayo tunayoisema mimi nadhani tuna bodi nyingi, kamisheni nyingi nadhani zina utaratibu wake kwa sababu hawa kwa kuwa zinakwenda kwa muda maalum hizi ni kazi za mkataba isipokuwa kwa wale watendaji wengine, labda kama huyu Katibu Mtendaji kwa sababu yule ni mtendaji wa kudumu huyu masharti yake yanaweza kufuata ile sheria ya utumishi wa umma. Lakini kwa huyu Mwenyekiti hapa mimi nafikiri sifa ya kulipwa stahili zake kama sheria ya utumishi wa umma itakuwa haistahiki, kwa sababu huyu kila anapomaliza muda analipwa mafao yake anapongezwa anapewa baskeli TV na vitu vyengine tena mambo mengine yatafuata baadae.

Mhe. Mwenyekiti, nakuona unaniwashia taa nimeshaona lakini naomba uniruhusu nimalize hivi vifungu kwa sababu nataka ufafanuzi baadae, katika kifungu cha 17(2) hichi kilikuwa naomba kukinukuu kidogo kinasema. "Kwa mujibu wa kijifungu cha pili cha kijifungu hichi mtu hatakiwi kuendesha au kufanya biashara ya kujitangaza kama anafanya biashara ya utalii mpaka awe na leseni ya biashara ya utalii iliyotolewa na Kamisheni".

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema hii sheria tunafunga banda wakati farasi ameshatoka, sasa hivi ukiangalia katika maeneo yetu ya uwekezaji watu wanajifanyia wanavyotaka utafikiri wenyewe hatupo, wenye mahoteli waliojenga katika miaka ya nyuma walifuata taratibu zote za mazingira. Lakini sasa hivi kwa kuwa wanatuona wenyewe tumelala na tunasinzia wanaharibu mazingira ndani ya mahoteli ambayo yamejengwa kisheria zaidi. Sasa mimi nadhani kwa hivi sasa hii sheria itakavyokuwa naamini kidogo ule ushauri utaweza kufuatwa, lakini naomba sana Mhe. Mwenyekiti sheria nyingi tunatunga nzuri hapa.

Katika nchi ambayo ina sheria nzuri ni nchi yetu ya Zanzibar lakini tatizo letu ni katika utekelezaji na usimamizi, tatizo letu tunaoneana muhali sana watu wameshavunja sheria mtu anajenga kinyume cha taratibu lakini baadae hatua za kisheria zinapotaka kuchukuliwa unaambiwa basi muachie kwa sababu Zanzibar hivi ndivyo tulivyo, sasa haya mambo hayawezi kutupeleka pahala.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile kwenye kipengele hichi ndio kimewekwa kwa ajili ya hii leseni inayotolewa sasa basi ndio hasa inayotakiwa kwamba hii biashara wanatakiwa wafanye Wazanzibari wao wenyewe, sasa hapa kwenye kifungu hichi hapa nafikiri ndio pa kuanzia kuanza kudhibiti kwa ajili ya wale ambao watapewa zile leseni za kufanyia biashara ya utalii hapa Zanzibar basi wawe Wazanzibari wenyewe, wengine watakapoajiriwa basi waajiriwe kama wageni na waajiriwe kwa mikataba maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 19(a) ambacho kinafanyiwa marekebisho nitaomba kidogo nikinukuu kinasema. "Mtu haruhusiwi kufanya biashara ya utalii anayefanya mabadiliko katika ofisi yake au jengo linalohusiana na kurugenzi jina la biashara",

Mhe. Mwenyekiti, hii nadhani mwenzangu kaizungumza sina haja ya kuzungumzia tena kwa sababu katika masuala mazima ya wawekezaji kuna taasisi maalum ambayo ZIPA wao ndio wanashughulikia wale wamiliki wa ile hoteli.

Lakini vile vile kifungu cha 2 kinasema endapo kamisheni itaridhika kwa mapendekezo ya marekebisho yaliyokusudiwa yanaweza kuruhusiwa kwa maandishi, sasa hapa ndipo ninapopataka. Sasa hivi tunamshukuru Mhe. Rais wetu sheria ikishapitishwa tu haichukui muda tayari anaisaini, sasa hii sheria akisha kiusaini itakuwa hii kazi ya kamisheni na kwa kuwa kutakuwa kunaundwa zile kamati za Wilaya kamisheni sasa itoe miongozo hasa kwa hizi kamati za wilaya, kuhakikisha kwamba ujenzi wote ambao unafanyika mpya katika maeneo yetu hasa katika maeneo ya fukwe basi lazima uweze kufuata taratibu na uweze kupata leseni kutoka Kamisheni.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, utakuta watu tayari wameshavunja sheria, watu wanachimba fukwe na katika fukwe wanaanzisha *Restaurant* lakini bado kamisheni ya utalii wanaendelea kutoa vibali vya kufanyia biashara, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hii sheria tutakuwa tunatunga sheria lakini sisi wenyewe tutakuwa hatuzifuati na hawa

wawekezaji sheria zetu wanakuwa wanazijua. Lakini wakishaona hatuzifuati basi wao ndio wanaendelea kuzivunja kwa sababu wanakuwa wanakopiana kwa ajili ya kuvunja sheria.

Mhe. Mwenyekiti kifungu cha 23(a) namalizia Kamati za utalii za wilaya mimi kamati yangu keshokutwa nikija kusoma ripoti mtakuja kuona, hasa katika maeneo ya Nungwi huku sasa hivi ufuska umezidi kuna siku maalum wanaita kitu kama *fullmoon* kitu kama hivo, lakini siku hiyo wanatoka vijana mjini mashamba kila sehemu wanakwenda huko huko siku ile inakuwa ndio ule mwezi mkali ule watu wanacheza bichi, wanaita *fullmoon* huko hatari, tena siku moja hebu vaa miwani uende na wewe. Utakwenda hiyo miwani itavuka wakati ipo kwenye maji.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tuzingatie muda.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mheshimiwa lakini hizo ngoma wanazocheza hapo na hivyo walivyovaa unaweza kuniuliza Mheshimiwa Mwenyekiti wa wenyeviti uliona vipi, huko nilikwenda kufanya *research* na nikaona yasiyoonekanwa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nakuomba wewe siku moja ufuatane na Mhe. Waziri ukisikia kuna *fullmoon* basi na wewe panda kidampa chako nenda kule utaona mambo yanayofanyika ndani ya Zanzibar hii, maadili yanavunjwa sana katika maeneo ya Nungwi kwa kweli kule kunahitaji nguvu za ziada.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa kamati hizi nafikiri hata juzi sisi tulikaa na Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tumekaa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuwaeleza namna gani kuweka zile kamati za ulinzi na usalama katika maeneo yale ili kudhibiti usalama katika nchi yetu.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kunipa nafasi hii, lakini namuomba sana Mhe. Waziri wizara hii aliyopewa aache muhali, katika sekta hii ya utalii ajira zote ziko huku, ukiwa na muhali vijana wetu watakosa kazi watakuja kutupiga ngwara muda pale unapofika. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru naunga mkono hoja. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa ya kuchangia mada hii iliyopo mbele yetu ya marekebisho ya sheria ya utalii, kwanza na mimi nataka niungane na wenzangu kumshukuru sana Mhe. Waziri kutuletea mswada huu katika kipindi hiki ambacho kuwa utalii umetajwa kwamba ni moja ya uti wa mgongo au unaotuletea mapato katika nchi yetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia nataka niungane na wenzangu kusema kama Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa utalii unatuletea mapato katika nchi yetu lakini tunatakiwa tuangalie je, huu utalii tunaoufanya na tunaoupenda? Je, unakwenda katika zile mila zetu, maadili yetu na silka zetu. Sasa lazima tujikosoe kwa makosa yetu sisi wenyewe, kwa sababu mimi nakiri kabisa kwamba watalii wanafuata sheria za nchi wanayokwenda lakini sisi ndio tunaowasababisha watalii aidha kwenda uchi au kuvunja maadili yetu, kswa sababu sheria zetu ndio zinawapa .

Nakumbuka wakati wa Marehemu Mzee Karume waataalii walikuwa wakiingia tu basi tayari wanavaa vikoi wanavaa shati vizuri, hasa mimi napenda kusema watalii ni watu wanaopenda kucheza wao wakielimishwa tu sasa hivi kwamba wavae nguo watavaa nguo na wataona kama wao wanakaa kama wazanzibar, kwa sababu tunaona hivi sasa baadhi yao wanakuja wakiona watu wanavaa nguo na wao wanavaa watalii ni watu ambao wanapenda mambo ya ucheza. Juzi nazungumziwa na rafiki yangu kama alikwenda kumkuta mzungu mmoja mtalii kuna uganga unapigwa pale basi na yeye alikuwa mchezaji mkubwa wa Uganga na yeye alikuwa mchangamfu mkubwa kuliko wale wenyewe. Kwa hivyo watalii ni watu ambao wanapenda ucheza sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sekta hii ya utalii ipange taratibu zake vizuri wazungumze na watalii na sio wakaidi kufuata, waone kama kidogo wanapunguza na wanafuata maadili yetu na nyenendo zetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninalotaka nilizungumze ni suala alilolizungumza jana Mwenyekiti wangu wa kamati Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na mimi suala hili nataka nilizungumze kwa nguvu zangu zote kwa sababu ni suala ambalo linanisikitisha. Mhe. Mwenyekiti, wazee wa kale wanasema bandu bandu huisha gogo na ukiacha mwana kulia mara unakujal kulia wewe.

Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ina sheria na taratibu vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi vilitayarishwa kwa ajili ya Wazanzibari lakini leo inasikitisha kuona vitambulisho wanapewa watu wageni wanaokuja kwa kufanya kazi za utalii tu na mfano hai aliuonesha Mhe. Makame Mshimba na ushahidi akaonesha,

inakuwaje leo wanakuja wamasai kwa ulinzi tu lakini wao wapewe vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, kuna watu wamekuja Zanzibar kutoka Ruanda, Burundi wamekuja kwa ajili ya kufanya kazi ya utalii lakini watu hawa ndio wanaopewa vitambulisho vya Mzanzibari lakini anaachwe Subeti ambaye kuwa ni Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti inasikitisha tutafika mahali Wazanzibari tutakuwa kama Wapalestina, Wapalestina walianza hivi hivi taratibu hivi ni visiwa na wenzetu walianza taratibu hivi hivi leo sasa hivi Wapalestina hawana nchi na Waizrail ndio wenye nchi, inakuwaje vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi vina sheria mtu mpaka awe na cheti cha kuzaliwa. Leo masheha wanawapa watu vyeti vya kuzaliwa kwa sababu ndio wanaowapa karatasi kwenda kuchukua vyeti vya kuzaliwa, kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, masheha ndio wanaotuharibia nchi hii haiwezekani mtu kaja kwa ulinzi tu wa hoteli yeye awe ana kitambulisho hiki, tunaelekea wapi hivi tumefikiri mara ngapi.

Mhe. Mwenyekiti, kila siku tukiambiwa inapangwa bajeti au wanapanga utaratibu wa uchumi wa nchi kuna mambo ya wakati mfupi, wakati mrefu na wa baadae hivi mnatizama hapa tu hamtizami mbele kwa nini mnatizama hapa chini, lazima tutizame na mbele tunakokwenda nchi hii tunaipeleka wapi jamani viongozi wetu nchi hii tunaipeleka wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna uwezekano mimi naomba iundwe kamati ya kuchunguza utaratibu wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, na iundwe kamati ichunguze kwa sababu haiwezekani Mkurugenzi anatupeleka wapi vitambulisho vinatolewa tu wanapewa wageni, jamani tusitizame leo tutizame na kesho nchi tunaipeleka wapi tusijitizame sisi tutizame na kizazi chetu cha baadae kinachokuja. Jamani sisi ni wachunga tumepewa dhamana tutakwenda kuulizwa na Mwenyezi Mungu uchunga wetu tuliouchunga huu tumeuchunga jee, tumepewa madaraka ya nchi halafu tunaiuza tunawauzia watu nchi yao jamani, sisi leo ni viongozi kesho tutaondoka watakuja wenzetu, tusifanye hivi jamani kwa nini kila siku atunapiga kelele lakini hatusikilizwi.

Mhe. Mwenyekiti, hivi vitambulisho vimefanywa kama roho ya nchi yetu sasa hivi hupati kitu chochote kama huna kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, leo tunawapa watu milki wasizokuwa nazo wale watu ambao kuwa wana milki ya nchi hii hawapewi wanapewa wageni kwa sababu tu tunatizama mambo ya kupiga kura, tuzitazameni kura tutizame na hii nchi kuna mangapi tuliyoyafanya huko nyuma lakini sasa hivi tunajuta. Tumeshatanabahi kwamba tulikosea sasa kupapatua ndio kazi jamani kufanya kitu mwanzo ni mara moja lakini huku nyuma ukimpiga mtu ni mara moja kumipiga, lakini sasa utakuja kuulizwa unampiga kwa nini sasa hii sababu ya kumpigia hii ndio matatizo. Leo tunawapa vitambulisho watu wanakaa navyo vina umuhimu wanawakosesha watu wenye haki ya kupewa tunawapa watu wasiohusika jamani vitambulisho vya Mzanzibari tokea lini na mmasai jamani.

Mhe. Mwenyekiti, tunaelekea wapi kwa hivyo Masheha na hawa wahusika wa vitambulisho lazima naomba kama kuna uwezekano iundwe kamati wachunguzwe wasiohusika wanyang'anywe wote, haiwezekani hivi jamani.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala la maadili jamani, hivi jamani Wazanzibari hivi sasa maadili yetu yeshakuwa ni kuvaa suruali wanawake ndio maadili yetu hayo jamani, nchi ikenda kama haina sheria tutafika pahala pabaya kweli kweli na sheria zipo lakini kule kufuatiliwa utekelezaji wake jamani kila saa tunakuja humu kupanga sheria lakini kutekeleza ni ugumu, hivi maadili yetu Wazanzibari ni wanawake kuvaa suruali. Kwa sababu sasa ndio limekuwa vazi kubwa ukizungumza unaambiwa haki za binaadam,. Jamani Mzee Karume nae wakati huo haki za binaadamu zilikuwa zipo na akizichunga, akija mtu kavaa suruali nyembamba inachanwa na mikwaju akichezea, akija mtu na nywele za kimaajabu ananyolewa hivi Mzee Karume yeye alikuwa hajui kama kuna haki za binaadam.

Jamani maadili yetu tunayapoteza naomba lazima tuwe na sheria na sheria tuziheshimu, hivi sasa tupo pahali pabaya kweli kweli na sisi Wazanzibari sasa tunafuata kwa sababu badala ya kuja watu na maadili yao ya kutoa na sisi tunafuata tunapotoshwa naomba na hili liangaliwe.

Suala jengine ambalo naomba kulizungumza ni kifungu cha 23 kuundwa kwa hizi kamati za utalii za wilaya, katika hawa wajumbe wa kamati hizi hapa kuna mjumbe ambae inasema katika hao wajumbe kuna kifungu kimeandikwa kwamba mfanya biashara katika wilaya nae ni mjumbe, basi na mimi napendekeza hata kama ni mfanyakazi katika wilaya lakini aonekane yule aliyekuwa ni mfanya biashara lakini ile ya utalii. Katika ile Wilaya yule mfanya biashara ambaye yumo katika ile fani ya utalii basi naomba apendekezwe zaidi kuliko mfanya biashara kumbe anauza matango, anauza mapapai aingizwe hapa. Lakini mimi napendekeza mfanya biashara katika wilaya lakini aliyekuwa ni mfanya biashara katika fani ile ya utalii.

Mwengine ambaye napendekeza ni huyu mtu mmoja kutoka Wizara ya Ardhi napendekeza asiwe mtu mmoja mfanyakazi wa Wizara ya Ardhi, kwa sababu anakwenda kuchukuliwa taarishi au mfanyakazi katika wizara ile ile ya Ardhi lakini ndio akachukuliwe yeye taarishi aingizwe pale, kwa hivyo awe ni Afisa mmoja kutoka Wizara ya Ardhi kwa sababu ndie atakayewasaidia. Nia na madhumuni hii kamati imekaa kwa ajili ya kuwasaidia watu sasa kama ni tarishi tu mule kwa sababu anafanya kazi katika Wizara ya Ardhi hatotusaidia, kwa hivyo naomba awe Afisa mmoja kutoka Wizara ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu chengine ambacho napendekeza ni hapa panapo kazi za kifungu cha 23 ambacho kinasema kamati za utalii za wilaya zitatekeleza majukumu yafuatayo. Sasa katika hayo majukumu kuna kifungu …

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe una dakika tatu za ziada.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Kuna kifungu hichi cha (c) kinasema kuanzisha mfuko wa fedha wa wananchi kwa njia ya michango ya hiyari ambazo zitatumika kwa maendeleo ya vijiji, mimi Mhe. Mwenyekiti kwa maoni yangu mimi hapa nasema kama pasiwe na michango ya wananchi kwa ajili ya kuendeleza hivi vijiji, bali ufanywe mfuko ambao utatokana na wale wale watalii waliopo katika zile sehemu za kijiji. Sasa huu mfuko mapato yale yapatikane kutokana na watalii kwa ajili ya kuwafaidisha wananchi lakini leo wananchi tuwachangishe tena wao kwamba wanataka kujiendesha katika hicho kijiji na wakati wana faida ya utalii pale haya faida yao ni ipi wanayoipata wao, itakuwa hawana wanachokipata.

Kwa hivyo na hapa napendekeza kama mfuko huu utokane na mapato ya wale wale watalii kwa ajili ya kuendeleza hivyo vijiji vyao kwa sababu watalii wanakwenda kukaa katika kijiji katika sehemu. Sasa wale wana kijiji kama hawana faida yoyote wanayoipata basi faida yao ni nini au faida yao ndio kuharibiwa maadili tu katika kijiji. Kwa sababu watalii wanapokaa katika kijiji karibu hakuna njia yoyote ile maadili yao yataharibika watu wa pale lazima yaporomoke.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Mhe. Hassan Hamad Omar alizungumza hapa tulikwenda kwenye semina tulikwenda Kiwengwa.Tulivyofika tulikuta watu kwa sababu wamekwenda katika eneo la utalii, walikuwa wanacheza ngoma mpaka nguo wanazivua zote.

Hayo maadili yanatengenezwa au yanaharibiwa. Mhe.Mwenyekiti, hili suala la maadili linataka litiliwe mkazo kweli kweli.Naomba Mhe.Waziri angetunga hasa kipengele maalum cha kutunza maadili, na mtu yeyote yule atakayekuwa amevunja maadili katika sehemu ya kijiji kile, achukuliwe hatua za kinidhamu, kuliko kuachilia tu hivi.

Mhe.Mwenyekiti, suala jengine ninalotaka nilizungumze kwa uchache kabisa kwa sababu muda wangu ni mdogo. Mheshimiwa umezungumza kama mwenyekiti aongezewe mafao au mapato, mimi napingana nalo kama Mhe. Hamza Hassan Juma alivyosema, na mimi naunga mkono kwamba asiongezewe mafao ya aina yoyote ile.Kipato chake kiwe kile kile sawa sawa na mapato wanayopata wenye viti wengine, lakini asiongezewe kuwa awe na mapato mengine.

Mhe.Mwenyekiti, kwa hayo machache na kwa kuheshimu muda wako naunga mkono hoja.

Mhe.Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti, na mimi kupata fursa hii mchana huu kuchangia Mswada huu wa Kuanzishwa Sheria ya Marekebisho ya Utalii. Kwa kweli na mimi niungane kwanza na ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati aliyoiwasilisha hapa mbele yetu jana.Yale yote aliyoyatoa kama ni changamoto, na mambo mbali mbali ambayo waliyaona kwenye sheria hii.

Ni kweli kwamba utalii ni “Uti wa Mgongo” wa mapato ya nchi yetu, na asilimia 80 ya mapato yetu inaonekana yanachangiwa kutoka kwenye utalii. Kwa maana hiyo utalii ni sisi wenyewe tutakaoufanya ukawa endelevu, na tukaweza kuu- *promote* kwa vile njia zilizokuwa ni sahihi kabisa.
Mhe.Mwenyekiti, kila jambo inakuwa kasoro haziwezi kuondoka, lakini ni jukumu letu sasa kuona kwamba ni namna gani utalii huu utaleta faida na hautaleta matatizo.Kwa kweli ni lazima tufate maadili ya nchi yetu, tusijaribu kuleta mambo ambayo yataharibu ule utamaduni wetu.Wenzangu wameshasema sana kwa hilo na mimi kuanzia tu nianze na huko, niseme kwamba utalii sasa ni lazima tuurekebishe ili tuone utalii unaleta sura mpya kabisa.

Mhe.Mwenyekiti, wenzangu wamekuja kwenye tafsiri ya Uzanzibari na kama kutoa fursa basi sekta hii iwasaidie zaidi Wazanzibari.Tunaona kwamba kuna vijana wetu wengi hawana kazi, wanazurura.Lakini kutokana na wageni kuvamia kazi nyingi zimekuwa zinafanywa na wageni.

Mhe.Mwenyekiti, niende kwenye kifungu moja kwa moja Sehemu ya Pili ya marekebisho inayosema "Mtalii maana yake ni mtu ambaye yupo katika sehemu ambayo sio makaazi yake, lakini yupo kwa ajili ya kazi, mapumziko au starehe".Mimi ningeomba hii starehe ingeondoka ikiishia hapa "kwa ajili ya kazi au mapumziko". Mtalii nahisi hata sisi wenyewe tunaweza kuwa watalii kwa kutembelea sehemu mbali mbali, ile pia inaingia kwenye utalii. Utalii si lazima mtu awe kutoka nje, hata sisi wenyewe kuna sehemu mbali mbali za kihistoria, kwa hivyo tunaweza kwenda kutalii, ili kuongeza pato la taifa na vile vile kusoma mambo mbali mbali.

Mhe.Mwenyekiti, kwenye Kifungu (a) kuingiza maneno na kuhusiana baina ya maneno ndani (katika tafsiri ya neno muungoza utalii na) kwa kweli mimi hapa sijafahamu, angalau ingekuja labda ni sentensi nzima nikajua ni namna gani. Hapa kuna maneno kwa kweli yananitatanisha sikujua ina ufafanuzi wake. Nahisi tu kuingiza maneno "kuhusiana na baina ya maneno" ndani "Zanzibar" katika tafsiri ya neno muongoza watalii".Kwa kweli hapa nimeshindwa kabisa kuifafanua.

Mhe.Mwenyekiti, nende kwenye kifungu cha 5 kamisheni itakuwa na mwenyekiti atakayekuwa Mkuu wa Kamisheni kwa muda wote na ambaye atateuliwa na Rais. Hili sina tatizo lakini bado tunatawaliwa na mfumo dume. Maana yake wajumbe wote hawa halafu mwisho ndio ikatiwa kwamba mjumbe mwengine yoyote ambaye atakuwa ni mwanamke.Kwani hapa kwenye hizi zote kuna kikwazo gani ambacho mwanamke hatokuwa. Jumuia ya watembezaji na kusafirisha watalii, Tume ya Mipango Zanzibar, ndiyo tume yenyewe, Mkurugenzi, Mipango, Sera na Utafiti, lakini mwisho ndio akawekwa mwanamke. Kwa hivyo hapa nahisi bado ule ushiriki hasa wa mwanamke bado kwenye vyombo mbali mbali bado haujakubalika.

Kifungu cha 5(3) "Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, mpaka awe:

(i) Na utaalamu wa kipekee katika fani inayofanana na utalii, uongozi wa wadau wa utalii au uhusiano wa kimataifa, ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo."

Na hapa vile vile ingawaje wenzangu wameshasema mambo yapo mengi.Kwa hivyo hapa ni lazima parekebishwe.Ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo.Mambo gani hayo hayajajulikana.Kwa sababu mambo yapo chungu nzima.

Mhe.Mwenyekiti, nikitoka hapo niingie kwenye kifungu cha 9 chengine ambacho kinasema

Kifungu cha 9 "Uamuzi wa Makamishna utakuwa kwa kukubaliana, lakini ikiwa watashindwa kufikia makubaliano katika ajenda yoyote, ajenda hiyo itaamuliwa kwa kura, na ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi".

Hili sina tatizo nalo, isipokuwa nisisitize tu kila mahali isipokuwa kuna upataji wa zile haki za msingi.Kama kawaida, kwa sababu ni nchi ambayo tumekubali utawala bora, hili ni jambo ambalo limefuata misingi ya kidemokrasia.

Kifungu cha 9(A)"Makamishna watalipwa mafao kama Waziri atakavyoamua"
Kwa kweli na mimi hapa sijaona usahihi wa kuwa mpaka Waziri atakavyoamua. Ni kuwe kitu sahihi, iwe ni lazima isiwe mpaka waziri atakavyoamua, kwa kuwa ile ni haki yake. Tukisema atakapoamua tu nahisi kama si lugha ambayo ipo sahihi.

Kifungu cha 11(1) "Kutakuwa na Katibu Mtendaji ambaye atakuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kamisheni atakayeteuliwa na Rais.

(a) Awe na angalau shahada ya kwanza au elimu inayolingana na hiyo na uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichopungua miaka saba"

Kwa kweli uzoefu ni jambo la maana sana, na hata uwe na digirii ya aina gani, kama hukuwa na uzoefu huwezi kufanya kazi vizuri. Kwa hivyo hapa mimi sina matatizo kwa kifungu hiki, isipokuwa lazima watu wawe na taaluma ya kile kitu wanachotaka kukifanya.

(b) "Mwenye dhamana ya usimamizi wa fedha, mali na shughuli za Kamisheni."

Lakini vile vile juu ya dhamana hizi, ni lazima kila mtu afuate uwajibikaji, vile vile ni lazima kwenye shughuli hizi tuwe wawazi, nidhamu, uadilifu na uaminifu. Kwa hivyo kila mtu ni lazima awajibike kwa ile shughuli tunayoifanya.

Kifungu cha 1I (A) (i) "Mkutano wa wadau wa utalii utafanya kazi zifuatazo".

Unaanzishwa mkutano wa wadau wa utalii utakaofanyika kila baada ya miezi sita unaozungumzia mambo yanayohusu maendeleo ya utalii.Mwenyekiti wa Kamisheni atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa Wadau wa Utalii. Kwa kweli lazima kila penye taasisi na kila penye mkusanyiko wa watu, na hasa taasisi ni lazima kuwepo na utaratibu wa uongozi uliokuwa sahihi kabisa, ili lengo na madhumuni ni yale yale kufanikisha au kuleta ufanisi katika kazi zetu mbali mbali.

Kifungu cha 14 marekebisho ya kifungu cha 12 cha Sheria mama kinarekebisha kufuta aya (a) ya Kifungu cha (2) na kuweka badala inayosomeka kwamba, "kiwango chengine cha fedha kama ruzuku kama zitakavyotengwa na Baraza la Wawakilishi", Ni sawa sawa kwamba ruzuku zinakuwepo lakini vile vile ni lazima zile ruzuku vile vile vifuate ile misingi ya uwajibikaji, na kutumia fedha kihalali kwa kutumia zile *instruction* za fedha.Kwa sababu ni jambo ambalo tumejiamini, ni lazima vifuate uadilifu ili yale malengo yetu ambayo tumeyakusudia yawe yamepatikana.

Mhe.Mwenyekiti, kwenye kifungu cha 16 cha sheria mama kinarekebishwa, marekebisho ya kifungu cha 16 kinasema (a) katika kijifungu cha kwanza kwa kufuta maneno "Mkurugenzi Mkuu" na badala kuwa neno "Katibu Mtendaji". Kwa kuongeza vijifungu vipya (3) na (4) kama ifuatavyo "Endapo kama leseni iliyotolewa chini ya kifungu hichi inapotea, itaharibu kamisheni, inaweza kutoa nakla kwa leseni hiyo badala ya kulipwa ada iliyoelezwa katika kanuni"

Mhe.Mwenyekiti, napenda kusema hii leseni iwe inakuwa *renewered* ili serikali iweze kupata mapato zaidi.Iwapo mtu atachelewa ku- *renew* basi ni lazima kuwe na faini ambayo atatozwa, ili mara ya pili aone kwamba ni lazima kila baada ya muda abadilishe kama tunavyobadilisha leseni za vyombo vyetu au kwenye maduka yetu. Awe anajijua kwamba tarehe fulani natakiwa kubadilisha leseni yangu. Marekebisho ya kifungu cha 18 katika kifungu cha kwanza kwa kufuta neno "aliyokubaliwa" na badala yake kuweka neno "anayehudumiwa".Mimi niseme kwamba kifungu hiki sina tatizo nacho.

Kifungu cha kazi za Kamati ya Utalii ni sawa sawa sina tatizo nacho, lakini kuna kifungu cha 23, kifungu cha 24, Sheria Mama. Marekebisho ya kifungu cha 24 vile vile kuna mtu yoyote anayefanya biashara ya utalii aliyeajiri mtu ambaye sio Mtanzania kutoa huduma iliyoelezwa chini ya kifungu cha (1) cha kifungu hichi, lazima apate ruhusa ya maandishi kutoka kwa Waziri baada ya kumthibitisha waziri kuwa hakuna mtu wa ndani wa kujaza nafasi hiyo.

Vile vile kwamba mtu kama huyu ambaye atakayemuajiri basi kuwe na kipengele ambacho kitamzuia kumuajiri mtu wa nje, na hiyo itatupa fursa sisi Wazanzibari.Kwa sababu kama atamuajiri mtu wa nje basi kuwe na *charge* kubwa zaidi ambayo itamfanya kwamba asiweze kumuajiri mtu wa nje isipokuwa amchukue Mzanzibari.Kwa hivyo ni lazima tubadilike badala ya kuwa mtu anamuajiri mtu wa nje kwa maslahi yake.

Hili ni tatizo kwamba tunaona kwamba wale Ma-PO wanaokuwepo wanakuwa si Wanzanzibari na wala hawana damu ya Kizanzibari, na hata yale mapato yetu yanapotea.Ndio maana hata kama zikisemwa pesa nyingi kutokana na utalii zinakuwa zinapotea kwa sababu wale Ma-PO sio Wazanzibari, kwa hivyo wanaweza wakafanya ubabaishaji wowote na hata ukienda huko kwenye hoteli wanakuwa hata yale mabuku ya wageni yanakuwa ni tofauti.

Vile vile Mhe.Mwenyekiti, niseme kwamba utoaji wa viza kutoka kwa watalii wanaokaa nje, viza zinakatwa kule moja kwa moja. Kwa hivyo hapa tunakuwa hatuna mapato yoyote tunayoyapata, kwa hivyo pale pia zinakuwa zinapotea fedha zetu.Vile vile tuone kwamba ni namna gani wale wageni wanaotoka nje basi waje moja kwa moja

na waje wachukue hapa viza zao kama sisi tunapotoka nje viza tunakwenda Uwanja wa Ndege tunapata visa.Ni lazima tubadilishe sera zetu za utalii.

Mhe.Mwenyekiti, kama kawaida yangu mchango wangu unakuwa hauchukui muda sana.Nakushukuru Mhe.Mwenyekiti.

Mhe.Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia kidogo Sheria ya Marekebidho ya Sheria ya Utalii.Awali ya yote kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuumba, aliyetupa uwezo leo wa kusimama hapa kwa afya njema.

Pili napenda unipe ruhusa kuchukua fursa hii kutoa salamu zangu za rambi rambi na pole kwa wafiwa, ndugu jamaa na marafiki wa marehemu, mpenzi wetu Mhe.Mtondoo ambaye ametutoka, tulikuwa tunampenda lakini Mwenyezi Mungu amempenda zaidi. *Innalillahi wainna ilaihi Rajiun*.

Mimi nitaanza moja kwa moja katika ukurasa wa 42.Katika kifungu cha 5 ni kuhusu muundo wa kamisheni.Mhe.Mwenyekiti, imetokea hapa kwamba kamisheni itakuwa, na kuna kipengele (a)(b) katika kipengele cha (b) kinaonesha wajumbe mbali mbali ambao watakuwa katika kamisheni hii. Mimi nilikuwa naomba kwamba tuongeze na kipengele cha "tuwe na mjumbe mmoja ambaye atatoka katika Idara ya Mazingira.''

Mhe.Mwenyekiti, nina sababu zangu kwa nini nikasema hivyo.Tumeutaka utalii uje utunufaishe katika nchi yetu.Lakini utalii huu huu sasa hivi unatuumiza na unatuumiza katika maeneo mbali mbali. Sina haja ya kutaja lakini moja katika eneo kuu ambalo linatuumiza ni sehemu ya mazingira yetu.Mazingira yetu yanaharibika na kwa sababu hao tuliowapa sehemu za kujengea, ambazo tulikuwa tuna tamaa kwamba watafuata taratibu zetu, lakini matokeo yake hawazifuati na wanapindukia mpaka.Kama walifuata hapo nyuma lakini sasa hivi hawafuati.

Sababu ya kuwekwa taratibu hizo ni kwamba, yale maeneo ambayo wameambiwa wasijenge ni maeneo ambayo wanaishi viumbe wa baharini. Eneo la fukwe kuna viumbe wengi ambao sisi hatuwaoni na wengine tunawaona wanaishi katika maeneo hayo.Kuna *species* nyingi ambazo katika sehemu nyengine duniani hazipatikani, kule zinapatikana. Zanzibar tunaanza kuzikosa, ni makosa makubwa tunafanya.

Pili, kuna sehemu za *corals* ambazo ni nyumba za viumbe wa baharini, lakini wawekezaji wetu wanakwenda kujenga katika sehemu ambazo wanaishi viumbe wengine, ni makosa.Kuna Mheshimiwa mmoja amesema hapa kwamba tunawaogopa.Inaelekea tunawaogopa kweli. Kwa sababu sisi ndio wenye mamlaka ya kuwaambia wao wasifanye hivyo, wao watafanya wataharibu kisha wataondoka, tutakaoumia ni sisi na vizazi vyetu.Kesho tutakuja kuwaambia nini vizazi vyetu, kwamba tuliyaona tukayanyamazia. Mimi namuomba Waziri hili alitilie maanani sana.Ujenzi wa hoteli Zanzibar unajengwa kiholela kwa makusudi, na kama tutaendelea hivi basi tutaharibikiwa sana. Nchi nyengine wamefanya makosa hayo, na matokeo yake sasa hivi wanajuta kwa nini utalii umekuja.

Mimi nafikiria Mhe.Waziri umeingia katika Wizara, lakini Wizara hii watu wanafikiria ni nyepesi, lakini hii wizara ni nzito.Huu ni Uti wetu wa Mgongo, kwa hivyo Mhe.Waziri tunakuomba sana uangalie suala zima la mazingira yetu.Tunataka utalii utuletee faida na sio hasara. Kwa hiyo naomba kipengele hichi ikiwa kama atatolewa mjumbe huyu ambaye anaambiwa ni mjumbe yoyote awe mwanamke, lakini lazima awe anatoka katika Idara ya Mazingira.

Katika kifungu hicho hicho cha 5 naingia kifungu kidogo cha 3 kinasema kwamba "mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti mpaka awe" kifungu kidogo cha pili mimi ningependa iongezwe "ujuzi na uwezo" nafikiria hapa imetafsiriwa ujuzi maana yake ni *skills.*

Lakini unaweza uka – *acquire skills* lakini usiwe na uwezo wa kufanya jambo, na hapa mwisho imeandikwa kwamba "ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo.Mambo yepi? Amesema hapa Mheshimiwa kila anachoweza kupigania tutasema kwamba kuna anayepigania suala jengine tutasema huyu anafaa.Hapa ibainishe ni mambo yepi.

Kifungu cha tatu vile vile kinasema kwamba mahusiano mazuri na watu.Mimi nafikiria kwamba "mahusiano mazuri na watu wa mataifa mbali mbali" kwa sababu hapa tunawahudumia watalii, lakini isiwe watu tu *in general,* lakini wawe watu wa mataifa mbali mbali.Hiyo ni sifa ambayo anatakiwa Mwenyekiti awe nayo.

Kifungu cha 6(1) "Mwenyekiti wa Kamisheni atakuwa siyo Mkuu wa Utawala na atafanya kazi zifuatazo:

(c) Kuwa mbele katika kuanzisha dhana ya utalii kwa wote."

Mimi hapo nimefikiria iwe "kuwa mbele katika kuanzisha na kuendeleza" tusiwe tunajua kuanzisha tu, tujue na kuendeleza, kuwa mbele katika kuanzisha na kuendeleza dhana ya utalii kwa wote. Hapa kidogo nilikuwa nafikiria kwamba tutakuwa na kipengele vile vile cha Mwenyekiti wa Kamisheni kuwa na dhima ya kusaidia katika kukuza utalii wa ndani.

Mhe.Mwenyekiti, nchi nyingi duniani zinapata sehemu kubwa ya pato lake kwa kutumia watalii wa ndani, mfano mkubwa ni China.China pato lake kubwa la utalii linategemea watalii wa ndani.Sisi bado hatujaweza kuhamasisha wananchi kutumia mali asili zao na mambo mengine ya kitalii ili serikali ipate pato. Kuna sababu nyingi najua moja umasikini nao unachangia, lakini wapo ambao wana uwezo wa kutumia, kwa hiyo tujaribu kusaidia wananchi wafahamu umuhimu wa kutumia maeneo ya kitalii, ili kwamba na wao vile vile waweze kuchangia katika pato la kitalii ni muhimu sana.

Mhe.Mwenyekiti, najua muda unatukimbia.
Katika kifungu cha 10 (2), 9(a) kinasema malipo ya Makamishna, kinasema kwamba,
Kifungu cha 9(A) "Makamishna watalipwa mafao yao kama Waziri atakavyoamua. Mimi nafikiri hii tusiseme kama Waziri atakavyoamua" .

Kama Waziri atakavyowapangia, kwa sababu tukisema leo tunavyosema hapo tunakuwa tumeiacha hii *sentence*.Ukisema waziri atakavyoamua kesho akikaa kikao anaweza akaamua wapate 50, kesho kutwa 100.Lakini apange utaratibu maalum wa kuwalipa makamishna.Kwa hivyo naomba vile vile kipengele hichi kiwekwe sawa.

Katika ukurasa wa 49 ambao ni wa mwisho kabisa. Kifungu cha 23 ambacho kuna sheria ya 24 ambayo imefanyiwa mabadiliko, mwenzangu na nafikiri na wenzangu wengine wamejaribu vile vile kuzungumzia suala hili.Suala Nam. 3 "mtu yeyote anayefanya biashara ya utalii aliyeajiri mtu ambaye sio Mtanzania inaaendelea". Hapa na mimi vile vile naomba Mhe.Mwenyekiti, nitie maneno yangu.

Mhe.Mwenyekiti, hili suala ni zito, moja katika sababu kuu ya utalii kuja katika nchi yetu ni kutengeneza ajira, vijana wetu hawana ajira hilo ni moja.Kujipanga tulishindwa kujipanga vizuri. Sawa tunakubali makosa kwa sababu ilikuwa mwanzo kabisa tutengeneze *human resource* hapo kidogo tulikosea, lakini tunaweza kwenda mbele. Lakini sasa tunao vijana wa kutosha. Kinachosikitisha kila hoteli ambayo unakwenda, Wazanzibari ambao unakutana nao wanafanya kazi pale, hata zile kazi za chini ni wachache au hamna kabisa. Hivi kwa nini? Ni kweli kwamba watoto wetu hawataki kufanya kazi au wanabaguliwa.Mimi nina wasi wasi tunabaguliwa Mhe.Mwenyekiti. Tunabaguliwa ndani ya nchi yetu na sisi wenyewe tumenyamaza kimya.

Lakini nasema Mhe.Mwenyekiti, hawa vijana wetu sio sawa sawa na sisi, watakuja siku moja watupige mawe.Hawa vijana wetu watakasirika mwisho kwa nini hawana ajira, Mwenyezi Mungu atunusuru tusifikie huko.Lakini tuwatengenezee, na ndio maana sisi sote tuko hapa.Sasa ikiwa katika utekelezaji wa sheria hii, sheria ipo kama hatukujipanga vizuri basi tutakuwa hatujafanya jambo lolote la maana. Sheria hizi zote zitakuwa hazina maana. Hatuna utaratibu mzuri wa kusajili vijana wetu wanaomaliza skuli na vyuo, tukajua wataalamu wangapi tunao ndani ya nchi hii.Hicho ni kitu muhimu na ni kitu kikubwa sana.Ili tuweze kuwa–*trace* wale vijana wetu zinapotokea kazi tuwape vijana wetu, lakini hatuna huo utaratibu. Hilo ni kosa kubwa.

Wenzetu nchi zinazoendelea wana utaratibu maalum wanajua, katika Mkoa gani kuna vijana wangapi wana ujuzi gani na ikitokea kazi wanapewa. Lakini sasa matokeo yake tunadanganywa kwa sababu hatuna utaratibu tunakwenda ovyo ovyo, matokeo yake na wao wanatufanyia ovyo sisi. Mhe.Mwenyekiti, hivi sasa hatuwezi kusema kwamba utalii umesaidia katika kutoa ajira Zanzibar, hilo tunajidanganya, hakuna kitu kama hicho.Lakini utalii umesaidia kuwapa ajira majirani zetu, hilo ni sawa.Na kama hatutokaa tukafanya kazi zetu vizuri Mhe.Mwenyekiti, tupo pabaya.

Naomba Mhe. Mwenyekiti, niseme licha ya kwamba vijana wetu hawapati kazi, lakini hata wakiwa kwenye makazi wananyanyaswa na wageni.Kwa sababu wageni wanapata kazi za ngazi ya juu wao wanawaona wale wa chini ambao ni Wazanzibari wapo katika eneo lao wenyewe. Umeyaona wapi duniani yanatendeka kama hayo.Wapo katika nchi yao wenyewe wananyanyaswa na mtu ambaye anatoka nje kwa kweli si haki.

Nawaomba watendaji wanaohusika wawe wakali kwenye hili.Wafanye kazi yao ili kuhakikisha kwamba tunanusuru hizi nafasi za vijana wetu.Wananyanyaswa kwenye hoteli.Tumesikia hapa watu wanasema wanawake wananyanyaswa.Mimi kama mwanamke sitokuwa tayari kusikia mwanamke mwenzangu kanyanyaswa na mgeni.

Mhe.Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kugusia ni kwamba katika hoteli zetu nyingi tuna wageni kutoka nchi za jirani ambao ni wafanyakazi katika kada ya *management*, anakaa miaka sita Zanzibar.Kwa nini hatuwapi masharti wanapokuja hapa wakasema kwamba wanataka kada ya *management* wakakaa miaka mitatu, wakawa –*train* vijana wetu wao ndio wakawa wanafanya kazi.Kwa nini hatuwapi sheria hiyo kuwambia, wanakuja wanafanya kazi tunawaambia muwa – *train* vijana wetu wao wachukue nafasi hizo, lakini sio mtu anakuja hapa anakaa miaka sita, akiondoka yule anapewa mwengine. Hayo ni makosa makubwa.

Sasa sisi tunaziweka sheria nzuri lakini tunakosea hapo kwamba hatuzifuatilii.Ikiwa leo muwekezaji anakwenda kujenga ndani ya pwani, Idara ya Mazingira imekwenda, imeona na bado anaendelea kujenga, anafanya jeuri, halafu hachukuliwi hatua, hata faini hapigwi. Jamani kuna njia nyingi za kupata pesa, hiyo ni moja.Waziri wa fedha hayupo lakini hiyo ni njia moja ya kupata pesa, anayejenga ndani ya fukwe au anayekiuka sheria za ujenzi apigwe faini kubwa. Na sisi tuwachukulie fedha zao kama wao wanavyotuharibia mazingira yetu, tuzichukue pesa zao. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilifanya kazi katika Ofisi ya Kamisheni ya Utalii, nilikuwa Ofisa Mahusiano, nikimsaidia Mkurugenzi.Tatizo moja kubwa sana wakati nilipokuwa ofisini pale, ofisi ilikuwa haipati fedha za kutosha za kuweza kujitangaza. Utalii tunasema kwamba unatupa fedha, lakini tutumie unapokuwa unapata fedha na ile fedha utumie kuendesha kile kitu au kukiendeleza kile kitu, ile Ofisi haipati fedha za kutosha.

Mhe.Mwenyekiti, naomba Waziri ahakikishe kwamba Ofisi ile inapata fedha za kutosha, ambazo zitaweza kusaidia katika kuitangaza Zanzibar. Tusitegemee kila siku kubebwa na Tanzania Bara.

Mhe.Mwenyekiti, ikiwa yatafanywa marekebisho ambayo nimeyapendekeza nitaunga mkono sheria hii.Nakushukuru Mwenyekiti. Ahsante (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe Mswada huu kwetu ni muhimu, na wachangiaji bado wapo wengi.Sasa ili tuweze kwenda vizuri na ratiba zetu, tumewaomba baadhi ya wachangiaji wawe wastahamilivu na tuwaachie nafasi wachangiaji wawili Mhe.Ashura Sharif Ali na Mhe. Ali Mzee Ali, ili wamalizie jioni, halafu tuwaombe Mawaziri sasa na waziri husika ili tuweze kumaliza kazi ambayo inatukabili mbele yetu.Baada ya maelekezo hayo nitoe tangazo ambalo limefika hapa kabla ya kuakhirisha.

Tangazo

Tunaombwa waheshimiwa wajumbe wote kwamba wageni wetu kutoka Arusha watafika kesho.Kwa hiyo tuwe tayari kuwapokea na kuwa nao na kuwapa mashirikiano kwa mujibu wa ratiba ambazo tumekabidhiwa. Baada ya maelekezo hayo sasa niseme kwamba tunaakhirisha kikao hichi hadi jioni ya leo saa 11:00.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Subhanahu Wataala aliyetujaalia uhai, uzima tukawepo hapa jioni hii kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. Pia nikushukuru na wewe Mwenyekiti wakati huu kunipatia na mimi fursa ya kuchangia mswada huu uliopo mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kutuletea mswada huu wakati huu muafaka ambapo mambo yetu yameanza kwenda mrama.

Mhe. Mwenyekiti, niseme nimepata nafasi hii hivyo nina furaha kubwa kwamba Mwenyekiti uliyekaa mbele yetu ni mwanamke mwenzetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kabla ya kuendelea na mchango wangu uniruhusu ninukuu yale maneno ya Rais wa mwanzo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Mzee Abeid Amani Karume. Hayati Mzee

Karume alisema: “Ili taifa letu liendelee lazima tunahitaji mambo manne, tuwe na ardhi, wawepo watu, ipatikane siasa safi na uongozi bora”.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia maneno haya ya kihistoria ya hayati Karume yananifanya niuchangie na mimi mswada huu japo kidogo katika sekta hii ya utalii. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sekta hii ya utalii kwa sasa tunaita sekta kiongozi ya kuweza kulipatia taifa fedha kwa asilimia 80. Ni kweli hilo halipingiki na ndivyo ilivyo, lakini tujiulize tukitumia yale maneno ya hayati Karume. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba ardhi tunayo je, tumeigawanya vipi katika matumizi yetu na sisi tukiwa Zanzibar. Ni ukweli usiofichika mwanzo tulipoanza kujikita katika sekta hii tuliingia kichwa na miguu bila ya kufanya tafiti za kina kuupokea utalii katika hapa nchini kwetu, jambo ambalo limepelekea kwa wakati huu kuleta hali ngumu na migogoro iliyokua si ya lazima katika utaratibu wa ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, tuliitumia ardhi yetu kwa kupokea wawekezaji wetu bila ya kuangalia kwamba ardhi hiyo tunaihitaji kuifanyia matumizi mengine. Ni dhahiri kwamba mipango yetu ya awali haikuonea huko katika sekta ya utalii na kujipanga kwetu. Najua kwamba ardhi hii tungelikua tumejipanga mipango mizuri kwa ajili ya kuelekeza nguvu zetu katika utalii kwa kuchagua ni kanda gani ambazo tunazihitaji ziwe na utalii, nadhani tungekua tumepiga hatua. Mhe. Mwenyekiti, tungelitenga maeneo yetu mengine kwa shughuli zetu za kilimo, ufugaji, viwanda na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, hali haikua hivyo, tulizivamia kanda za pwani na kuzitoa na kuupokea utalii na utalii wenyewe bila ya kufanyiwa tafiti, utalii huo ni wa aina gani, ni wageni gani, ni kiwango gani tunachokihitaji cha utalii huo. Sisi tuliingia katika utalii naweza kusema kwamba ni kweli umetuletea manufaa kwa upande mmoja, lakini kwa upande wa pili nao pia umetuletea athari.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba umefika wakati katika sekta hii kiongozi kwa ajili ya pato la taifa kuweza kutathminiwa, ni lazima tujiulize hapo tulipoanzia, tulipo na tunapoelekea kwa manufaa ya Wazanzibari. Hivyo tukiendelea kuutumia ardhi yetu ndogo ya nchi yetu kwa ajili ya kuitapakaa na kueneza hoteli ambazo hazina kiwango na ubora unaostahiki yawezekana baadae tukashindwa hata maeneo ya kilimo na makaazi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme sasa kwamba Zanzibar ina mila na utamaduni wake ambao utamaduni huo umekua ni kivutio kikubwa kwa wageni wetu wanapoingia nchini kwetu. Kwa bahati mbaya sana katika wakati huu utalii ukiwa umetapakaa kwa kweli tumefika pahala, nadhani nyote mtakiri ya kwamba umetuporomolea maadili yetu kwa asilimia kubwa. Na kwa nini yaporomoke maadili yetu? Yameporomoka maadili yetu kwa sababu hatukujiwekea utaratibu wa kuona ni kanda gani hasa zinafaa kuwekwa kwa ajili ya utalii, hatukuweza kupambanua ya kwamba sehemu hizi wanazokaa hasa wananchi wenyewe basi zilikua hazifai kabisa kujengwa hoteli kwa ukaribu wa aina hiyo. Sisi tuliona kwamba ni fukwe tu basi zikatumika fukwe hizo kwa ajili ya kujengwa hoteli hizo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia utalii kwa hapa kwetu ndio chanzo cha migogoro mikuu ya ardhi hapa Zanzibar pamoja na mengine yote lakini na hili limechochea kuwepo kwa migogoro ya ardhi hapa kwetu. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu leo tupo hapa kwa ajili ya kutengeneza sheria ambayo ikitumiwa vizuri ipaswavyo kwani tumezoea mara nyingi na tumeona kwamba tuna sheria nyingi zimepitishwa, lakini matumizi yake yamekua dhaifu, imefika mahala sasa iko haja ya kuona sheria hii ya utalii inafanya kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, utalii tulionao sasa kwa kweli hauna tija kwa wananchi wetu, wale ambao wamebahatika kupata ajira, basi mishahara yao haieleweki, unyanyasaji umekua mwingi, matatizo mengi wakufuatilia matatizo yao vijana hao angalau wamepata hiyo ajira basi pia hawaonekani.

Kwa hivyo, hili ni tatizo hawa ndio Wazanzibari, hawa ndio wananchi, hawa ndio wazalendo, hawa ndio wenye rasilimali ya taifa hili, wana haki sawa kimsingi na kikatiba katika nchi yao. Hivyo basi Mhe. Mwenyekiti, umefika wakati tutunze mila na silka za Wazanzibari ili kivutio hicho kiweze kuwavutia wageni wetu wengi wanaoingia hapa. Lakini pia tuone kwamba utalii huu haupotezi mila, silka na utamaduni wa Zanzibar ambao unasifiwa kote duniani. Mhe. Mwenyekiti, historia mimi nakumbuka miaka ya nyuma akija mgeni akisahau kitu chake sehemu yoyote ile basi kitatunzwa na hatimae atakipata. Lakini je, tujiulize hali tuliyonayo sasa hivi hapa kwetu utamaduni ule bado upo? Je, yale ambayo yalikua yakitendeka kwa Wazanzibari kama ni mila na silka zao leo yapo?

Mhe. Mwenyekiti, ukija kwenye mavazi ya Kizanzibari ambayo wenzetu yaliwavutia sana na mara nyengine walikua wakishangazwa. Mhe. Mwenyekiti, nikirudi kule kule kwa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume nadhani

sote tunakumbuka kihistoria kwamba wakati wageni wanapoingia katika taifa letu basi mara nyingi aliweka sheria kuwa mgeni ambaye ataingia Zanzibar hakufanana na mila na silka za Wazanzibari kimavazi basi aliwekewa utaratibu maalum na nguo maalum kwa ajili ya kupewa. Mhe. Mwenyekiti, leo hilo limepotea hatujui liko wapi na sisi tuliopo ni Wazanzibari tena ni warithi kabisa wa yale mazuri aliyotuachia hayati baba Karume.
Mhe. Mwenyekiti, hali hii tukiacha iendelee basi nasema kwamba historia ya Zanzibar itapotea na tutasahau kwamba kizazi chetu hakitojua historia yake, hakitojua silka yake na utamaduni wake, jambo ambalo ni kosa kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ipo haja ya kuona wakati sasa umefika wa kujiwekea utaratibu maalum tukajielewa na tukajipangia wenyewe katika ardhi yetu ndogo tuliyonayo nini tunakihitaji, vipi itumike, utalii gani tunautaka ili waweze kupata haki zao Wazanzibari katika taifa lao, ukizingatia serikali yetu imepoteza nguvu yakuwa na ajira kwa vijana wake. Sekta hii tunaitarajia sana ya kwamba ingewezesha kuwapatia ajira vijana wetu kupitia sekta hii ya utalii, katika dhana ile ile ya utalii kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tumefika mahala sasa wenzetu wageni hata ndugu zetu wa damu hao Tanzania Bara wanapewa vitambulisho vya ukaazi na wakapata nafasi ya kuajiriwa katika mahoteli mbali mbali, ushahidi, Wazanzibari wao wakiwa wanatazama macho hawana la kufanya. Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huu katika watu wanaohitaji maendeleo ya kweli kama yale aliyosema Mzee Karume ya uongozi bora, basi hii ni nafasi ya aina yake itumike kuona kwamba Wazanzibari sasa wanapatiwa nafasi hiyo na kuwanasua katika matatizo ya kiuchumi, lakini pia kuondoa wimbi kubwa la ukimwi pamoja na ujambazi na madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, vijana wakikosa kazi ni tatizo na mzigo huo sio wa mtu mwengine ni wa taifa hili. Mhe. Mwenyekiti, pale ambapo nafasi inapatikana basi tuhakikishe kwamba vijana wetu wanapatiwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba umefika wakati wa kukiimarisha Chuo chetu cha Utalii cha Maruhubi kuona kinazalisha vijana wenye uwezo na wenye ushindani wa soko katika mahitaji ya utalii. Mhe. Mwenyekiti, pia Serikali kupitia wizara hii ni bora ipange mpango maalum juu ya vijana ambao wamehitimu ili waweze kuajiriwa wale Wazanzibari halisi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tuna muda mchache kwa hiyo naomba ufupishe ili na wengine pia waweze kuchangia.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, sasa basi kwa vile kuna muda mchache basi niende katika kifungu cha 5 (1) (vi) kinasema hivi:

“Mjumbe mwengine yeyote ambaye atakuwa ni mwanamke”.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nimetazwa kidogo, ni kwamba sekta inayozungumzwa hapa ni utalii, lakini ningeomba sehemu hii huyu mwanamke apewe sifa zake ili zieleweke na isije ikaleta utata baadae ionekane hasa mlengwa wa nafasi hii ni nani.
Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kifungu hicho hicho cha 5 (3) (ii) kinasema:

“Awe na ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo”.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ni bora tuone kwamba imegusana moja kwa moja kuja kwenye utalii, na hicho kifungu chengine kinasema kua awe na mahusiano mazuri na watu. Mhe. Mwenyekiti, ni bora ingekua na utaratibu uliochambua kuonesha kwamba hao wahusiano wenyewe ni akina nani. Mhe. Mwenyekiti, nije katika majukumu ya Makamishna.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Makamishna wamepewa nafasi kubwa katika taifa hili na kuonesha kwamba wao wanapata nafasi ya kuishauri serikali na uongozi wa Kamisheni. Hii ni nafasi nyeti sana na ni muhimu sana kuweza kujua majukumu yao. Hawa ndio wale ambao wataielekeza serikali ni utalii wa aina gani, ni ule wa watalii vishuka ambao wanaingia mitaani mwetu na kutuharibia maadili yetu, au tunahitaji watalii wa daraja la kwanza ambao wataweza kutukuzia uchumi wetu bila ya kuathiri mila na desturi zetu. Mhe. Mwenyekiti, hawa wana nafasi nzito sana katika utekelezaji wa adhma yetu hii, vyenginevyo basi lawama kubwa inaweza ikawaangukia wao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mengi waliyazungumza wenzangu na kwa sababu naamini kwamba michango yao hiyo ilikua na nia kama yangu kwa hiyo niungane na wao kwa yale ambayo, mimi nimeyawacha na wao

waliyatangulia kuyafikisha kwa nia ile ile nzuri ya kuliendeleza taifa letu hili na kuwakwamua wananchi wetu kiuchumi na kuweza kumudu maisha yao ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wenzangu wa Wilaya ya Kaskazini "B" naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia angalau muda mchache wa kuzungumzia mswada huu uliopo mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, sote tunatambua kwamba hivi sasa nchi yetu inategemea zaidi utalii kwa mapato yake, na tunakusudia kuuweka katika vile tulivyosema ni vipaumbele. Lakini kila nikiangalia sheria hii naona kama vile tumeiweka kiasi kwamba kuna watu labda tumewapanga tumewawekea *designation* yao ili baadae tuwapatie ajira. Lakini hasa hauna lengo la kusema kwamba tunataka kukuza uchumi kupitia utalii.

Mhe. Mwenyekiti, utalii kama wanavyosema siku zote Mhe. Waziri ni *double sword* huwa ndio anavyotwambia kwa maana ya kuwa una pande mbili. Kwa hivyo, ncha moja ni hatari na ncha nyengine ndio labda inayosaidia kuleta maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, sisi katika nchi yetu hii tunajuulikana kwamba ni Waislamu na tuna imani hiyo kwamba wengi ni Waislamu, lakini tukikaribisha mambo kama haya sijui kwamba tutakua tunabadilika tutakua ni wale wale Waislamu, lakini tutapata athari tena athari kubwa sana. Kwa hivyo, kama tumeamua kwamba tunataka kuingia katika sekta hii basi tunaamua moja kwa moja, sio hili tunalikubali na lile hatulikubali. Mhe. Mwenyekiti, sisi Waswahili tunasema ukipenda boga basi unatakiwa ulipende na ua lake. Kwa maana hiyo kama tumekubali kuingia katika sekta ya utalii na kuifanya kwamba ni sekta ambayo itazalisha ili tupate ajira, ili tupate mapato basi hayo ni lazima tuyatambue kwamba utalii athari zake ni kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna nchi za Afrika ya Kaskazini ambazo nchi hizi moja kwa moja wao waliukaribisha utalii, nchi kama zile za Morroco, Algeria na Tunisia matokeo yake total wali-*ignore* dini zao na utamaduni wao baada ya kuingia utalii. Matokeo yake nafikiri mnakumbuka miaka ya 1991-1992 ilibidi paanzishwe vyama vya kisiasa vilivyo na *affiliation* ya dini kwa ajili ya kuokoa dini zao na vyama hivi viliitwa *FIS (Front Islamic Salvation)* kwamba walifika wakati wakaona kwamba leo tunakwenda siko, kwa maana hiyo turudi.

Mhe. Mwenyekiti, matokeo yake walipoingia katika uchaguzi watu hawa walishindwa kwa sababu waendeshaji utalii ulimwenguni ni wale *Westerners* na wao hawako tayari kuona kwamba *civilization* yao inaporomoka kwa sababu imani yao ni kwamba *Islam is the great enemy towards their civilization*. Kwa hivyo, watatumia njia zao zote ili utamaduni wao uwe uko juu na wetu uweko nyuma. Kwa maana hiyo basi sasa ni lazima tuamue kama tunataka kuingia katika utalii, basi tuingie utalii sio tena tuanzishe kamati huko vijijini Kamati za Wilaya ambazo tukawaingiza Mashekhe kwa nia labda ya kusema kwamba watu wote katika nchi hii tayari wameshakubali kwamba utalii iwe ndio chombo chetu cha kupatia utamaduni.

Mimi nafikiri bado hatujafikia hatua hiyo, bado watu wana *negative attitude* kuelekea utalii, hivyo hayo ya kuwaingiza labda viongozi wa dini isiwe ndio sababu ya kuona kwamba tutapata salama.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa mapendekezo yangu watu kama hawa wangelikaa wao mbali tukaweka kama wao ni *watch dog* wao wakawa wanakaa mbali wakapata kutukosoa sisi katika hizo sera zetu, lakini tukiwaingiza hapa mimi nafikiri sio jambo la busara kwa sababu bado hatujaamua nini tunataka kufanya katika sera hizo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba hivi sasa nafikiria hata hiyo wizara ambayo inashughulikia shughuli za utalii haijajua hasa nini kile kivutio kikubwa katika nchi yetu cha wale watalii. Kwa maana hiyo bado tunakwenda tu sisi tunasema tunataka watalii, watalii ndio watakuja lakini je wataingiza kipato katika nchi yetu, je, *organization* zetu tulizozifanya ziko vizuri ili kuhakikisha kwamba kipato kinaingia japokua wananchi wanalalamika. Kwa nini nasema hivi? Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba inatulazimu tuamue au tujue nini hasa kinachowavutia hawa wenzetu kuja katika nchi yetu. Je, wanakuja kuangalia *stone town*, ikiwa wao wanakuja kuangalia *stone town* hebu tuangalieni wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, watembezaji watalii mara nyingi huwa naona wanaingia pale sokoni, lakini leo ukienda sokoni sijui utapata harufu zaidi ya kumi pale. Kweli huyo akirudi kwao kesho atakua na nia tena ya kusema mimi nakuja tena Zanzibar.

Je, kivutio kikubwa kwa watalii ni nini? Ni *long beaches*, mimi nasema bado hatujaamua kwa sababu hivi sasa kuna malalamiko makubwa kwamba hizo *beach* zetu tumeweka sheria inayosema zijengwe kwa utaratibu fulani, lakini

bado hatufuati utaratibu huo na badala yake tunajenga tunavyotaka wenyewe. Kwa hivyo, hata hizo *beach* zinaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, ukenda kwenye barabara ili magari ya watalii yapite ukipita Maruhubi kwanza uondoe ng'ombe ndio watalii wapate kupita na magari yao. Kwa hivyo, ningewaomba mimi hawa wizara watakaoshughulikia basi wajue nini tunachotaka kukifanya hasa ili tukapata kukitunza zaidi ikawa ndio kivutio cha utalii. Tunajua kwamba kuja kwa Tanzania wengi wanavutika kwa sababu ya mlima Kilimanjaro. Lakini je, kuja Zanzibar ni kipi kivutio chao hasa ili tukapata kukitunza zaidi, kinyume chake tutakua tunasema tu kesho hamna kitu.

Mhe. Mwenyekiti, hii ina maana kwamba sekta hii ya utalii ni sekta inayoingiza mapato, lakini ni kitu ambacho wakati wowote kinaweza kikaporomoka kwa sababu mbali mbali na sababu nyengine ni kama hizo tunazozitaja. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Kenya wakati wa *Bombing* za Mombasa walikaa sijui miaka mingapi nafikiri mpaka hivi leo wamekumbwa na *Alshabab* bado utalii unalega lega na wao vile vile ni sekta yao kuu ya kuingizia mapato. Nafikiri na sisi tungefikia wakati tukajua nini tunafanya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nikisoma mswada huu unakutia kuna kipengele kinachosema kwamba kutakua na mkutano wa wadau, sasa je wadau hawa wamekusudia ni wadau gani? Kwa sababu sekta ya utalii inahusisha watu wote.

Mimi ningependa kuja kuona mkutano wa wadau hapana yule muuza vinyago na mtembeza watalii *no*, kama tunasema ni wadau tule gharama, je, wizara imeshakubaliana na hayo kwamba hivi sasa tunakubali kula gharama.Kwa sababu kuna mashirika ya Ndege pia na wao ni wadau, kuna mabalozi ambao wanawajibika kutoa *visa* pia ni wadau.Sasa je, tumeshajipanga kwa hayo yote? Ni kwamba tukisema sasa tunaita mkutano wa wadau kama tunavyofanya mkutano wa *sullivan* tukaja hapa tukafanya jambo tunalolijua, sio mkutano wa wadau ukaenda kumkuta sheha wa nyumba kumi na wengineo.

Mhe.Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo kwamba sisi tuna *design* sheria, kiasi kwamba tumuweke mtu katika madaraka au tumpatie ajira, hatuna ile nia ya kwamba tuna-*design* ili ku-*promote*, kujenga uchumi wetu uwe mkubwa zaidi.

Leo ukisoma kipengele cha Ukurugenzi au Mwenyekiti, utakutia kwamba mwenyekiti huyo anatakiwa apewe ajira, lakini hana sifa yoyote ambayo imewekwa kwa ajili ya kuwa akubalike kuwa yeye ni Mkurugenzi.Sijui masuala kama haya tutaendelea nayo mpaka lini, kwa sababu hivi sasa imekuwa kama ni mtiririko, huyu Mkurugenzi awe hivi awe hivi, kama tunakusudia kujenga kweli basi tutafute mtu ambaye anaeleweka.Huyo huyo Mkurugenzi kwa hivi sasa hiki chombo ni kikubwa sana, lakini tunakifanya kama ni kitu kidogo tu kinacholegalega, kama kweli tunataka kuleta maendeleo basi mtu huyu awe angalau ana shahada ya pili.

Hivi sasa watu waliokuwa na shahada ya kwanza kina sisi tupo tele, sisi tunazo miaka 20 iliyopita nyuma sasa watafutwe angalau na hao waliochuchuka zaidi, kwa sababu hiki chombo ni kikubwa.

Mhe.Mwenyekiti, mimi pia ningesema kwamba, hivi sasa hata Kiswahili kinaanza kutupiga chenga.Ukiangalia vifungu vingi vya sheria sijui maana ya sheria, ningeshauri kwamba mara nyengine mkaweka wakalimani katika kuitafsiri miswada yetu kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.Utakuta neno 'awe mstari wa mbele katika kupigania mambo', mstari wa mbele hayo mambo gani, au awe mstari wa mbele vipi?

Mimi nafikiri Mhe.Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba nikae.

Mhe.Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninakushukuru kunipa nafasi hii. Kwanza mimi ni Mjumbe wa Kamati wenzangu wamezungumza juu ya muundo wa Kamisheni.Kamisheni hii sio mpya ni kongwe, nitazungumza baadae historia yake.

Lakini kuhusu Mwenyekiti, mwenyekiti huyu hatakiwi kuwa Mwenyekiti Mtendaji wala hatakiwi kuwa halafu ana madaraka hapana, huyu ni Mwenyekiti wa Kamisheni na huu sio mwanzo.
Kamisheni mwaka 1996 ilipoanzishwa Sheria ya Kamisheni ndugu Abdalla Mwinyi alikuwa Mwenyekiti, na ndugu Walid Fikirini alikuwa Mkurugenzi.Mwaka 2000 Mhe. Mohammed Aboud alikuwa waziri, ndugu Issa Ahmed

alikuwa Mwenyekiti na ndugu Vuai Mwinyi alikuwa Mkurugenzi pale, na ni vitu vya kawaida hivyo.Sasa hii mwenyekiti kumpa madaraka na kumpangia apate mafao huu ni mpango ambao sio sahihi.

Kwa sababu Kamisheni hii sio jambo la mwanzo, tunazo kamisheni tena juzi tumepitisha, tuna Utumishi Bora, tuna Mohamed Faki ni Menyekiti Kamisheni ya Utumishi, yeye sio *full time job* anakwenda kwenye vikao tu, tena chombo kikubwa sana chombo cha utumishi. Tunae Mwenyekiti Othman Bakari Tume ya Utumishi ni mwenyekiti, lakini kuna utendaji, kuna ndugu Mtoro ambaye ni Kamishna wa Utumishi, kuna ndugu Moh'd Khamis. Kwa hivyo hata Baraza la Wawakilishi ambalo ni chombo kikubwa sana, kina mwenyekiti wake ndugu Sultan Moh'd Mugheir, yeye sie wa kudumu anafanya vikao vyake tu.

Sasa suala hili waziri akubaliane kuwa jambo hili si sahihi, na hasa kumuwekea maslahi ya utumishi, mtumishi gani anafanya kazi miaka minne apate hayo mafao? Hii haiwezekani afute kabisa abakie Mwenyekiti wa Kamisheni kama wenyeviti wengine.

Mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Shirika la Meli, pale unapata posho lako, waziri tunampelekea maombi yetu tunataka tupate *fee* ya Ukurugenzi au tupate fedha za kuondokea (*cabinet benefit*), waziri akiikubali basi tunapata posho kwenye vikao, tunapata *fee* ya u-*director*, waziri mmoja anasema mpate mamlaka yake ya waziri, na tukiondoka tunapata chochote basi hakuna zaidi.Kwa sababu huu ndio utaratibu ulivyo.

Kwa hivyo, hili kwanza naunga mkono na wote waliosema hii Mhe.Waziri akubali hili jambo abakie kuwa Mwenyekiti wa kawaida. Hilo la mwenyekiti.

Lakini katika wajumbe wa kamisheni, kamisheni ile ina wajumbe wake. Kwa sababu hii ni kamisheni wanaitwa *commissioners,*wewe mwenyewe Mwenyekiti ni Kamishna umechukua nafasi yangu kule *TCU*, mimi nikiitwa sasa hivi ni wewe *commissioner*, lakini mwenyekiti wako yeye sio wa kudumu. Kwa hivyo, hawa makamishna ndio kama *Board Members*, lakini katika kamisheni wanaitwa makamishna. Hivyo, makamishna hawa mwenyekiti abakie kuwa ni mwenyekiti wa kikao cha kamishna hana kazi nyengine, akimaliza aende kwake.

Wajumbe wengine ambao wanatakiwa wawemo hapa kuna *hospitality industry*. Nakubaliana na ndugu Ismail Jussa Ladhu kasema hapa wawekwe *ZATI, (Zanzibar Association for Tourism Investors)* hiki ni chombo kikuu sana, kwa sababu hii ni *bulletin* ya serikali, inasema *according to survey carrying out by Zanzibar Commission of Tourism and ZATI 2011*. Kwa hivyo, *ZATI* ndio chombo kikuu cha kusimamia mambo ya hoteli. Kwa hivyo, *ZATI* iwe mjumbe rasmi kwenye ile *hospitality* kwa sababu wao hoteli zote hizi kubwa Kempinski, Lagema, Karafuu wote hao ni *members* nao ni investors wakubwa. Kwa hivyo, *ZATI* iwe *member*.

Lakini ndugu Ismail Jussa nakubaliana naye mimi aliposema, sisi nchi yetu hii ni Waislamu na utalii umeanzishwa na Uislamu, mbele huko nitaeleza *Islamic Tourism*. Lakini watu wetu wanataka kuelimishwa, kwa hivyo sio vibaya katika ile kamisheni itapokuwa katika ile Kamisheni ya Wilaya kuna mashekhe wa dini nitaeleza mbele huko. Lakini kwenye tume hii ndugu Jussa ali-*suggest* aingie mtu wa dini na kuna uzuri wake, tuache kuweka kwenye hizi kamisheni watu wa serikali tu, mtu wa *planning* hapana, hivi vyombo ni *private* hasa ukitaka kukua.

Sasa mimi naona hii inayoitwa *Association Traveling Tour Operators* kuna *interest* fulani hapa.Lakini mimi nafikiri madhali kuna chombo kama *ZATI*, huwezi kufanya *duplication* tena ya hawa *Travel Tour Operators*. Sasa hapa kwa sababu sasa hivi kuna *tourism police* hivi juzi Mhe.Rais amesema iko haja sasa vizuri kiongozi mkuu kutoka Jeshi la Polisi wakawemo humu sio kule, kwa sababu watalii wanataka usalama wao na vyombo vya usalama vimo. Kwa wale wanaokwenda kwenye mbuga kuna *wide life police*, sasa hivi tuanzishe *tourism police* kusaidia uhalifu unapotokezea.

Kwa hivyo, ipo haja kuweka mtu kama huyo badala ya kumuondoa yule, na ninakubaliana na ndugu Jussa kuwa mwanamke atafutwe awekwe, katika uteuzi wake waziri azingatie *gender* nakubaliana naye moja kwa moja. Kwa sababu wanawake ni muhimu wawemo.

Lakini watu wengi wamezungumza na mimi nasema hii tume ya mkono, halafu kwenye hii kamisheni kwenye wilaya, kwenye wilaya kuna wajumbe wa wilaya naomba Mhe.Mwenyekiti niisome kwa sababu hawa ni wapya na kwa nini wakawekwa?Kwa hivyo, mimi naunga mkono kwa sababu sote tulikuwa tunajiuliza kwa nini mmeunda kikosi hiki cha wilaya, kamati ya wilaya? Kwa sababu sasa hivi tunataka kulinda mila, desturi za Kizanzibari kutoka

huko, hawa vichangudoa, hawa wenye nini sijui, lazima wilaya isimamie na ujumbe wake anaongoza Ofisa Mkuu wa Polisi.

Nakubaliana na hilo mwenyekiti wa masheha wa wilaya, nakubaliana na hilo kwa sababu masheha ndio wanaojua watu pale, mtu mmoja kutoka Makumbusho kwa sababu utalii wetu una mambo ya makumbusho, majumba ya kale, mfanyabiashara wa wilaya, mkulima na wengine wote waliosemwa, mtu mmoja kutoka Wizara ya Ardhi, mmoja kutoka Wizara ya Mazingira, yale yaliyosemwa asubuhi mtu wa mazingira yumo kwenye wilaya *very important*, mtu mmoja Jumuia ya Kiraia ndani ya wilaya, Viongozi wa Dini katika wilaya, mtu mmoja kutoka Mamlaka, sasa sisi tuliongeza katika kamati tukasema na mtu mmoja kutoka kwenye Kamati za Mambo ya Mila na Utamaduni awemo humu.

Kwa sababu tatizo lote hayupo hapa Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi, juzi tulimsikia alivyoeleza hali, na ametualika saa mbili ya usiku twende kule tukaone mambo.Sasa haya yote si kazi ya Sekta ya Utalii, ni kazi ya Wilaya na Mkoa, sasa kamati hii kazi yake moja ni kusimamia mila, utamaduni, unasimamiwa pale. Kwa hivyo, mimi naunga mkono sana kamati hii na aongezwe mtu huyo, na kamati hii na sisi wawakilishi tuwasaidie hizi kamati katika majimbo yetu.Hili jengine ambalo limo ndani ya sheria hii, haya mambo mawili, kwa sababu natilia mkazo kuongezwa wale watu wengine, mwenyekiti awe wa kawaida.

Sasa tuje katika suala la historia ya utalii.Hapa mimi ninayo sheria Mhe.Mwenyekiti, jambo la utalii si jipya.Nina *Presidential Decree No. 13 of 1967*, *decree* hii imetengenezwa kwa mujibu wa *power* za *logical* za mwaka 54, "*Exercise of the powers conferred by the Legislative Powers Law, 1954, the President of Zanzibar by and with the advice and consent of the Revolutionary Council…"*

Kwa hivyo, Baraza la Mapinduzi ana- *make this decree."This decree may be cited as the Hotel Accommodation (Imposition of Levy)* hapa ndio *vision* mwaka 1967 ya Mzee Abeid Amani Karume. Baraza la Mapinduzi lile liliona ipo haja likachukua *hotel levy*, Hoteli ya *Africa House* ikiitwa *English Club*, ilikuwa ni hoteli ya wazungu *English*, sio kila mzungu, si Mjerumani, Mfaransa, *English* kama mimi hivi. *Starehe Club* ilikuwa wazungu wale Wajerumani, Wataliana pale karibu na Mambo Msiige.*Zanzibar Hotel* ya Wazungu vile vile, *The Golf Club* pale Maisara. Zile zote zingechukuliwa zikawekwa kwenye sheria hii na Mzee Karume akajenga hoteli tatu Pemba; Chake Chake, Wete na Mkoani na akawa na azma akajenga nyengine Bwawani na akaanzisha kitu kinaitwa *Tourist Board*.

Lakini Mzee Karume sheria hii inasema serikali itaanzisha: *"Tourist Bureau"* maana yake ni *Tanzania Tourist Friendship Bureau established under the Public Enterprise Decree, 1966.* Hii kazi yake ni nini? Tulianza yule mzee ile vision chombo hiki kuanza kuzungumza na nchi marafiki kuanza kuiuza Zanzibar kiutalii, ndio maana hii. Na ile *TFB* aliongoza Pili Khamis *Boys House*, pale *Ben-Bella School.* Kwa hivyo imekwenda wee mpaka mwaka 1991 Dr. Salmin Amour alibeba nishani kubwa ya kukuza utalii, amebeba nishani kubwa katika historia ya nchi hii. Kwa sababu alipoingia madarakani mwaka 1990 akaanzisha sheria ya utalii, sheria ambayo inasema:

"*An Act to repeal....*" inafutwa ile sheria ya mwaka 1967, sheria gani? "*To promote and strength* (ana *promote* na ku *strength*) kwa hivyo akaanza sasa ku-*promote* na ku-*strength*.Ilikwenda mpaka mwaka 1996 ndio akaanzisha Kamisheni ya Utalii, alianzisha Dr. Salmin Amour sheria nyengine hii hapa ya mwaka 1996, ndio tumekwenda nayo mpaka sasa hivi tunaifanyia mabadiliko.

Sasa katika miaka kumi ya Dr. Salmin ali-*promote* aka-*strength* hali ikenda, miaka kumi ya Karume ndio hizi hoteli zimeanza kukua ni kubwa kubwa hizi, Kempisk, Karafuu na kadhalika, leo asilimia 80 ya pato la serikali linatoka ndani ya utalii, sasa unasema utalii hautusaidii, mapato ya serikali asilimia 80 hii hapa *bulletin* ya serikali. *Zanzibar Economic Bulletin* sio Ali Mzee Ali anasema, hii hapa. Lakini hii asilimia 80 inayotoka inataka kuchungwa, vivutio vya utalii vipo vitano.

Mhe.Mwenyekiti, kuna *Stone Town* ndio inayoongoza, lakini leo hebu pita *street about the street* utaona vitu vya Kimasai. Sasa hayo ni mambo ya Kamisheni kuhakikisha inakuwa *maintain*, lakini je, Mji Mkongwe ukiondoa majumba, harufu ya Karafuu Zanzibar utaipata, ukienda sokoni uchafu ule? Sasa hayo ni mambo ya serikali kuhakikisha Mji Mkongwe unakuwa safi mtu akiingia pale afurahi, ile historia ya Mji Mkongwe watalii iwavutie kwa sababu ile ni *heritage* katika mambo ya duniani moja ile.

Kivutio kingine ni historia.Tuna magofu Pemba kule kuna vitu vimevumbuliwa mji uliozama miaka 3000 nyuma, *Mazrui Estate* iko kule magofu mengi.Iko haja Kamisheni hii ifanye ziara wawakilishi wakaone hayo magofu wakaone historia, iko haja.

Halafu Zanzibar tuna *beach* safi sana, mchanga wake mzuri uko safi, lakini je usalama upo? Sasa ndio nikasema *Tourist Police,* serikali ina jukumu la kutengeneza miundombinu, umeme uwe wa uhakika, maji ya uhakika, barabara za uhakika, ili tuweze kuupeleka utalii katika *hundred percentage* katika *growth* ya serikali yetu, hilo jambo muhimu sana.Lakini basi, leo watu wengi sana wamezungumza mambo ya kuwa watu wananyanyaswa, *employment* na ndio maana sasa hapa pana vyombo.

Kuna Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ndio inayotoa *working permit,* serikali yenyewe ndio inayotoa *working permit,* unaanza utalii pale ndio wanatoa *certificate,* huyu anafaa kupewa mtu wake wamuajiri, anapeleka kule ukifika kule kuna *Immigration* unapewa sasa *resident permit*.Sasa hivi vitu viko kwenye mikono yetu, Mhe. Makame Mshimba yupo au hayupo? Hivi ni sisi wenyewe tusimamie, tusimamie wenyewe Wizara ya Uwezeshaji, Wizara ya Utalii *Immigration* wasimamie kuhakikisha kuwa watu ambao kazi zao zinafanywa na Wazanzibari wapewe Wazanzibari, nchi inajengwa na Wazanzibari wapewe Wazanzibari, tusiwalaumu wale. Kwa sababu wale wenye hoteli wanaomba *permit* serikalini na serikali inatoa *permit* hizo, sasa ikiwa inatoa kwa mlango wa nyuma, mlango wa mbele tunasema sisi Baraza tunakemea watazame watu wanaostahiki wapewe. (*Makofi*)

Mambo ya Ufukweni. Leo nchi kama Singapore, Dubai wanaijaza bahari yao ili nchi itanuke, sasa hivi kuna hoteli ziko chini ya bahari, sio ufukweni, chini ya bahari. Lakini ukikaa tu hapa Mhe.Mwenyekiti, wamesema China ni mfano mzuri, China ni mfano mzuri kweli kwa sababu China sio nchi ya leo, miaka 1340 Mtume Muhammad (*SAW*) kasema, nenda mpaka China, sasa China sio nchi ya jana ni nchi ya muda mrefu sana, lakini nenda Rwanda hapo utizame usafi. Zanzibar ilikuwa na sifa ya usafi, usafi wa sura za watu, usafi wa nchi, leo imeharibika na sisi tunaharibu, marikiti aibu.Sasa yako mambo yamo ndani ya mikono yetu.

Mhe.Mwenyekiti, sasa tuje suala la dini.Rafiki yangu kazungumza hapa tuchague, kwanza niseme Sekta ya Utalii ndio sekta kiongozi hii sheria inasema hivi: "*Tourism the Engine for Zanzibar Economic Growth,* ni *engine* ya Zanzibar economic growth, utalii ni asilimia 80 ndio *engine,* mishahara yetu, posho zote ziko huko lakini sasa suala la dini.

Dini mimi nina waraka hapa ambao ulizungumza juu ya dini.Watu wengi tunachanganya hapa, dini Uislamu kwanza nifasiri Mhe.Mwenyekiti, kabla sijenda huko kitu gani utalii. Kwanza sheria imefasiri utalii, lakini dini imesema hivi, "Utalii ni kutembea kwa kufuata matakwa ya sheria, mfano kama vile kuzuru Misikiti Mikuu mitatu", kwa wale waliokwenda Umra, ule ndio utalii, utalii ni kuona nini, kuona misikiti mitatu? Kutafuta elimu na rizki ya halali na matibabu au jihadi ya kulingania dini au kutafakari, kuzingatia juu ya maumbile aliyoyaumba Mwenyezi Mungu.Huo ndio utalii Kiisilamu.

Ibni Batuta amesafiri dunia nzima kutalii, lakini tazama ndani ya Qurani mara ngapi umetajwa utalii, utalii neno la Kiarabu, Suratul Yussuf aya ya 109. "Je, hawakutembea katika ardhi wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale wabaya waliokuwa kabla yao"? sura ya 12:109. Suratul-Al-Hajj aya ya 46 "Je, hawatembei katika ardhi ili wapate nyoyo (akili) za kufahamu, masikio ya kusikia"? Ingekuwa Mheshimiwa hujenda China, leo ungetoa mfano wa China" lakini umekwenda, umetembea umeona na siku hizi kila mtu China China, Inshaallah, kwa sababu wametekeleza Mwenyezi Mungu vile alivyoagiza.

Suratul-Muhammad, "Hawakutembea katika ardhi wakaona imekuwaje mwisho wa wale waliotangulia"? Suratul-Ruum aya ya 9, "Je, hawatembei katika nchi na kuona jinsi ilivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao"? Suratul- Fatir aya ya 44, "Je, hawakusafiri katika ardhi wakaona jinsi ilivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao"? Sulatu-Al-Imran, "Basi safirini katika nchi na mwone ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha".Sasa hizi zote ni usahihi kuwa Uislamu umezungumza juu ya utalii, sasa wale mashekhe vilemba waliosema aa shauri yao.Lakini umezungumza.

Mhe.Mwenyekiti, sasa lakini kuna mambo ambayo yanakatazwa.Unapochukua mashekhe ukawatia ndani ya kamati ile, watakuwa kazi yao kuelimisha jamii, sasa hayo mambo ya kwenda utupu, sijui mambo ya nini.

Nakumbuka utalii ulipoanza, kweli mimi rafiki yangu sana Dr. Salmin Amour Juma, alikuwa ananiita Sheikh, akanambia Sheikh Ali ee wamekuja watu hapa shamba wakanambia Mzee unayo habari mambo yaliyoko Nungwi?Akauliza kuna nini? Akaambiwa aa Mzee hatari watu wako uchi.Akawauliza nyinyi mmewaonaje?Wakasema sisi kule huwa tunapitapita kwa sababu ni njia, akawambia basi mkipita msiwatazame, wakamwambia macho hayana pazia tunawatizama bwana, wanawatizama.Lakini haya mambo yapo tu huko, lakini hakuna dini wala serikali, na wale watu aliosema Mheshimiwa wa *Kibanda Ugali* wale ni Machangudoa. Sasa hii kamati ndio kazi yake kusimamia machangudoa na mengine yote. Leo nchi yetu hii baa, ulevi vimejazana kila pahala, ndani ya majumba.Sasa hizi kamati ndio kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una muda wa dakika tano malizia.

Mhe. Ali Mzee Ali: Sawa, kwa hivyo, haya mambo yanataka serikali iyasimamie na sisi viongozi tusimamie.Niliona nieleze haya kwa sababu sisi ni viongozi na mimi naunga mkono mswada huu na tuwasaidie sana, Kamisheni ya Utalii ifanye kazi iache majungu, na chombo hiki ni chombo *independent* kisiingiliwe, kisimamiwe na waziri, wizara, lakini ni chombo *independent*.Kwa sababu tuna mazoea kwenye vyombo, wizara hii inaviingilia sana.Kwa hivyo mambo kama haya watu wajue kuwa huu ni wakati mwengine na naona nimejaribu kueleza yote haya, kwa ufupi mimi naunga mkono hoja hii moja kwa moja.

La mwisho kabisa naomba Kamisheni ya Utalii chini ya waziri wetu mpya Mhe.Said Ali Mbarouk mwenzako ameondoka, mwenzako mpya wewe mzoefu, tumekuwa pamoja *backbencher,* ulikuwa msemaji mkubwa na tunaamini mtasaidiana usukume mbele gurudumu hili kwa kuandaa semina. Waambie hao wenye hoteli kubwa wafanye semina kwa wawakilishi kuwaelimisha juu ya hii sekta ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, nimemuona Mhe. Said Ali Mbarouk amenijibu amekubali namshukuru sana, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kusema machache katika waraka huu wa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii Nam. 6 ya mwaka 2009.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Mzee Ali katoa mengi sana hapa kama historia, mambo ya kidini na kadhalika. Kwa kweli naamini kwamba hii ndio semina ambayo wawakilishi wetu wakiitaka wapate zaidi na kwa undani zaidi. Tangu jana nimeangalia wawakilishi wametoa mawazo mengi sana ambayo mimi nayaheshimu sana na sina pingamizi nayo. Isipokuwa tu nataka kueleza haya yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, asili ya visiwa vya Zanzibar yaani Unguja na Pemba vinatokana na mambo mawili, vinatokana na biashara, vinatokana na utalii, ndio maana ukaona sote tuliopo hapa tuko rangi mbali mbali na *origination* mbali mbali kwa sababu ni visiwa na kwa kweli vimekua kwa misingi ya kibiashara na misingi ya kiutalii.

Kama alivyoelezea Mhe. Ali Mzee Ali kabla ya Mapinduzi kulikuwa na hoteli moja lakini baadae tukawa na hoteli za Chake Chake, Mkoani, Wete na Bwawani, ikaja mpaka hoteli ya Amani. Lakini nakumbuka vyema katika miaka ya 85 kwamba tulianza kutafuta wawekezaji kutoka kila kona ya dunia tukataka waje wawekeze katika sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya utalii. Wakati ule vile viwanja vya pwani pwani kule ilikuwa hata ukipewa bure huvitaki vilikuwa jiwe tupu hakuna kitu, lakini baada ya kuja wawekezaji nchini wakaitikia wito na wakaweza kuwekeza katika masuala ya utalii.

Sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, tumeweza kuwekeza hoteli nyingi tu za kitalii, tumekuwa na *diving game,* tumekuwa *tour operators* wengi, tumekuwa na *fishing investment,* utakuta tuna miradi 15 kwenye *fishing investment* na tuna miradi mingi tu ya mahoteli. Tuna vitanda 12,000 mpaka sasa hivi na tuna hoteli takriban 293, tuna vyumba 5,550 na mwaka jana tumepata watalii wanaofikia 213,,000 ukiingiza ile asilimia 15 ya watalii kutoka Tanzania Bara.

Yote haya yamefikiwa kwa jitihada ya mwaka hadi mwaka. Jitihada ya kwanza kutafuta wawekezaji kuja kuwekeza na jitihada ya pili kuitangaza Zanzibar kuwa ni pahala pa kuja watalii na kuja kufanya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili halikuwa rahisi serikali imefanya kazi kubwa ya kuitangaza Zanzibar na imetumia gharama nyingi sana. Malengo ya serikali ni kuona kwamba Zanzibar kama ni kisiwa hatuna madini, Zanzibar kama visiwa vyote duniani uchumi wetu ni uchumi wa huduma yaani *service oriented economy,* tutoe huduma tupate

kujenga uchumi wetu. Moja katika huduma muhimu ni huduma ya utalii ambayo inakua na duniani ni maarufu sana. Katika azma hizo ni kwamba nchi yetu ipate tija, vile vile wananchi wetu wapate ajira.

Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumza ajira kuna ajira aina mbili, ajira ya kwanza ni *direct employment* na ajira ya pili ni *indirect employment. Direct employment* maisha huwa na wachache lakini *indirect* inakuwa na wengi. Kwa mfano, Kiwanda cha Soda inawezekana kinakuwa na wafanyakazi 30 hao ndio *direct employment*, lakini wale wauza soda mmoja mmoja ndio *indirect employment*. Ukiangalia soda pengine milioni 11 kwa mwaka kila soda moja ikapatikana shilingi 100/- ni ajira ya watu wengi.

Katika hii ajira ya moja kwa moja ni ile ajira ambayo inatakiwa vijana wetu waajiriwe katika mahoteli sehemu za upishi, *house keeping* na mambo mengine. Kwa bahati mbaya sana mimi ninayo kidogo a, b, c, d ya hoteli, namuunga mkono sana Mhe. Hamza Hassan Juma pale aliposema kwamba ipo haja ya kukikuza Chuo chetu cha Utalii, kikuzwe sio kwa *certificate* tu lakini kwa kutoa diploma hata *degree* kwa sababu tuna nia ya kuwekeza katika masuala ya utalii.

Utakuta vijana wetu wengi wa Kizanzibari kwa mfano utatangaza kazi wewe ukasema unatafuta meneja wa hoteli utakaa mwezi mzima unatangaza lakini maombi yote yatakapokuja ya umeneja hoteli basi hamna mtu mwenye sifa za kuwa meneja wa hoteli. Ina maana vijana wetu bado hawajasomea masuala haya, katika upishi hivyo hivyo, katika *house keeping* hivyo hivyo. Mishahara mikubwa ya wafanyakazi kwenye mahoteli ni mameneja, *house keepers* na wapishi, hawa wengine mishahara yao ni midogo.

Kwa hivyo, mimi nasema kwamba ipo haja ya Chuo chetu cha Utalii kupanuliwa namuunga mkono Mhe. Hamza Hassan Juma moja kwa moja na nahimiza vijana wetu wasome katika sekta hii ya *hotel management*, *house keeping* na sehemu ya mapishi.

Lakini katika sekta hii ya utalii ambayo inatoa ajira katika masuala mengineyo yanashajihisha na biashara. Katika nchi yetu biashara imeshamiri, wakulima wanapata vile vile nafasi ya kuuza bidhaa zao mboga mboga, matunda na vyakula, wafugaji kuku wanapata masoko ya kuku na mayai, wafugaji ng'ombe, mbuzi, vile vile wavuvi. Hivi sasa samaki Zanzibar bei yake ni kubwa kutokana na mahoteli yanavyonunua samaki. Kwa hivyo, wavuvi nao wananufaika, wasanii wananufaika, biashara za kitalii yaani *handicraft* ndio zawadi wanayonunua watalii, eenye mahoteli, wenye mikahawa, wenye makampuni ya uzamiaji na vitu vyengine. Kwa hivyo, hii ni sekta ambayo inaweza ikaimarisha sana nchi yetu ikiwa tutaiangalia.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nilipata nafasi ya kwenda Malaysia ambayo ni nchi mojawapo kuna waislam wengi sana na utalii ni mkubwa sana. Utalii kule Malaysia unaendeshwa lakini misingi ya kidini ya kiislam iko pale pale na waislam wanazidi kufanya ibada zao. Huko Malaysia nimekwenda kutembelea katika kisiwa kimoja kinaitwa Lankawi, Lankawi ni kisiwa kidogo sana, urefu wa kisiwa hicho ni kutoka hapa mpaka Mahonda tu, kina wakaazi wasiozidi 80,000. Lakini Lankawi inaingiza watalii milioni 2.4 kwa mwaka, inaingiza fedha nyingi za kigeni zaidi ya milioni 500 kwa mwaka. Kwa hivyo, Lankawi ni kisiwa kidogo wakaazi wote ni waislam lakini kisiwa kinatengeneza pesa kama biskuti.

Nasema mifano hai ipo katika nchi za Malaysia na nchi nyengine za kiislam ambazo utalii unaendeshwa lakini mila, desturi na dini haziingiliwi na utalii ule. Kwa hivyo, ipo haja ya kuelimishana na kuona kwamba tunafanya nini ili kuweza na sisi kuiga mfano kama huo.

Mhe. Mwenyekiti, watalii wanapokuja Zanzibar wakifika hapa wanataka kuja kujionea wenyewe mila zetu Wazanzibari. Watalii hawaji hapa kwa mambo ya mchezo mchezo, wanapoteza pesa nyingi wanakuja hapa wanataka waone mila zetu, vivutio vya nchi yetu na wako wengine wanataka kujua hasa ile historia yetu. Zanzibar vivutio ni vingi kama alivyotaja Mhe. Ali Mzee Ali kuna vivutio vya mila zetu, historia yetu, fukwe zetu na mengi mengineyo.

Sasa mtalii anapokuja hapa akamuona Mzanzibari hakuvaa nguo hafurahi kwa sababu anajua kama hii sio mila ya Mzanzibari, mtalii anapokuja hapa akimuona Mzanzibari kavaa buibui anasema hii ndio mila ya Mzanzibari. Mtalii anapokuja hapa akawaona watoto wetu wako katika mila na desturi zao wamevaa kanzu zao na kofia wanaingia msikitini wakitoka mtalii anajua hii ndio mila ya Kizanzibari. Sasa ikiwa leo sisi walezi wa watoto wetu saa nne

usiku mtoto mdogo wa miaka 10 unamuachia anazubaa zubaa katika Mji Mkongwe pale halafu unasema unalaumu watalii itakuwa mambo ya kuchekesha.

Malezi tunayowalea vijana wetu si mazuri kwa hivyo ipo haja ya sisi Wazanzibari kurejesha malezi ya kizamani kwa watoto wetu, kurejesha mila zetu ili watalii na wao waone kama sisi tuna mila na hizo ndio mila zetu na moja katika kivutio cha watalii kuwa waje kuona mila zetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi serikali imo katika mkakati wa kuimarisha utalii na tuna *theme* ya Utalii kwa Wote. Utalii kwa wote tunakusudia kujenga utalii wenye misingi bora ya kujenga mila zetu na bila ya kuathiri maadili ya Wazanzibari. Serikali imejikita katika kuona kwamba tunapata *quality tourism* yaani utalii wenye viwango unaozingatia maadili, silka ya Mzanzibari.
Ndio maana tukasema kwamba Utalii kwa Wote sio utalii kwa baadhi ya watu. Tukiweka *concentrate* tukasema kwamba tunaukubali utalii ambao utalinda misingi ya kimila na desturi za Kizanzibari tunaweza. Kwa nini wenzetu waweze sisi tusiweze, kwa nini tujipangie *impossible*, kwa nini hawasemi kama ni *possible*. Naamini kama tukiweka nia kwamba inawezekana kuweza kuutaka utalii nchini utakaoweza kulinda mila zetu, kurudisha mila zetu na kurudisha heshima zetu inawezekana. Kwa hivyo, naamini kwamba hilo suala linawezekana na naamini kwamba tukishirikiana kwa pamoja tutafika katika malengo hayo ya kuwa na Utalii kwa Wote *(Tourism for All).*

Mhe. Mwenyekiti, nisipoteze muda wako mrefu na ndio maana sasa hivi wizara imeleta mbele yenu ndugu zangu wawakilishi waraka huu kwa ajili ya marekebisho ili tuweze kufikia malengo ya kuwa na utalii ambao utaheshimu silka zetu, dini yetu na kadhalika. Kwa hivyo, michango yetu *positively* ndio itakayoweza kuijenga Zanzibar, Zanzibar inategemea sana huduma, moja ya huduma ni utalii na kwa sasa hivi uchumi wetu umejengeka katika misingi ya utalii. Hatuwezi kubomoa utalii tutakuwa tunabomoa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mauritius licha ya kuwa imeshasonga mbele katika sekta nyengine lakini bado sekta ya utalii inaimarishwa na wenzetu wanatengeneza fedha za kutosha kutokana na utalii. Vivutio zaidi vinahitajika kwenye nchi yetu, huduma zaidi inataka iimarishwe katika nchi yetu, kwa hivyo mashirikiano baina ya Wazanzibari wote katika kujenga utalii kwa wote ni suala la msingi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe tamko kwamba sote kwa pamoja tuchangie *positively* waraka huu, tumshauri Waziri *positively* juu ya waraka huu na tujue kwamba bado utalii una hadhi kubwa Zanzibar na Zanzibar itaweza kufikia kiwango kikubwa sana cha uwezekezaji katika utalii. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia yale yote ambayo hofu tuliyonayo katika nyoyo zetu yataondoka pindi tutakaposhirikiana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa heshima na taadhima kuunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kupata wasaa kidogo wa kuchangia mswada wetu huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii Nam. 6 ya mwaka 2009.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia na mambo mazuri ya kurekebisha mswada wetu huu na hasa wachangiaji wanne wa mwisho waliomalizia.
Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umekuja kama ni marekebisho baada ya utendaji wa sheria ile ya Nam. 6 ya mwaka 2009 kumeonekana kwamba kuna mapungufu mengi na hiyo ndio kawaida unapotenda ndio unapoona wapi kuna matatizo, wapi ufanye vizuri zaidi, wapi uondoe, wapi urekebishe. Kwa hivyo, si ajabu vifungu vyetu vingi kwenye *marginal note* vimeandikwa kufutwa, kurekebisha, kuingizwa, hii yote ni kurekebisha ule mswada wa nyuma. Kwa hivyo, michango ya Waheshimiwa Wajumbe naamini Mhe. Waziri ameipata na pale panapopaswa atarekebisha.

Lakini mimi Mhe. Mwenyekiti, nafurahi sana yale marekebisho yaliyofanywa na kamati, marekebisho nimeyapitia yale na nayaona ni ya msingi sana katika mswada wetu. Kubwa naomba sana nipongeze yale marekebisho yaliyofanywa kwenye Kamati za Utalii za Wilaya kwanza zile kazi zenyewe na wale wajumbe. Kwenye kazi hasa nimevutiwa hapa alipomalizia Mhe. Nassor Ahmed Mazrui aliposema kwamba ni lazima tuendeleze dhana ya Utalii kwa Wote *(Tourism for All)* hii ndio *theme* yetu ya utalii kwa nchi yetu. Kama tulivyoazimia kulifufua zao la karafuu na kuliendeleza na kuliuza ipasavyo basi na utalii sasa halikadhalika sote tuzungumze utalii, utalii, utalii.

Mhe. Mwenyekiti, imezungumzwa katika zile Kamati za Wilaya kwamba kuna Viongozi wa Dini wa Wilaya, kuna watu wa Mazingira, kuna Taasisi za Kiraia, kuna Mamlaka ya Vitega Uchumi, kuna Masheha, kuna Wafanyabiashara, kuna watu wa Ardhi, kuna Wakulima, hii inaonesha ile kwamba watu wa rika zote *(multi-sectoral)* wamewakilishwa kwenye kamati hizi.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la msingi sana kwa sababu mapungufu mengi ambayo tumeyabaini waheshimiwa wameyazungumza nafikiri kamati hizi zikifanya kazi vizuri zikafanya kazi ipasavyo mengi haya tunaweza tukayaondoa.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi nimefurahishwa kazi waliyopewa hii Kamati ya Utalii ya Wilaya pale Mhe. Nassor Ahmed Mazrui aliposema kwamba kulinda, kuendeleza na kukuza utamaduni wa kiasili wa Zanzibar kama ni sehemu ya bidhaa ya utalii. Ile nayo tunaiuza na hili Mhe. Mwenyekiti, si jambo rahisi nchi zote zenye watalii kuna matatizo makubwa sana kati ya zile silka, mila, tamaduni za nchi ile pamoja na watalii wanaoingia kunakuwa na mvutano na hasa vijana. Lakini sasa sisi wananchi ni wajibu wetu hasa kwa watoto wetu na vizazi tuwape taaluma ipasavyo ili wasifuate zile mila za kigeni. Ni ngumu kwa sababu mbali ya kuwaona tu watalii lakini hata wanaona kwenye michezo ya sinema, taarifa za habari za nje, lakini lazima tuwape mafunzo vijana wetu wasikopi yale mambo kidogo sio mazuri kwa jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui amezungumza suala la Indonesia kule mimi nitatoa mfano wa Cairo, Misri. Misri nao ni katika nchi ambazo zina watalii wengi kweli kweli na hasa kule Warusi. Kuna kisiwa kile cha Samir Sheikh kule watalii utafikiri labda kile kisiwa chao, sasa na Wamisri tunawajua waislam wengi kama sisi Zanzibar lakini hawafuati mila zao. Ukisikia *Allah Akbar* basi mle maduka yote wameweka mitandio ile ya kuzuia kwamba bidhaa kidogo zimefungwa na watalii wanaheshimu wanakaa wanangoja kwanza mpaka pamalizwe sala halafu maduka yanafunguliwa wanaendelea. Sasa haya mambo Mhe. Mwenyekiti, mimi niliona tujitahidi tuyaendeleze.

Lakini kubwa jengine Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kusisitiza sana suala la *promotion* na nimefurahi sana kwamba wenzetu wamejiandaa vizuri na tunawaona kwamba wanashiriki katika maonesho ya kilimwengu kama Ufaransa, Ujerumani, Japan, hata Uingereza. Lakini kubwa huko mbali mimi nasema yale magazeti tu ambayo yanaonesha mambo yetu.

Nitatoa mfano kuna hili journal moja Mhe. Mwenyekiti, linatolewa bure ndani ya ndege na hawa ndugu zetu wa *Precision Air* lakini karibu kila baada ya kurasa tatu kunazungumzia jambo la Zanzibar, vipi wanaitumia Zanzibar kukuza biashara yao na wanajua Zanzibar inavyozungumzwa.

Humu mmezungumzwa mambo ya Sauti za Busara, *collobus monkey*, pilau vipi inavyopikwa na viungo vyake, alimradi mambo kama haya ukiyazungumza wewe kwa mtalii basi ndio mambo ya kuuza. Sasa mimi ningeomba sana Mhe. Waziri haya tuyasisitize.

Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na gazeti letu lile la Karibu sijui linaendeleaje lakini ningeomba tuliendeleze na nafikiri litatusaidia sana. Mimi nimefurahishwa sana na hili na nitamuomba Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa sababu ni sekta yake tuwaombe *Precision Air* angalau kila Mhe. Mjumbe apate hili buku moja tuone vipi wenzetu hawa wanavyoutumia utalii katika kisiwa chetu kukuza biashara yao.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tu nafikiri kila baada ya saa moja hapa *Precision Air* inatua ndege yao. Zanzibar ni kituo chao kimoja kikubwa sana wanafanya biashara kubwa sana. Sasa suala la *promotion* Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba tulitilie mkazo sana.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ajira sipendi kulisisitiza sana Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumza. Lakini kuna utabiri wa jinsi kasi yetu ya utalii inavyokwenda ambapo sasa tunaambiwa kwamba utalii wetu unakua kwa asilimia 15 na zaidi kwa kila mwaka na kuletea *GDP* ya asilimia 25, basi inakisiwa kwamba nusu ya Wazanzibari kwa njia moja au nyengine ifikapo mwaka 2020 watakuwa nao wamejihusisha na utalii, sio moja kwa moja tu, kwa njia moja au nyengine.

Hii Mhe. Mwenyekiti, inathibitisha katika mapato Mhe. Ali Mzee Ali alinukuu lakini mimi naomba nizitaje sekta chache ambazo moja kwa moja hizi zinachangia utalii. Kwa mujibu wa takwimu hizi za *Zanzibar Revenue Board*

nachukua mwezi wa Februari tu mwaka huu katika vianzio 15 basi vianzio 7 hivi ndio moja kwa moja vya utalii na viko juu kabisa au kwa njia moja au nyengine vinachangia utalii. Kwanza kuna *hotel levy, restaurant levy, tour operation levy, airport service charge, seaport service charge*, hata *petroleum levy* nayo inachangia, *airport safety fee*. Hizi ndio moja kwa moja zinachangia lakini hata nyengine nazo kwa njia moja au nyengine zinachangia.

Kwa hivyo, ile dhana ya kwamba Utalii kwa Wote au kwa njia moja au nyengine utalii unachangia pato letu la taifa kwa asilimia kama ilivyozungumzwa 70 mpaka 80 ni kweli kabisa na tuna kila sababu ya kuusaidia utalii ukue.

Mhe. Mwenyekiti, si jambo la kuficha kwamba Chuo chetu cha Utalii kinafanya vizuri tusijiangushe, chuo chetu kina hadhi kinatoa wanataaluma na vyeti vyao vinatambulika kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja tulikuwa Doha pale tulialikwa mkutano, basi tuko kwenye *restaurant* tunaongea Kiswahili tunaangalia nyuma hivi wakatushtua jamani hamjambo, hatujambo, nyinyi nani, sisi Wazanzibari, mnafanya nini hapa, tuko Doha hapa bwana. Mhe. Mwenyekiti, *Doha Hilton Five Star Hotel, graduate* wa Chuo cha Utalii wamepata kazi pale.

Sasa chuo chetu kinatambulikana kimataifa wanaopata kazi pale wana sifa zote. Kwa hivyo, mimi naungana na wenzangu kwamba chuo kile tukiendeleze tuna kila sababu tuwe na fahari wasiwe na *inferiority complex* wanaohitimu pale kwamba wawe labda wamesoma pale kuna watu wamesoma Mombasa, Nairobi, Dar es Salaam hata kidogo. Chuo kile kinatambulikana tena wana-*apply* kwenye mitandao tu. Tumewauliza mmepata vipi kazi, wakasema aaa tumeona tu kwenye mtandao kuna nafasi ya kazi tumejaribu tumepata. Tumewakuta watano kwenye *Doha Hilton*. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, naomba kusisitiza tu kwamba chuo chetu kinafanya kazi nzuri na iko haja tukiendeleze ili tuweze kutoa matunda zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kama nilivyosema Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia sana na mimi sina zaidi ya kusema nilikuwa najaribu kukazia tu yale mambo ya msingi ya hapa na pale. Kwa hivyo, nimalizie kama alivyosema Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, sasa *theme* ya serikali yetu ni utalii kwa wote, *tourism for all.* Sote waheshimiwa tujifunge mkaja, wenzetu ambao hawajafahamu tuwafahamishe.

Mhe. Mwenyekiti, kule kwetu katika Jimbo la Dimani kuna visiwa viwili vya pungume na Kwale, basi asubuhi watalii wote wanaotoka Kiwengwa na kwengineko wanakuja kule wanapanda boti, watalii mamia kwa mamia kwa siku. Kwa hivyo, ajira ya wananchi wangu kule imekua kubwa kabisa na wanafaidika. Lakini mambo yale ya watalii ya kwenda wakaweka nguo zao na kuota jua, yale wanayawacha kule kule kisiwani, wakirudi huku wanavaa nguo zao za staha hao wanakwenda zao. Sasa haya yote ni lazima tuwaunge mkono wafanye yao na wastarehe wenyewe sisi tusiyaingilie yale na wao hawatayaingilia yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani, naomba kwaidhini yako nitoe majumuisho ya michango yote iliyotolewa juu ya Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii nambari 6 ya mwaka 2009 ya Kamisheni ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kutoa majumuisho haya kwanza kabisa nitoe shukrani zangu za dhati kwa wachangiaji wote na shukrani za pekee kwa kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari iliyochini ya Mwenyekiti wake Mhe. Asha Bakar Makame.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwataje Waheshimiwa Wajumbe waliochangia mswada huu kikamilifu nao ni kama wafuatao:

1. Mhe. Asha Bakar Makame
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Shawana Bukheti Hassan
4. Mhe. Asaa Othman Hamad
5. Mhe. Saleh Nassor Juma
6. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
7. Mhe. Raya Suleiman Hamad

8. Mhe. Farida Amour Mohammed – mchango wake kwa maandishi
9. Mhe. Abdi Mosi Kombo – mchango wake kwa maandishi
10. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
11. Mhe. Asha Abdu Haji – mchango wake kwa maandishi
12. Mhe. Hassan Hamad Omar
13. Mhe. Bikame Yussuf Hamad – mchango wake kwa maandishi
14. Mhe. Hamza Hassan Juma
15. Mhe. Subeit Khamis Faki
16. Mhe. Fatma Mbarouk Said
17. Mhe. Mgeni Hassan Juma
18. Mhe. Ashura Sharif Ali
19. Mhe. Ali Mzee Ali
20. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
21. Mhe. Panya Ali Abdalla – mchango wake kwa maandishi
22. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
23. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Mwenyekiti, takriban wajumbe wote waliochangia mswada huu walikua ni wajumbe 23, nawashukuru sana. Shukrani za pekee vile vile zimwendee Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ambaye na yeye wakati nilipokua waziri wa wizara hiyo, namshukuru kwa umoja wake na mashirikiano yake aliyonipa kwa wakati wote katika kufanikisha kazi za wizara hiyo. Upole, busara, ushauri na mawazo yake katika kazi sitayasahau kabisa, namwambia ahsante sana kwa mashirikiano aliyonipa.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika hoja ambazo zilitolewa na wajumbe ambapo wengine walitoa mapendekezo na wengine walitoa kasoro na yote tunayakubali na tutaeleza moja baada ya jengine, ili kuona ni kwa kiasi gani tunaweza kusaidia kwa yale ambayo yamesahaulika au mengine labda hayajaridhisha, basi kwa pamoja tutajadilia na yanazungumzika.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuhusu michango ya wajumbe katika Mswada wa Kurekebisha Sheria ya Utalii katika kifungu cha 3(c), tunakubaliana na mjumbe kwamba hili neno la *executive secretary* litumike badala ya *executive director*. Kwa hivyo, hilo linakubalika tulikosea tu kimaandishi, lakini tulikusudia ni executive *secretary.*

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 3(b), kutokana na utata uliojitokeza katika tafsiri ya neno ‘starehe’. Tumeshauri neno ‘burudani’ litumike badala ya neno ‘starehe’. Nafikiri kidogo linaweza kukubalika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya neno ‘aya’ ambalo lilipigiwa kelele sana hili kama lilivyotumika katika kifungu cha 4. Tnakubaliana na Mhe. Mjumbe kuondosha neno hilo na badala yake litumike neno ‘kifungu kidogo’.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kuondoshwa kwa kifungu cha 5(1) (d) (ii), jumuiya ya watembezaji watalii. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinakusudiwa watembezaji na wauza misafara ya watalii, kwa Kiingereza wanaitwa *tour operators and travel agency*. Hawa ndio watembezaji watalii na wauza misafara. Tumeshauri kifungu hiki kiendelee kubakia kutokana na umuhimu wa jumuiya hizo katika kuendeleza na kukuza utalii, kwani jumuiya hizo zina jukumu la kutoa huduma kwa wageni pamoja na kusaidia jitihada za serikali katika kuwatafuta wageni wao na kuwaleta nchini na kuwahudumia pale wanapokua nchini. Kwa hali hiyo, wana mchango mkubwa katika kujua mahitaji ya sekta kulingana na masoko ya wageni wanaowahudumia.

Hivyo, kuwa kwao katika safu ya makamishna kutasaidia kwa kiasi kikubwa kujua mwelekeo na mahitaji ya wageni katika nchi yetu, ili serikali iweze kujenga mazingira mazuri ya kutia na kuhakikisha kuwa wageni wanaendelea kuja Zanzibar na mahitajio yao yanatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee nasema vile vile huo ni mwendelezo wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi, yaani *Private and Public Partnership* (PPP).

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije kwenye kifungu cha 5(1) (b) (VI) ambacho kinazungumzia uteuzi wa mwanamke, nacho kidogo kilileta mjadala. Tunakubaliana na hoja ya wajumbe ya kwa kumwekea sifa zake.

Tunashauri uteuzi wa mwanamke uzingatie uwezo wa kielimu na uzoefu katika masuala ya utalii, uchumi na biashara.

Aidha, kuhusiana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe kuhusu uteuzi kuzingatia jinsia, yaani *Gender*. Napenda kuwajulisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba uteuzi wa makamishna umezingatia zaidi taasisi na sio mtu. Hivyo, ni matarajio yetu kuwa taasisi itateua mtu ambaye atakua na uwezo bila ya kujali jinsia yake.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 5(2). Tunakubaliana na mapendekezo ya wajumbe kuwa Mwenyekiti akae madarakani sio zaidi ya vipindi viwili.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 5(3) (ii), awe na ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo. Hili nalo kidogo lilileta mjadala ni mambo gani hayo. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki tunakubaliana na ushauri wa wajumbe wa kuongeza uwezo katika sekta hii. Aidha, makusudio ya kifungu hiki, sio kama kinavyosomeka bali kimekusudiwa kwamba mwenyekiti awe na ujuzi mkubwa wa kushawishi na kushauri mambo katika masuala ya utalii yaani *advocate skills*.

Aidha, tunakubaliana na ushauri wa wajumbe wa kuwa mwenyekiti awe ni Mzanzibari na awe na kiwango kisichopungua stashahada.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 5(3) (iii), Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe vile vile na kuongeza maneno ‘wa mataifa mbali mbali’.

Kifungu cha 6(1), pia tunakubaliana na maoni ya wajumbe ya kwamba mwenyekiti pamoja na kazi nyengine, ahusike na kwanza ushajihishaji wa taasisi za fedha ili kuweza kutoa mikopo kwa wananchi ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika biashara ya utalii. Vile vile kuwa na dhima ya kushajihisha na kukuza utalii wa ndani. Hayo yalikuwa ni maoni ya wajumbe na tumeyakubali na tumeyaingiza.

Vile vile kuhusu kifungu cha 6(1) (d), Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana na ushauri wa wajumbe wa kuongeza neno ‘kuendeleza’ katika kifungu hiki. Aidha, tunakubaliana na ushauri wa wajumbe wa kuongeza kazi za mwenyekiti, kwa kumpa kazi kama zilivyokwisha ainishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 6(4) mshahara na mafao ya mwenyekiti. Ushauri wa wajumbe utazingatiwa kwa sheria ya utumishi wa umma nambari 2 ya mwaka 2011 kulingana na masharti ya uteuzi. Hapa tulikuja na hoja tu kwamba kwa sababu mtu atakuwepo *full time*, kwa hivyo madamu atakuwepo *full time*, haitokua vyema kwamba asipate ile sheria ya utumishi nambari 2. Ingekua ni *part time* ingekua ni suala jengine, lakini kwa sababu huyu ni mtu muhimu sana. Tunasema ni muhimu kwanza kwa sababu ya ile dhana nzima ya utalii kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, mtu ambaye anaweza kuzungumza na umma ni mtu ambaye anaweza kuzungumza na nafsi yake. Kwa hivyo, kuwepo kwake *full time* kuna umuhimu mkubwa. Halafu tuelewe kwamba hii sekta au kamisheni ina mambo mengi sana na ina changamoto nyingi sana, kwa hivyo kuwepo kwake kutasaidia sana. Hatuwezi kumuachia katibu mtendaji peke yake hawezi kuyamaliza. Lakini kukiwa kuna mwenyekiti na kwa dhana nzima ile ya utalii kwa wote, tuna imani kwamba basi utalii utakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 9(a), makamishna kulipwa mafao kama waziri atakavyoamua. Hili nalo lilileta utata vile vile. Kwa heshima yako Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana na ushauri wa wajumbe na kuweka mpangilio maalum wa ulipaji wa mfao ya makamishna.

Aidha, napenda kuwahakikishia wajumbe kwamba makamishna hawa sio wa kudumu, bali watakuwa wanapatikana kwa muda tu.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea kifungu cha 11(2), kuhusu sifa za uteuzi wa katibu mtendaji. Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wameshauri kwamba katibu mtendaji awe na shahada ya pili. Mhe. Mwenyekiti, tunashauri sifa iliyoeleza katika sheria inatosheleza kwani inatoa fursa kwa anayeteua, kuteua mtu mwenye zaidi ya shahada moja.

Aidha, kuhusu uteuzi katika nafasi za ngazi kama hii na kwenye taasisi kama hizi unafuata mtiririko wa utumishi wa umma. Kwa hivyo, hakuna haja ya kuitangaza nafasi hii.

Vile vile kifungu cha 16(3) kuhusu mkurugenzi kutoa leseni za biashara ya utalii. Mhe. Mwenyekiti, michango ya wajumbe ya kuomba tena leseni au ku-*renew.* Suala hili limezingatiwa katika sheria mama kwenye kifungu 15(2) suala la adhabu, tutalizingatia katika kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 23(a) (1) kinahusu kamati za utalii za wilaya. Mhe. Mwenyekiti, tunakubali ushauri wa wajumbe wa kua uteuzi wa wajumbe wa kamati za utalii za wilaya, waziri ashirikiane na mkuu wa wilaya kuteua wajumbe hao.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 23(1) kinahusu kuongezwa kwa mjumbe wa kamati. Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana na michango ya wajumbe ya kumuongeza Afisa wa Utamaduni wa Wilaya katika Kamati na mjumbe mfanyabiashara, kua mfanyabiashara wa utalii.

Aidha, wajumbe wamependekeza mtu kutoka Idara ya Ardhi awe ni afisa. Kwa hivyo, tunakubaliana na ushauri huo na kwa kua neno ‘mtu’ limetumika sana katika kifungu hiki, basi tunashauri neno ‘afisa’ litumike badala ya neno ‘mtu’.

Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana na ushauri wa wajumbe wa kua makini katika uteuzi wa wajumbe wa kamati. Suala hilo tutakua makini. Aidha, suala la kumuongeza mwakilishi katika Kamati ya Utalii Wilaya na makamishna wa polisi katika makamishna, pamoja na kuwashirikisha watu wa bandari na uwanja wa ndege.

Mhe. Mwenyekiti, tunapenda kuwahakikishia wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba watu hao hawajasahauliwa, kwani marekebisho haya yamezingatia zaidi ushirikishwaji wa wadau wote wa utalii. Hivyo, imeundwa *forum* maalum kwa wadau hao. Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho kinafanyika kila mwaka hua tunawakutanisha wadau wote wa sekta ya utalii, kubadilishana fikra na kuangalia na kutathmini, ili kuona nini cha kuongeza na nini cha kupunguza. Kwa hivyo, nafikiri kulikua hakuna haja kwa sababu ipo *forum* hiyo kila mwaka. Hivyo, natumai Waheshimiwa Wajumbe wataliridhi hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 23(b) (1) (c), kuhusu mfuko wa fedha wa wananchi. Mhe. Mwenyekiti, michango iliyokusudiwa hapa sio ya kutolewa na wananchi, bali ni kutokana na sekta yenyewe. Hivyo, mtu yeyote ambaye atakua anajishughulisha na biashara ya utalii anaweza kuchangia mfuko huu kwa maendeleo ya kijiji.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 24(b) kinachohusu mtu ambaye sio Mtanzania kupata ruhusa ya maandishi kutoka kwa waziri. Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana na rai hiyo ya wajumbe ya kwamba mamlaka haya yaachiwe kamisheni. Kwa hivyo, tunashauri marekebisho ya kifungu hiki yaondolewe na kifungu kibakie kama kinavyosomeka katika sheria mama.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea na hoja ambazo zimetolewa juu ya masuala ya mila, silka, ajira na ujenzi wa hoteli ufukweni. Mhe. Mwenyekiti, suala la uporomokaji wa maadili limekua likizungumzwa sana, ambalo linaelekeza moja kwa moja katika sekta ya utalii. Mhe. Mwenyekiti, hakuna utafiti uliofanywa ambao unaonesha kuwa utalii unachangia kwa kiasi kikubwa katika kuporomoka kwa maadili ya Wazanzibari. Hivyo, suala la kumomonyoka kwa maadili halihusiani moja kwa moja na utalii, kwani kuna mambo mengi yanayochangia kuporomoka kwa maadili yakiwemo suala la utandawazi na kukua kwa matumizi ya sayansi na teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, matumizi mabaya ya mitandao ya *internet* kuwepo na kupatikana kwa *channels* mbali mbali za televisheni ambazo baadhi yake hazifai katika mazingira yetu. Matumizi mabaya ya simu za mikononi, magazeti huchangia kwa kiasi kikubwa kuporomoka kwa utamaduni na silka za baadhi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo pia linachangia kuporomoka kwa maadili yetu ni tabia ya baadhi ya watu na hasa watoto, kupenda kuingia au kuiga tamaduni za kigeni, jambo hili linakwenda sambamba na wazazi kutowaonya watoto pale wanapoanza kubadili tabia ambayo hua tofauti na utamaduni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuyadhibiti haya ni vyema basi jamii ya Wazanzibari ikarejea katika malezi yetu ya zamani ambapo watoto hulelewa na jamii ila na wazazi tulikubali hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa utamaduni wetu serikali imeunda kamisheni ya utamaduni, iliyopewa jukumu la kusimamia utamaduni wa Mzanzibari na kuhakikisha kua unalindwa na kuhifadhiwa kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa malengo ya kuanzishwa kwa kamati za utalii za wilaya ni pamoja na kusaidia katika maadili na hii inaoneshwa katika majukumu ya kamati.

Kifungu cha 23(b) (1) (f), hapa ndipo unapoonekana ule umuhimu wa kamati hizi, kama pale nilivyosema utalii kwa wote. Ndio maana tukasema kamati hii ishirikishe wadau wote wa kila taasisi ya kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, kamisheni inatambua umuhimu wa maadili ya Mzanzibari na lengo lake ni kutumia utamaduni wa Mzanzibari kama ni kivutio cha watalii. Halikadhalika tunakubaliana na ushauri wa wajumbe wa kuweka kipengele cha kutunza maadili ndani ya sheria. Kipengele hiki kinaonekana katika kifungu cha 23(b) (1) (f).

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa hoteli katika maeneo ya fukwe kutofuata viwango vilivyowekwa ili kudhibiti mazingira. Suala hili husimamiwa na sheria za ardhi na mazingira, kwani mradi wowote wakati wa ujenzi unapaswa kusimamiwa na taasisi hizo ili kuhakikisha kua ujenzi huo unafuata sheria zilizowekwa pamoja na masharti ya ujenzi waliyopewa.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba ajira ni nyanja muhimu katika kupima utalii unaonufaisha nchi husika. Lakini kadiri siku zinavyokwenda ndipo wananchi wetu na wao wanapata ajira katika sekta hii ikilinganishwa na huko mwanzo tulipoanzia. Juhudi kubwa zilichukuliwa kwa kukitanua na kukiendeleza chuo cha utalii Maruhubi, ili kuhakikisha kwamba vijana wetu wengi wanapata mafunzo ya utalii ili waweze kuajiriwa katika soko la utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna nia thabiti ya kukikuza chuo hiki ili kiweze kwenda sambamba na soko la ajira. Kama mnakumbuka Baraza la Wawakilishi lilipitisha hapa kiasi cha milioni 4 kwa ajili ya ujenzi wa chuo hiki. Vile vile kuna mradi huu wa ADB ambao hivi karibuni utaanza ujenzi wa chuo hiki. Mhe. Mwenyekiti, kuhusu sheria ya uajiri haimfungi mtu yeyote kufanya kazi Zanzibar, hata kile kipaumbele kinatolewa zaidi kwa Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la usimamizi wa utendaji kazi katika sehemu za utalii. Suala hili haliko katika mamlaka ya kamisheni kisheria. Kwani sheria ya ajira ndio yenye mamlaka ya ajira. Hata kamisheni huangalia mazingira ya wafanyakazi na kutoa ushauri pale inapohitajika.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kulipa malipo zaidi kwa mtu anayetaka kuajiri asiyekuwa Mtanzania. Hili linasimamiwa moja kwa moja na sheria ya kazi, sheria nambari 11 ya mwaka 2005 na halimo katika mamlaka ya kamisheni.
Mhe. Mwenyekiti, kuhusu watalii wanaokuja Zanzibar kulipia kwao. Naomba kutoa maelezo kidogo juu ya suala hili. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar inapata watalii wa aina mbili. Kuna wale wanaokuja kwa makundi na wale wanaokuja mmoja mmoja. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar inapokea kiasi kikubwa cha wageni wanaokuja kwa makundi yaani kwa asilimia 60 na asilimia 40 pekee ndio wanaokuja kwa kujitegemea, yaani mmoja mmoja.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hali hii hatuwezi kuiepuka kwa hivi sasa kutokana na sababu zifuatazo. Kwanza kutokua na uhakika wa uchumi wa ulimwengu hai, hii ilijitokeza zaidi katika kipindi cha mwaka 2008 na Zanzibar iliweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa, ukilinganisha na nchi nyengine kutokana na aina ya utalii huu wa makundi.

Vile vile kukosa Shirika la Ndege la moja kwa moja kutoka kwenye masoko ambayo tunayategemea kupata watalii wetu, yaani Ulaya na Amerika. Hali hii inapelekea kukosa wageni wakujitegemea na hivyo wageni wa makundi au wa misafara huwa ni bora zaidi kwetu.

Halikadhalika umbali wa Zanzibar na masoko yetu, watalii wa kujitegemea hupendelea zaidi kwenda sehemu zilizokaribu na kwao. Aidha, usumbufu wakati wa safari nao unachangia kukosa wageni wa kujitegemea.

(Hapa umeme ulizimwa na kuwaka kwa muda wa dakika 2)

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba watalii wa makundi hulipa pesa zote kwao. Hata hivyo, kutokana na matumizi yanayofanywa na hoteli wanazofikia ni dhahiri kwamba baadhi ya pesa hizo hubakia nchini kulipia huduma walizotumia.

Kwa mfano, kodi za kiwanja cha ndege, maegesho, usafiri wa ndani, viingilio katika maeneo ya utalii

(Hapa umeme ulizimwa tena)

Wajumbe: Pasaka hii. Eeh! mtihani.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tuwe na ustahamilivu kidogo unaweza ukawashwa tena.

(Baada ya dakika 3 umeme uliwaka)

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee Mhe. Mjumbe.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba watalii wa makundi hulipa pesa zote kwao, hata hivyo kutokana na matumizi yanayofanywa na hoteli wanazofikia ni dhahiri kwamba baadhi ya pesa hizo hubakia nchini kulipia huduma walizotumia.

Kwa mfano, kodi ya za Kiwanja cha Ndege, maegesho ya usafiri wa ndani, viingilio katika maeneo ya kitalii, kodi za mahoteli pamoja na kulipwa wasambazaji wa huduma wanazozitumia.

Kuhusu ufafanuzi wa maeneo yaliyoingizwa katika kifungu cha 2(f), kuhusu muongoza watalii. Mhe. Mwenyekiti, katika tafsiri iliyokuwepo katika sheria mama imeonekana kua na mapungufu na hivyo yameongezwa maneno haya ili kuondosha hayo mapungufu yaliyojitokeza. Hata hivyo, kifungu hiki kitasomeka kama ifuatavyo.

Muongoza Watalii, maana yake ni mtu anayetoa taarifa kufahamisha, kuelekeza watalii kwa malipo kuhusu maeneo, uoto, utamaduni, uwasili, jografia, historia na mambo yanayofanana na hayo

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kutokana na taratibu zetu Kanuni ya 71 haituruhusu kuchukua maamuzi iwapo hatutotimia nusu ya Baraza. Kwa kweli idadi ya Waheshimiwa Wajumbe ninaowaona hapa bado haijatimia nusu.
Kwa hivyo, naomba tupumzike kwa dakika tano, ili wahudumu waweze kwenda nje kwa ajili ya kuwatafuta Waheshimiwa Wajumbe na baadaye tuendelee. Nakushukuruni.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Utalii Nam. 6 ya 2009 pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima, ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA BARAZA ZIMA
Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii, Nam. 6 ya 2009

Kifungu cha 1	-	Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu cha 2	-	Kusomwa
Kifungu cha 3	-	Marekebisho ya kifungu cha 2 pamoja Marekebisho yake.
Kifungu cha 4	-	Marekebisho ya kifungu cha 4 pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 5	-	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Wakati nilipokuwa nikitoa mchango wangu kuhusiana na kifungu cha 5 cha mswada nilipendekeza mambo kadhaa, ambayo katika majumuisho ya Mhe. Waziri kwa bahati mbaya sikusikia kuyazungumzia. Kwa mfano, moja nilipendekeza kwamba kile kifungu cha 5(1) (b) (i) Wadau wa utalii, kuwa kisomeke Jumuia ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii, kwa kutambua kwamba wanayo jumuia yao kama ilivyotajwa kwenye kifungu cha 2 Jumuia ya Watembezaji na Wasafirisha Watalii.

Vile vile katika Muundo wa Kamisheni nilipendekeza kwamba kama ilivyo kwa Kamati za Utalii za Wilaya, ambazo zimeingiza Viongozi wa Kidini, basi nilipendekeza kwenye Makamishna hapa awepo Mjumbe mmoja ambaye anayewakilisha Taasisi za Kidini kwa ajili ya kusimamia masuala ya maadili na hilo Mhe. Waziri hakuligusa kabisa kwenye majumuisho yake. Kwa hivyo, naomba kusikia kauli ya Mhe. Waziri kuhusiana na masuala hayo Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kwamba Mhe. Mjumbe alitaka kwenye Wadau wa Utalii, iingizwe Jumuia ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii, tumeingiza na tunakubali hilo. Kwa hivyo, kitasomeka hivi Jumuia ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii (*ZATI*) na pia kuna Jumuia ya Watembezaji na Kusafirisha Watalii, ambayo inaitwa (*ZATO*) na hizo hazina matatizo nimekubali Mhe. Mwenyekiti ahsante. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kuna suala zima la watu wa dini ambalo Mhe. Mjumbe aliomba pia wahusishwe na Kamati hii na wala hili hukulijibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, labda naomba kujua wahusishwe katika ngazi gani hasa, yaani ya wilaya au taifa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba katika ngazi ya wilaya tayari wametajwa hapa.

Kwa hivyo, nilipendekeza hapa kwa sababu tunazungumzia kifungu cha 5 kwenye hii Kamisheni huku juu katika wale Makamishna kama ambavyo kuna *stakeholders* tofauti, ambao wametakiwa wawemo kwa ajili ya kulinda zile *interest* zao.

Kwa kweli suala linalopigiwa kelele kubwa sana katika nchi yetu ni suala zima la maadili kwenye Sekta hii ya Utalii, basi nilipendekeza katika Makamishna awepo Kamishna mmoja ambaye anawakilisha Taasisi za Kidini Zanzibar, ambaye atakuwa anaisaidia Kamisheni kwa kuipa mawazo, fikra pamoja na njia za namna gani kuhakikisha Sekta ya Utalii inakwenda sambamba na maadili yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri hata Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko wakati alipokuwa akichangia ameligusia kwamba kuna nchi za wenzetu wamefanikisha hilo. Kwa hivyo, tukitaka na sisi utalii wetu uendane na maadili yetu basi inawezekana, ndio nikapendekeza hapa kwenye hao Makamishna atajwe pia Kamishna mmoja ambaye atawakilisha Jumuia na Taasisi za Kidini Zanzibar. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakubali hakuna mashaka tutaliingiza. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuongezea nyama kidogo.

Kwanza nataka nishukuru pamoja na kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa mambo mengi ambayo tuliyoyashauri mengi ameyakubali nafikiri wizara anaiaga vizuri, tunampongeza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza hoja hapa kwenye kifungu cha 5(1) naomba kunukuu.

Kifungu cha 5(1) kinaeleza hivi:-

> "Kamisheni itakuwa na:
>
> (a) Mwenyekiti atakayekuwa Mkuu wa Kamisheni kwa muda wote na ambaye atateuliwa na Rais.
>
> (b) Makamishna wengine wasiozidi sita watakaoteuliwa na Waziri kutoka katika hizi taasisi zilizoelezwa".

Mhe. Mwenyekiti, nilishauri kwamba hili ni wazo lililokuja kuwa Makamishna wawe sita ambao watakaoteuliwa na Waziri, lakini hawa wote waliotajwa hapa ni muhimu na kutokuwepo itakuwa ni tatizo. Pamoja na hayo, kuna taasisi moja ambayo ni muhimu sana ambayo hapa haikutajwa nayo ni Idara ya Mazingira.

Kwa hivyo, mimi nilipendekeza Makamishna badala ya kuwa sita wawe saba, ili Mkurugenzi anayeshughulikia Masuala ya Mazingira aingie hapa. Kwa kweli hili nalizungumza Mhe. Mwenyekiti wewe mwenyewe ni shahidi kwamba ni Mjumbe wa Kamati yangu, wakati tunapotembelea katika maeneo ya mahoteli ya utalii, basi mengi sana yanakiuka utaratibu katika uhifadhi wa mazingira na mengine yalijengwa katika miaka ya 1990 yalifuata Sheria zote za Mazingira.

Lakini hivi sasa wameanza kufanya ukarabati wanaingia mpaka kwenye yale maeneo ambayo hayaruhusiwi kimazingira. Kwa maana hiyo, hoja hii Mhe. Waziri ameitilia nguvu katika kifungu cha 19(a) cha mswada huu naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 19A (1) kuhusu Masharti ya kubadilisha biashara ya utalii kinaeleza hivi:-

> "Mtu aliyeruhusiwa kufanya biashara ya utalii hatofanya mabadiliko katika ofisi yake au jengo, wanahisa au wakurugenzi, jina la biashara au huduma anayoitoa mpaka awasilishe kwa Kamisheni maelezo ya mapendekezo ya mabadiliko au marekebisho yanayokusudiwa kwa maandishi".

Mhe. Mwenyekiti, ina maana hapa ndio inazidi kutilia nguvu, kwa sababu hawa wanapofanya marekebisho ya majengo yao taarifa wapeleke kwa Kamisheni. Sasa huku Kamisheni kama hayupo mtu ambaye anatoa ushauri au mwenye kusimamia mazingira, ndipo pale utakapokuja kuona majengo tayari yameshatolewa leseni, lakini ukienda kwenye *field* uharibifu wa mazingira umetokea na kwasababu hakuwepo mtu mwenye kusimamia.

Hata hivyo, miradi yetu yote mikubwa Mhe. Mwenyekiti, inatakiwa kabla ya kufanyika lazima kwanza ifanyiwe ile *Environment Assessment Impact*, sasa huyu ndiye mwenyewe na hapa hayupo.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba akubaliane na hoja yangu aongeze badala ya watu sita wawe saba na mmoja awe Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira, kwa ajili ya kuondoa matatizo ya mazingira huko mbele. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kuongeza Mkurugenzi wa Mazingira si vibaya, lakini tuelewe tu kwamba kilichozungumziwa hapa hasa ni Kamisheni kuwa

na taarifa, kwa sababu mambo ya mazingira na wanapotaka kuanza *investment* huwa haji katika Kamisheni ya Utalii.

Kwa hivyo, lazima anakwenda kwenye taasisi husika, yaani anakwenda *ZIPA* na bila ya shaka kule anakutana na taasisi mbali mbali na kwanza lazima apeleke *document* kutoka Idara ya Mazingira iwe tayari imeshapitishwa pamoja na sehemu nyengine, kwa sababu zile ndio taasisi ambazo zinazohusika na hii *investment*. Mhe. Mwenyekiti, sisi Kamisheni wajibu wetu ni kupata ile taarifa kwa ajili ya kujua tu kwamba kuna kitu fulani kimefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna mifano mingi tu ambayo imetokezea ya kutaka taarifa hizi, kwa sababu kuna watu wetu ambao wanaojenga mahoteli na halafu baadaye akamuuzia Mzungu. Sasa inawezekana baadaye wamenyang'anyana huko na halafu anakuja wakati jambo tayari limeshaharibika.

Kwa hivyo, tukasema hapana na tukasema kwamba bora unapofanya mambo haya usifanye kwanza mpaka utuletee taarifa, ili tuelewe na sisi tuwe na *information*, ndio maana tukasema kwamba hakuna umuhimu sana wa Mkurugenzi wa mazingira kuwepo hapa, kwa sababu anapofikia kujenga huyu ina maana tayari ameshapitia kwa Mkurugenzi wa Mazingira na wala hawezi kukubaliwa kama hajapitia huko.

Kwa hiyo, tunaona hakuna umuhimu wa kumuingiza, kwani hii ni *process* yetu inapita, kama vile kwenye mazingira pamoja na sehemu nyengine mbali mbali na mpaka tunafika hapa tunampa leseni ya kufanya *Hotel Operation*. Mhe. Mwenyekiti, sisi tumeona hivyo na kwa mantiki hiyo tunahisi hakuna ulazima. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri tutahadhari kabla ya athari. Kwa kweli hivi sasa hoteli zinajengwa na sheria inasema kabla ya kujengwa hayo mahoteli ifanyike hiyo tathmini ya mazingira, lakini ndio hayo yanajengwa na kuharibu mazingira. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba kuna hoteli nyengine ambazo zimejengwa kwa muda mrefu, lakini zinakuja kufanyiwa ukarabati wenyewe sasa ndio unakwenda katika kuharibu hayo mazingira.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana nikasema kwamba Kamisheni wakija kupelekewa hiyo taarifa kama yupo mwenyewe mdau wa mazingira, basi kitu cha mwanzo kwa sababu yeye yupo pale kwa ajili ya kuangalia athari ya mazingira na hili ndilo tunaloliona.

Mhe. Mwenyekiti, kama tukichukulia uzoefu kweli hiyo miradi inapitia ardhi, mazingira, lakini hakuna hatua zozote ambazo zinazochukuliwa na uharibifu wa mazingira unatokezea. Kwa kweli kwa umuhimu wa miradi hivi sasa Taasisi ya Mazingira inakuwa kama chumvi, yaani kila pahala wanatakiwa wawepo na washirikishwe kikamilifu kuanzia pale mwanzo.

Kwa mfano, hivi sasa kuna hizi hoteli ambazo leseni zao wanapata kutoka kwenye Kamisheni na Mhe. Mwenyekiti ni shahidi tumeshakwenda watu wamejenga ndani ya fukwe, yaani tokea wanaanza kuchimba wanachukua mchanga baharini wanafukia na *Restaurant* iko ndani ya bahari. Sasa kama atakuwepo mtu wa mazingira hatokubali kufanya *extension* au kutoa kibali ambapo watu wameharibu mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana kwa sababu tatizo wakati tunapokwenda kwenye kamati wakati mwengine tunaonekana wakorofi, mimi nikiona sheria imekiukwa namwambia ondoa jengo lako au vunja, kwa sababu amekiuka sheria. Kwa hivyo, ili tusiende huko isiwe siku zote, kwa sababu ndio maana tunasema kwamba hizi sheria zetu tufike pahala tuzichome moto.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anikubalie kwa sababu mtu wa mazingira hivi sasa ni chumvi kwa kila eneo, nafikiri Mhe. Waziri anikubalie.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sikatai kwa sababu suala hili mpaka kufikia Kamisheni ya Utalii hapewi *certificate* yoyote ya ku-*operate* mpaka pale amekidhi yale masharti ya *ZIPA*. Kwa hivyo, kama amekwenda kujenga tu sisi hatuna mamlaka kiasi hicho. Kwa kweli jambo kubwa hapa ni kushirikiana kwa Kamisheni na *ZIPA*, ili tuhakikishe kwamba watu wetu wanafuata yale masharti. Kwa maana hiyo, sioni kama kuna sababu lazima aweko huku, kwa sababu mtu wa mazingira yupo kule na itakuwa kama tumemuingilia kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe aniachie hili kwa sababu nimemuachia mambo mengi, hivyo namuomba aniachie na tutalifuatilia kwa karibu sana kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira pamoja na *ZIPA* yenyewe, ili tuhakikishe kwamba watu wote wanafuata yale masharti tunayoyataka.

Kwa kweli naona si jambo kubwa, kwa sababu hata tukimuingiza kama hataki basi anaweza kufanya tu na hilo ni tatizo, yaani kila kitu tukapitisha sisi na baadaye kwani wapo wengi waliofuata hizo sheria na baadaye wakakiuka. Kwa hivyo, nadhani ni suala la ufuatiliaji tu, yaani kuhakikisha ile sheria inasimamiwa pamoja na kutiliwa mkazo. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri tufanye hivyo namuomba Mhe. Mjumbe anikubalie kwa hisani yake. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tuangalie na Sheria zetu za Uwekezaji pamoja na mambo mengine zinavyosema na haya tunayakuta wakati tunapokwenda kwenye ziara za Kamati. Kwa kweli kuna miradi mingi ambayo inafanywa, lakini wakati tunapowauliza watu wa Idara ya Mazingira kupitia Mkurugenzi, anasema tatizo letu hatushirikishwi. Sasa ina maana kushirikishwa mtu ukimtia kwenye sheria hawezi tena kuja kutoka au kukataa.

Kwa hiyo, hapa ndio maana nikasema kwamba kumuongeza mtu mmoja kutoka watu sita na kuwa saba na huyu mpaka hizo sheria zinasema mwekezaji yeyote lazima upate *authority* ya Mamlaka ya Mazingira, lakini tayari ndio maana wakati mwengine tunakwenda na kulaumu, kwa nini Kamisheni ya Utalii mmetoa leseni. Mhe. Mwenyekiti, kama hapa kwenye kifungu cha 19 mumesema wenyewe anapotaka kufanya ukarabati aidha wa jengo au ofisi lazima atoe taarifa Kamisheni.

Kutokana na hali hiyo, labda nitoe mifano ambayo taasisi yake Mhe. Waziri imeshatoa leseni kuna Hoteli inayoitwa Palumbo Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri atembelee. Kwa kweli hivi sasa *Restaurant* imo ndani ya uharibifu wa mazingira, yaani wamechimba ndani ya bahari na kuweka tuta kwa kuchukua mchanga baharini na kufukia pale na tayari tumeshawapa leseni na wanaendelea kunywa *soda* na chai pale.

Mhe. Mwenyekiti, kama kwenye Kamisheni atakuwepo mtu wa Idara ya Mazingira hatokubali kitu hiki, ndipo pale tunaposema kwamba tutakwenda kuwabomolesha watu vitu wakati kumbe sisi wenyewe hatukujipanga vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri katika miradi yetu yote narejea kusema kwamba takribani miradi yetu inakiuka masharti ya mazingira na unapokwenda Idara ya Mazingira wanakwambia hatukushirikishwa.

Lakini kama kwenye Kamisheni tumeshamuingiza kwenye sheria na hapa tunakuja kumkamata kwa nini ilitoka leseni ya huyu kuweza ku-*operate* katika sehemu ambayo ameharibu mazingira na yeye ni Mjumbe wa Kamisheni basi tutapata kumuadhibu, lakini hapa hatujamtaja tutamuadhibu wapi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mhe. Hamza Hassan Juma, naomba tuangalie kifungu cha 5 ambacho tunachokijadili. Lakini hapa ni mambo ambayo naweza kusema ni *national*, sasa unapoanza *project* yako unakwenda *ZIPA*, ambapo kule yote haya ya mazingira wanayatizama na wala wao hawawezi ku-*approve project* kama masuala haya ya mazingira hayapo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kujua hayo serikali kwa kupitia sheria hii imeweka kwenye kifungu cha 23 naomba tukiangalie. Kwa hiyo, kwenye zile Kamati za Wilaya ambapo hiyo *project* yako utakwenda kuitengeneza au kuifanya huko katika wilaya kuna kifungu cha 23(h) kuna mtu mmoja kutoka Wizara ya Mazingira, sasa pale ndipo anapotakiwa yule mtu wa mazingira atizame pale *project* inaanza katika wilaya au eneo lako kwamba mtu wa mazingira yupo.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna haja ya kuweka kwenye kifungu cha 5 katika *national* kwa sababu huku tayari imeshakuwa *approved*. Lakini kule wilayani huyo mtu anayesema Mhe. Hamza Hassan Juma yupo.

Kwa hivyo, kwa maelezo haya Mhe. Mwenyekiti, hakuna haja ya kuweka mtu wa mazingira katika kifungu cha 5, hasa kwa sababu imekuwa *taken care* katika kifungu cha 23(a) katika wilaya ambapo *project* yenyewe inafanywa. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma, naifahamu sana *concern* yako, kwa sababu mimi na wewe tumo kwenye Kamati mmoja na hayo ambayo unayasema wewe na mimi niliyasema pia. Kwa hivyo, naomba kukupa

nafasi ya mwisho kwa ajili ya kutetea hiyo hoja yako. Lakini namuomba Mhe. Waziri naye aichukulie hiyo kwamba ni muhimu kwa sababu ni kweli kunahitajika kiungo cha mazingira.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kutumia kura ya *VETO*. *(Makofi)*

Kwa kweli kawaida ya Mwenyekiti anakuwa hachangii katika vifungu, lakini hapa ametia uzito kwa kuona umuhimu wa huyu kiungo wa mazingira. Kwa nini amelizungumza hili Mhe. Mwenyekiti? Kwa sababu tunayaona na tunajiuliza, hivi jamani kweli haya yanayofanyika hizi taasisi kweli zipo, lakini unapokuja Idara ya Mazingira wanakwambia hatukushirikishwa.
Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria hiki kifungu cha 23 nilikiona. Lakini hii Kamisheni ndio yenye maamuzi na wale kule Kamati ya Wilaya baada ya maamuzi ya huku. Kwa hivyo, ndipo pale niliposema hata miradi mingine yote inayopita *ZIPA*, kwa sababu hao *ZIPA* kabla ya ku-*approve* mradi lazima huo mradi ufanyiwe *assessment* ya mazingira.

Kutokana na hali hiyo, ndipo pale tuliposema kwamba ili hivi sasa tuisende huko ambako tumeharibikiwa basi tumuweke hapa huyu Mkurugenzi wa Mazingira hayo hayatotokezea tena. Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira kwa kuwa hakushirikishwa tokea mwanzo. Kwa kweli matokeo yake hivi sasa katika Kamati yangu ninazo *copies* za barua za *Stop Order* nyingi sana katika hoteli nyingi, hivyo Mkurugenzi tumpe meno aende kuvunja, sasa tutakuja kuonekana kwamba huku tunajenga na kule tunabomoa.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana tukasema kwamba na hii hoja sio kama yetu sisi tu, isipokuwa ndivyo inavyotakiwa, yaani mtu wa mazingira katika *project* yoyote anatakiwa awe ile sehemu ya juu ya maamuzi na sio kwenye wilaya, kwa sababu wilaya wanapokea maagizo.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwa kuangalia uzito wa kiti chako na wewe ulisisitiza hilo kwamba aliangalie hilo, basi nadhani Mhe. Waziri atatumia busara atakubaliana na mimi. Ahsante.

Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi, pia nataka nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kututanabahisha sana upande wetu wa serikali, kwamba tuwe waangalifu zaidi katika kusimamia suala la mazingira.

Kwa kweli nataka nimhakikishie Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba suala la mazingira linapewa kipaumbele na haya makosa yanayofanyika kwenye ujenzi ambao haufuati taratibu za mazingira, basi tutakuwa karibu zaidi, ili kuhakikisha kuwa wale wote wanaovunja taratibu, sheria zinachukua mkondo wake.

Vile vile tutazidisha nguvu zetu katika kupambana na wale wote ambao wanaovunja taratibu za kimazingira na sheria ipo wazi kabisa anayevunja taratibu za kimazingira hatua zichukuliwe.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake kwamba kabla ya kupata ruhusa ya ujenzi wowote wa hoteli kwanza lazima upate ruhusa ya mazingira. Kwa maana hiyo, kwa vyovyote vile tayari jambo hili limepewa nafasi kubwa kiserikali.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba atukubalie tuendelee na hoja yetu hii, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti hivi sasa ukitizama tayari tumeshakuwa na Waheshimiwa Wajumbe saba, nadhani kutakuwa na Wajumbe wengi kwa msingi huo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe atukubalie tuendelee na sisi kwa upande wetu serikali tutachukua kila hatua kwa wale wanaovunja taratibu za kimazingira, basi sheria ichukue nafasi yake na kabla ya kutoa hizi ruhusa za ujenzi wa hoteli, tutakuwa makini zaidi, ili kuhakikisha kuwa taratibu za kimazingira zinafuatwa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Mjumbe atukubalie, ili tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa najua kwamba unatumia busara tu, kwa sababu hoja zinakuwa na idadi yake. Mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iko chini ya Kamati yangu kitu kikubwa ninachoudhika kuendelea kuharibiwa mazingira kwa Zanzibar. Kwa hivyo, sitokubali Mjumbe mjumbe kutoka idara ya mazingira asiingizwe katika kamisheni Mhe. Mwenyekiti, japo kura moja mimi nitapiga ya kupinga kwa sababu ninasimamia taasisi

niliyokabidhiwa na nimeshaona mahala ambapo pana upenyo athari, watu wanapotumia *loop hole* ya kuharibiwa mazingira na hakuna hatua nyengine zinazoweza kuchukuliwa ni hapa hapa Mhe. Mwenyekiti nikiruhusu hapa ziara zangu zote nitakapokwenda nikiona kitu chochote kinafanyika kinyume na mazingira nitaambiwa wewe mwenyewe ulipokuwa pahala ambapo ulikuwa uongeze nuvu kwa uhifadhi wa mazingira hukufanya kazi yako.

Mhe. Mwenyekiti msinione tatizo naamini watu wa Idara ya Mazingira wote wananisikia na wataamini kwamba kweli kazi ninayoifanya sasa hivi ya kulinda na kuhifadhi mazingira. Hoja zimeshakuwa nyingi sasa kama tutakwenda kwenye kura sawa haidhuru nitakuwa peke yangu lakini nitapiga kura ya kupinga hapa mjumbe wa mazingira anaingizwa.

Mwenyekiti: Mhe. Waziri tunaomba utupe mtizamo wako na wewe sitaki twende kwenye kupiga kura isipokuwa nataka twende katika makubaliano, hivyo na wewe nakupa nafasi ya mwisho ili na wewe hasa sababu kuu ya kuwa huyu mjumbe mmoja akashindwa kukubali.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Utalii: Mimi nafikiri hii *investment* inapokuja kamisheni inakuwa ni mtu wa pili, ina maana ile *stage* ya mwanzo yote sisi hatupo, lakini zote tunazokuwemo ndio zimeshapitisha ule mradi baada ya kufanya *inspection* na kila sisi ni *stage* ya pili wanakuja tunaangalia *document* taasisi zote zimepitwa zinazohusika za mazingira ndio tunatoa leseni.
Sasa hata kwa mwendo huu kamishna wa mazingira mimi sioni chochote kwa sababu ni *stage* ya pili, kwa sababu mtu wa mazingira tumemshirikisha huku ndani ya kamati kwa sababu hii kamati inafanya kazi sambamba na kamisheni huku ya utalii kwa hivyo na wao wana *interest* zao za kutoa kwa sababu hizi hoteli hazijengwi mjini zinajengwa huko. Kwa hivyo kwenye hizo *comment* ndio unaona kila kitu kwa hivyo wao watatoa *import* zao kwa kamisheni, kwa hivyo nahisi *movement* zipo ndio maana tukasema utalii kwa wote ndio maana tukasema vile kwa sababu wao kule ndio wanaona mambo huku juu si aghalabu lakini huku chini ndio wanaona mambo.

Sasa wao wataleta *import* zao kwa kamisheni kuna hili na hili basi tunaweza kulisawazisha na tunaweza kusema sisi hatutoi leseni ya hoteli, kwa sababu kuna sharti hili na hili tunaona haliendi.

Kwa hivyo mimi nahisi Mhe. Hamza Hassan Juma tukubaliane kwamba *involvement* ipo kamati ile ambayo inafanya kazi sambamba na kamisheni, kwa sababu kamisheni nao wana *income* sawa sawa sio kwamba tunakwenda tu, mimi namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma hata tukimuingiza sisi ni *second stage* ya utekelezaji mwanzo inapita ZIPA ambako kule kote kuna zile taasisi ambazo zinahusika, kwa hivyo hata ukimuweka huyo wa mazingira mimi bado ni *second stage* inakuwa lazima apitishe tu kwa sababu imeshapitisha kule.

Mimi nafikiri sio jambo kubwa hebu tulitizame nafikiri kubwa ni kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kwa pamoja na mazingira, tuhakikishe kwamba mambo yetu wawe na uhakika nafikri tufanye hivyo. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi naona kwamba sasa itabidi tupige kura kwa wale ambao wanakubaliana na Mhe. Hamza kwamba mjumbe mmoja.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti nadhani kabla ya kufika huko tufike pahala tukubaliane kabla ya kufika kupiga kura, maana nahisi hili jambo si la kufikia pahala pa kupiga kura nimuombe tu Mhe. Hamza akubaliane na hoja ya kwamba mtu wa mazingira asihusishwe kwenye Kamisheni hii, nazungumza hili kwa msingi kwa sababu watu wa mazingira wanayo sheria kamili ya kuzuia na kuhifadhi mazingira eneo lolote wala wao hawahitaji kushirikishwa kwa sababu ni wajibu wao, kitendo cha kutaka kushirikishwa ni kutaka kukwepa wajibu wao wa kazi.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti hata kama tutawashirikisha kwenye kamisheni ya utalii basi kazi itakuwa ndio hiyo hiyo, sasa mimi nimuomba Mhe. Hamza Hassan akubali tusipige kura na hawa wajumbe kadiri ya kwamba wako wilayani basi wabakie wilayani, kwa sababu kamisheni ya utalii bahati tumefanya kazi pamoja na Mhe. Hamza kwenye kamati yetu ya Fedha na Uchumi suala la ujenzi la hoteli katika hatua ya mwanzo linakuwa kwa wenyewe watu wa ZIPA pamoja na watu wa ardhi na watu wa mazingira wenyewe, watu wa kamisheni ya utalii wao wanasimamia suala zima la biashara ya utalii na ku- *promote* utalii peke yake.

Kwa hivyo masuala ya uchafuzi wa mazingira yako kwenye taasisi hizi mbili, kwa hivyo hata kama mjumbe wa mazingira akipelekwa kwenye kamisheni ya utalii atakuwa hasaidii kitu ataongeza zogo tu, mimi ninaloliona ni

watu wa mazingira wanakwepa kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kwa sababu wao ndio wenye wajibu wa kuzuia mazingira wakati wowote wala hawahitaji kushirikishwa, wakati kamisheni ya utalii inapotaka kutoa leseni imetayarisha fomu ambayo inakwenda katika maeneo yote ikiwamo idara ya mazingira, lazima watu wa mazingira waweke maelezo yao kwenye ile fomu kabla ya yule mtu kupewa leseni na kamisheni ya utalii.

Kwa hivyo nimuombe sana Mwenzangu *back bencher* mwenzangu Mhe. Hamza Hassan tusifikie pahala pa kupiga kura tumkubalie Mhe. Waziri, kwamba huyu mtu asiingizwe kwenye ile kamisheni ya utalii na kwa sababu hoja ni kwamba watu wa mazingira wanatafuta njia ya kukwepa wajibu. Sisi tukamatane na watu wa mazingira tuhakikishe kwamba wanatekeleza wajibu wao wa kuhakikisha mazingira hayachafuliwi wao kwa kushirikiana na ZIPA pamoja na kushirikiana na watu wa Ardhi, kwa sababu wao ndio wenye majukumu ya kuhakikisha kwamba mazingira yanafuatwa.

Mimi Mhe. Mwenyekiti maombi yangu hayo tena nimuombe Mhe. Hamza tukubali kwamba mtu wa mazingira asiingizwe hapo ili tuwaachie wenzetu wa Kamisheni wafanye kazi yao yak u-*promote* utalii na mambo mengine, na wale wa mazingira tuhakikishe kwamba wanahifadhi mazingira wanazuia uchafuzi wa mazingira na kila kitu kinachohusika Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza naomba kidogo ukae muda umefika wa kuahirisha kikao kwa hivyo tuombe muda ili turudi tena ili tuendelee.

(Baraza lilirudia)

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda uliopo mbele yetu hauotoshi kumaliza shughuli iliyo mbele yetu kwa hivyo naomba kutoa hoja ya kutengua kanuni ya muda ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwanza nashukuru sana kwa busara zote zilizotolewa na ma-*backbencher* wenzangu, nakubaliana na kwamba tusiende kwenye kura. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kinapopitishwa kifungu hiki mimi nitoke nje halafu kikisha kupitishwa mimi nitarudi *(Makofi).*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, jana wakati na mimi nachangia kwa hisia kali sana nilieleza jinsi ya umuhimu wa hii kamisheni, nilieleza wazi kwamba ilitakiwa iwe makini na madhubuti sana katika kusimamia suala zima la utalii katika nchi yetu, kwani kumekuwa na uvunjifu wa sheria za nchi pamoja na viashirio vya kuhatarisha amani kwa mfano kama vile Nungwi tumeambiwa akina mama wananyang'anywa waume zao na baadhi ya wanawake kutoka Tanga jambo ambalo tunahisi linaweza kuhatarisha amani ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika muundo wa kamisheni kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu kamisheni mmoja awe ni kamishna wa jeshi la Polisi Zanzibar aingie kama mjumbe wa hii kamisheni, kusudi aweze ku- *switch on* ile *system* yake ya kushughulikia mambo ya uvunjaji wa amani hilo ni moja.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika kipengele hichi hichi cha tano taatu, mwenyekiti hatoweza kutolewa kuwa mwenyekiti mpaka awe na utaalam wa kipekee katika fani inayofanana na utalii, uongozi wa wadau wa utalii au uhusiano wa kimataifa. Kile kiwango cha taaluma yake kingetajwa hapa kwa sababu sisi zamani ilikuwa tuliposoma

hatukufahamu, lakini tulipojifunza tumejua. Sasa itajwe kwamba mwenyekiti awe na digirii ya mwanzo au kitajwe kiwango chake cha taaluma, sio itajwe tu awe na utaalam hilo la pili.

Halafu jengine nikasema kwenye kamisheni huku lazima kipengele cha 3.2 ujzi wa kutosha katika kupigania mambo ni kupigania mambo gani hii ni kuongeza maneno tu naomba kipengele hiki kiondoshwe Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Utalii: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu huyu polisi tumemshirikisha huyu katika kamati ya Wilaya yupo afisa wa polisi, na kuhusu haya mambo mbali mbali mambo yenyewe ni mambo ya kimataifa hatukusema mambo tu tumeeleza kule. Labda nilivyokuwa nasoma Mhe. Mjumbe hakusikia lakini tumeeleza hilo suala na tumelifafanua vizuri tu, kwa hivyo Mhe. Salehe hatukuliacha tumelifafanua vizuri tu.

Tumesema Afisa wa Mkuu wa polisi wa wilaya itakuwa yumo mwenyekiti wa masheha katika wilaya, mtu mmoja kutoka taasisi ya makumbusho ya mambo ya kale, mfanya biashara wa utalii katika wilaya, Mkulima katika wilaya na mtu mmoja kutoka jumuiya ya wafanya biashara ya utalii wilaya, afisa mmoja kutoka wizara ya ardhi, afisa mmoja kutoka mazingira, afisa wa kutoka jumuiya ya kiraia ndani ya wilaya, kiongozi wa kidini na tumesema vingozi wa dini kwa sababu kuna dini nyingi tuelewe hilo, Afisa mmoja kutoka mamlaka ya vitega uchumi, afisa utamaduni wilaya pamoja na DC mwenyewe hao ndio watakuwa wenye kamati hiyo.

Mhe. Saleh sasa sijui anataka zaidi aingizwe.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri anachokisema mjumbe ni kwamba kwenye kamisheni yeye kwa mawazo yake awekwe kamishna wa polisi kwenye kamisheni na sio kwenye wilaya ndio anachokisema yeye.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Utalii: Mhe. Mwenyekiti, kidogo naona hii itakuwa ngumu kumuweka Kamishna kuwemo kwa sababu ana majukumu yake, nafikiri ilikuwa inatosha kuwemo afisa wa polisi ndani ya wilaya kwa sababu anafanya kazi sambamba na kamishna. Kwa hivyo naona ushiriki upo tu wa polisi pale pale.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, OCD na Kamishna ni vitu viwili tofauti, katika maeneo yale wakati nachangia nilisema kwamba kuna udhalilishaji wa wananchi na akasema kwamba kuna ishuu za kimataifa, sasa uwezo wa OCD kushughulikia matatizo ya kimataifa kama alivyosema waziri ni mdogo ukilinganisha na Kamishna, mimi nadhani kamati ya wilaya haina nguvu ulinganisha na kamisheni yenyewe.

Sasa kwa mnasaba huu naendelea na msimamo wangu Mhe. Mwenyekiti kwamba ni vyema Kamishna wa Polisi wa Zanzibar akawa mjumbe wa Kamisheni ya Utalii, kusudi pale patakapotokea vitendo vya unyanyasaji na vinavyoashiria uharibifu wa amani kama alivyosema Mwakilishi kwamba kinamama walipigana kule na akinamama wa Tanga, basi yeye anaweza *swich on system* yake ya ulinzi na kuweza kudhibiti hivyo. Lakini OCD aliyekuweko Chake Chake hawezi kudhibiti vitendo vya Nungwi nadhani katika hili bado nasimamia kwamba Kamishna aendelee kuwa Mjumbe wa Kamisheni/

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo mazuri ya Mhe. Waziri nimshukuru tena Mhe. Saleh Nassor Juma kwa maelezo yake.

Mhe. Mwenyekiti serikali imeamua kupambana na vitendo vya uhalifu na imeamua kuimarisha ulinzi katika maeneo ya utalii, hivi sasa kuna mpango maalum wa kuanzisha *Tourism Police* msingi wake ni kupambana na vitendo vyote vya uhalifu kwa watalii, kwa sababu kamishna wa Polisi ana dhamana kubwa ya kupambana na uhalifu na atakuwa anaongoza operesheni mbali mbali za mambo ya uhalifu. Kwa hivyo ikiwa kila sekta tutaiweka katika muundo wa Kamisheni ya Utalii na kwa sababu Kamisheni ya Utalii ni *cross cut issue* itakuwa sekta nyingi ziwemo humu.

Mimi ninachokiomba kumuomba Mhe. Saleh Nassor Juma akubali kwamba tuzidishe juhudi zetu katika kupambana na vitendo vya uhalifu katika kupambana na vitendo vya unyanyasaji, haya anayoyasema nataka nimhakikishie kwamba serikali imeyapokea na itazidi kuyafanyia kazi. Lakini namuomba atukubalie kwamba idadi hii ya Kamishna inatosha tunachokitaka hapa ni wa tu watakaotusaidia katika kuimarisha utalii wenyewe, pia watakaotoa maelekezo mbali mbali ya kufanya shughuli za utalii ziende vizuri, naamini kamishna wa Polisi tunakuwa nae mara nyingi katika mapambano haya ya hualifu hasa katika maeneo haya ya utalii.

Namuomba sana Mhe. Salehe Nassor Juma atukubalie tuendelee na shughuli hizi na nimuhakikishie kwamba tutachukua kila jitihada kupambana na uhalifu hasa wahalifu wanaosumbua sekta yetu hii ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Saleh vipi tuendelee umeridhika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo ya na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Utalii Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambae pia ni mpiga kura wa Jimbo la Wawi jimbo langu, natumai nitumie fursa hii kusema tuendelee.

Mhe. Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimuomba Mhe. Waziri kwa kuwa aweke *Zanzibar Tourism Investor* lakini akasahau na Mhe. Ismail Jussa Ladhu akamkumbusha nashukuru.

Lakini katika sheria ya kiingereza hawa aliwaita *hospitalism Industry* lakini hawa *association Travel tower operator* kawataja kwa jina, kwenye kamati tutamuingiza hawa nani na hawa nani, akasema hawa watakuwa jamaa wa VAT hiki ni chombo ambacho *investors* wote Tanzania, Zanzibar *Association of Tourism Investes*, hawa *two operates* nikamwambia Mhe. Waziri madhali mmeshaweka hawa shughuli zao japo kuna baadhi ya watu *boar members* huko lakini haya mambo tumeshayasaini sio mambo ya ushindani, nimeeleza historia ya utalii tangu tumeanza tangu 1967 tunafungua mpaka tumekuwa sasa tumefikia pahala mambo ya kutafuta watu rafiki zako, ndugu zako kuweka weka hatufiki.

Tutengeneze vyombo ambavyo vitapromoti utalii na utalii sasa hivi imeelezwa kwamba ni 80% nimeeleza hapa Dk. Mwinyi Haji Kaniunga mkono, sasa mimi nikasema kwa nini *duplication* ndio mimi nikatoa wazo. Uzuri awekwe polisi sio Kamishna wa polisi kwa sababu sasa hivi kuna utaratibu ambao serikali inaendeleza sasa hivi kwa kuwa hali ni mbaya, nasema katika mbuga kuna askari wa mbuga lakini hapa kwetu malalamiko mengi sana na Mhe. Mohammed Aboud akiwa waziri wa Wizara hii zamani anajua, hivi karibuni yaliyotokea anajua.

Sasa hivi serikali yenyewe inafikiria kwa sababu polisi ni muungano serikali inafikiria sasa kutafuta fedha kuongezea kwa polisi za kuanzisha chombo hichi. Sasa katika hii hili sio *district* hichi ni chombo kikubwa sana ndio *Policy Maker* sasa akiwepo watu wengine hawa basi muondoshe mmoja, ukiweka polisi humuweki kamishna wa polisi.

Baraza la Mapinduzi la Mwanzo limesema Kamishna wa Polisi halijasema Edington Kisasi wengine wote wametajwa kwa majina, lakini kamishna wa polisi hakutajwa kwa jina wajumbe 31 wa Baraza la Mapinduzi AG yule pale kama nasema uwongo kesho nisutwe, yule katajwa Kamishna wa Polisi sisi wengine wote kwa majina Ramadhani Haji, Kaujore lakini kamishna wa polisi hatuwezi kumleta. Sasa katika hali hii ya sasa hivi ya kutaka kuwapa moyo hawa *investors* juu ya malalamiko yaliyoko ipo haja tusifanye ushindani. Ramadhan Abdalla Shaaban alikuwa sio mkaidi haina haja ya kushindana sana mambo mengine haisaidii tusishindane sote ni wamoja, hakuna mbabe tutizame mambo ipo haja.

Lakini jengine sasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu ametaka aongezwe mtu wa dini, Mhe. Hamza ametaka aongezwe mtu wa *environment*, Mhe. Shadya anasema watu sita sijui Mhe. Waziri amenikubalia mimi na Mhe. Jussa Ladhu kwa kuwa nimekubali sijui atamtoa nani, kwa sababu sheria inasema watu sita japokuwa mtendaji anaingia yule. Lakini Waziri anachagua watu sita yote yameelezwa hayo na ameshakubali mwengine atiwe huyu wa mambo ya dini sasa sijui atamtoa nani, sasa hapa yupo mtu wa polisi lakini hata watu wa ZIPA wapo kule vile vile huku wapo na kule wapo na ukitizama haya mambo si mapya hata ukitizama hii sheria ya 1991 hii bodi inazungumza kuwa itakuwa na *Chairman member* wake *commission of land and environment, local Government.*

Mhe. Mwenyekiti: Kuna taarifa tu kidogo Mhe. Waziri wa katiba na Sheria kidogo alikuwa anataka kusaidia kwa hili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate muongozo wako, kwa mujibu wa utaratibu wetu ni kwamba kama suala limeshazungumzwa na limeshakubaliwa. Suala hili la Kamishna wa Polisi alilitoa Mhe. Saleh Nassor Juma na yeye mwenyewe kakubali. Kwa hivyo lile haruhusiwi mtu mwengine kulizungumza kwa sababu limeshakubalika la kwanza. Pili mtu anayetoa hoja hachangii, anakwenda dakika mbili anazungumza halafu anatoa ile hoja yake. Lakini sasa tunasikiliza hotuba nyengine ya kuchangia. Hivyo sivyo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Mzee naomba utoe hoja kama kuna hoja ambayo unayotaka kuitoa naomba uitoe.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimechangia kuhusu *policy*, labda Mhe. Abubakar Khamis Bakar alikuwa kidogo anasinzia. Ulikuwa mjadala unakwenda na mimi nangojea umalizike, kwa sababu na mimi nilichangia na sio kwamba nimerukia hoja. Nimechangia na nilieleza na hansard ipo, nilitaja *tourism policy.* Lakini kwa heshma na taadhima lile jengine anambie nani anamfuta katika wale. Mimi sipendi kubishana na Mhe. Abubakar Khamis Bakari, namuheshimu sana.

Nilipokuwa nashindana nae, anajua ushindani wangu kuwa mimi siwezi kushindana naye, namuheshimu japo kuwa ni mdogo wangu. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri anambie katika hili nani atamfuta katika ile hoja ya Mhe. Ismail Jussa wale, asiweke huyo Kamishna wa polisi, asiweke nani lakini maelezo haya tumetoa nataka nijue atamfuta nani kwa sababu sheria sita.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Mzee hili tulikuwa tayari tumeshalizungumza na limeshapita. Mhe. Waziri alilitolea ufafanuzi akasema kwamba hili wamelikubali. Lilikuwa ni suala la Mhe. Ismail Jussa, aliomba kwamba waingizwe ZAT pamoja na ZATU na Baraza limeliridhia tahari. Kwa hivyo naomba tuendelee kwa hilo.

Kifungu cha 5 Kufutwa na Kuweka Kifungu cha 5 Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 6

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu na katika michango ya wajumbe wengi sana waliochangia, tulipendekeza kwamba hichi kifungu cha 6 ambacho kinaweka kifungu kipya cha 6 katika sheria. Pamoja na kwamba kinatamka *expressly* kwamba mwenyekiti hatokuwa mtendaji. Lakini tukasema kwa hivi alivyowekwa na kazi zake na halafu baadaye ukikisoma kijifungu cha 4 cha kijifungu hichi ambacho kinampa mshahara, kinatoa nafasi ya kuweza kuja kutokezea mgongano baina yake na Katibu Mtendaji.

Bado hata kama tunasema sio Mwenyekiti Mtendaji inaweza ikatafsirika hivyo. Kwa hivyo tumependekeza kwamba haya majukumu ambayo kijumla yalipaswa yawe ya Kamishna kwa ujumla wake yaliyootajwa kwa Mwenyekiti, yakahamishiwa katika kazi za Kamishna na Mwenyekikti akabakishiwa zile kazi *ceremonial* tu.

Kwa mfano kifungu kilichokuwemo kwenye (b), (d) na (f) na vile vile yale mengine yakabakia katika kazi za Makamishna kwa ujumla wao kama Kamisheni. Vile vile kile kifungu kidogo cha 4 ya ule mshahara ikaondoka ikawa kama inavyokuwa kwa wenye viti, wengine wote. Kwamba mwenyekiti huyu atapata mafao na posho kama itakavyoamuliwa na waziri kama vilivyokuwa vyombo vyengine, ili kuweka *precedent* ya kuwa na mwenyekiti wa aina nyengine. Nikaona hili katika majumuisho yaliyofanywa na Mhe. Waziri hakuligusia nilikuwa naomba atupe ufafanuzi na nini *position* yake katika suala hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, na waheshimiwa wajumbe, kwa kweli tumesema kwamba mwenyekiti, kwamba si mtendaji, yeye atakuwa ni msimamizi mkuu wa ile Kamisheni ni kama waziri. Waziri anakuwa ni msimamizi wa ile wizara nzima lakini si mtendaji. Kwa hivyo ndio tukasema hapa na mwenyekiti muache abakie vile vile kama ni mwanasiasa au ni msimamizi wa ile Kamisheni kama vile waziri kwenye wizara, Mtendaji Mkuu ni Katibu Mkuu, Waziri ni msimamizi wa zile sera na mipango na vile vile kutoa fikra, namna gani twende na kupata ripoti.

Nafikiri hakuna ubaya kumuachia mwenyekiti majukumu haya kama ulivyosema kuwa mbele katika kuanzisha dhana na kuendeleza utalii, kwa mfano kutoa maelekezo katika kuendeleza. Nafikiri ni kutoa maelekezo tu lakini mtekelezaji ni Katibu Mkuu, hata waziri anatoa maelekezo katika wizara, lakini mtekelezaji ni Katibu mimi sio mtekelezaji na ndio tumeona kwa njia hiyo. Kwa hivyo Mhe. Ismail Jussa unaweza kukubaliana mimi, nafikiri tungeacha hivyo kama tulivyosema kwamba si mtendaji huyu ni msimamizi mkuu wa ile kamisheni, mtendaji ni katibu mtendaji.

Suala la mafao nalo tumeona kwasababu mwenyekiti atakuwa ni *full time* kwa hivyo itakuwa si vyema kwamba mtu anafanya kazi wakati wote halafu asipata mafao nafikiri itakuwa kidogo ni kinyume na sheria ya utumishi. Tukaona kwamba ni lazima apate mapae mafao kwa sababu ni mtumwa huyu kwa sababu *full time* sio kwamba *part time* ingekuwa wa muda ni suala jengine. Na kwa sababu ya uzito wa kazi yetu tukasema ni lazima afanye kazi full time ili kuhakikisha kwamba malengo yanafikiwa ya utalii kwa wote.

Nafikiri Mhe. Ismail Jussa atakubaliana na mimi wala hazitoletwa mgongano kiasi hicho unavyofikiria. Kwa sababu yameelezwa wazi ya katibu mtendaji yameelezwa na ya mwenyekiti, yameelezwa yeye ni msimamizi mkuu tu. Kwa madamu sio mzee anayo haki ya kutoa fikra. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, majibu ya Mhe. Waziri yamenichanganya zaidi na pengine yanatilia nguvu hoja yetu wajumbe. Kwa sababu tukisema kwamba huyo atakuwa kama Waziri pale waziri si mtendaji ni dhana tofauti kabisa hapa. Lakini zaidi tulisema kwamba hoja yetu ya msingi au nisema hoja yangu. Kwamba vyombo kama hivi kwa kawaida, mwenyekiti anaongoza vikao na anatoa uongozi wa jumla kwa kile chombo. Vile vile hapa kaongezewa jukumu la kusimamia mkutano wa Kamisheni na wadau.

Lakini ukisoma kifungu cha 6, ukisoma kiundani hizi kazi ambazo kapewa mwenyekiti na ukisoma kazi za makamishna ambazo zipo kifungu cha 7 kwa ujumla wake. Kuna mambo yanaingiliana sana na ndio ukaona kwamba mwenyekiti huyu hanatofauti sana na Makamishna wengine Mhe. Mwenyekiti, lakini tumetaka kumpa nafasi ya ziada.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokihofia mimi kwamba kutakuwa na mgongano lakini tulipokuwa tukichangia tumesema hapa, Kamisheni hii hii hata tusende katika vyombo vyengine umeshatokezea mgongano baina ya mwenyekiti na katibu mtendaji, hatutaki kutaja majina hapa Mkurugenzi mtendaji kwa wakati ule.

Kwa hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti nadhani hili tukubali kwamba tusifanye chombo hichi kikawa tofauti na vyombo vyengine vyovyote kwamba kutakuwa na katibu *over role in charge* wa *policy* katika utalii, atabakia kuwa Waziri wa Utalii kama ilivyokuwa katika sekta nyengine yoyote.

Chombo hichi kwa masuala ya kusimamia utendaji, tubakishe kwamba ni katibu mtendaji na makamishna pamoja na mwenyekiti wao tuwataje kama ni kamishna, ambao watakuwa na majukumu ya kusimamia *policy* ile. Huyu Mwenyekiti tumtaje kama tulivyopendekeza katika michango yetu abakie na jukumu la jumla la kuiongoza kamisheni na atakuwa kama ni mtu wa *public relations*, lakini tusimpe madaraka ambayo yatakayomuonesha katika mtendaji kama watakuja ku- *invites* ushindani baina yao.

Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo huo naomba tena kurejea kwamba kijifungu cha 4 kile kinachohusu mshahara kiondoke abakie kama mwenyekiti mwengine wa vyombo vyengine vyombo kwamba atalipwa posho na mafao kama waziri atakavyoona inafaa na sio kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma. Namba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tumesikia hoja ya Mhe. Waziri kwa nini kifungu hichi kimewekwa kwenye Mswada, dhamira yake. Yaani dhamira na mwenyekiti alivyowekwa na sio tu imewekwa kifungu kimoja lakini kuna na kifungu chengine kinachoeleza kazi zake na masuala mengine yanayohusiana na kazi zake. Sasa nadhani anachokieleza Mhe. Ismail Jussa mapendekezo ambayo anapendekeza. Mimi hadhani anabadili dhamira ya msingi ya mwenyekiti kuwepo katika kamisheni.

Yeye anacho -*challenge* kwamba labda kutakuwa na mgongano au hatofanya kazi hizo ambazo anatakiwa. Lakini nadhani waziri kaeleza dhamira ya kuwepo kwa mwenyekiti. mapendekezo anayopendekeza Mhe. Ismail Jussa nadhani yanakwenda kinyume na dhamira ile ya mleta Mswada mleta hoja hii ameyakusudia katika Mswada. Sasa nadhani kwa sababu hiyo na ni kwa sababu hayo ni marekebisho ya msingi yanahusu zaidi ya kifungu kimoja na kuuondoa kama alivyopendekeza mwenyewe Mhe. Ismail Jussa kwamba tuondoe labda kifungu hichi kichanganywe na kifungu chengine. Mimi dhani marekebisho hayo yalipaswa yafate Kanuni ya 83 kanuni ndogo ya 13(b).

Sasa kama hakufata utaratibu huo mimi nadhani hatuwezi kuyajadili katika steji hii ya kamati ni kinyume na utaratibu nadhani.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa kutokana na maelekezo ya Mwanasheria Mkuu kwamba dhana yako au hoja yako inabadilisha dhamira ya sheria hii kwa hiyo anakuomba kwamba hicho hakiwezekani. Taarifa ilikuwa iende mapema kabla ya kupitishwa kwa sheria hii.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Mwanasheria Mkuu lakini mimi kimsingi ninatofautiana naye. Nadhani kama kasikiliza katika maelezo yangu nilisema kwamba kiini, roho ya kazi za mwenyekiti pia zimetolewa katika kifungu cha 7 kwa makamishna kama chombo kwa ujumla. Labda nifahamike nitoe mfano si kama inabadilisha dhamiri ya Mswada kama anavyotaka Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba Baraza hili liamini. Naomba nitoe mfano ukisoma (a) kwenye mwenyekiti, inazungumzia kutoa maelekezo ya mikakati kwa uongozi katika kuendeleza na kukuza biashara ya utalii.

Ukisoma kwenye makamishna kwa jumla (a) inasema kuwa washauri wakuu wa serikali na uongozi wa Kamisheni kwa mambo yote yanayohusiana na maendeleo, taratibu kukuza na kuendeleza biashara ya utalii na huduma zinazoendana na utalii, zinafanana kabisa ni maneno tu.
Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia katika kifungu cha (d) kuwa mbele katika kuonesha dhana ya utalii kwa wote. Ukisoma kwenye makamishna katika (c) inazungumzia kusimamia uendelezaji na utekelezaji wa dhana ya utalii kwa wote. Ukiangalia katika (c) kusimamia, utekelezaji wa sera ya utalii na kutoa miongozo kwa uongozi juu ya utekelezaji wa sera hiyo. Ukisoma huku kwenye makamishna katika (d) kuna kutoa miongozo ya jumla kwa uongozi wa kamisheni kwa wadau wa utalii. Kwa hivyo vitu hivi Mheshimiwa kuna maneno mengi tu yanafanana sana ndio maana nikasema kwamba bado unaweza ukayaondoa bila ya kuharibu msingi wa Miswada ukabakisha yale machache ambayo mwenyekiti kama kawaida katika nafasi nyengine zote anakuwa nazo.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyengine unatumika utaratibu wa kutaka kuyafanya mambo kama ni mazito au makubwa sana ili kukwamisha juhudi zifanye kazi yake ya kutunga sheria. Lakini nadhani kimsingi hakibadilishi kifungu alichonambia Mwanasheria Mkuu nilikuwa nakijua na nilikuwa nafikiria, lakini nilipoona hakibadilishi dhana ya Mswada sikuona haja ya kuleta marekebisho hayo niliyosema niyalete.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachozungumzia kuhusu dhamira, anaweza kudhani kwamba maneno yanafanana. Ukisoma ni kweli maneno yanaweza kufanana . lakini ninachosema dhamira ya Mswada, dhamira ya kuwepo Mwenyekiti, kwa nafasi na hadhi waliyopewa cha msingi ni kuwa na mtu kutokana na umuhimu wa sekta ya utalii, kuwe na mtu ambaye amepewa sifa. Maana yake na sifa zimetajwa, maana hata zile sifa pengine zinakuwa sio za msingi sana zilizowekwa katika kile kifungu.

Lakini dhamira ya msingi ni kwamba kuwa na mtu wa kudumu ambaye atasimamia yale ambayo makamishna wanayasimamia pia kuhakikisha kwamba yanatekelezwa. Hiyo ndio dhamira kubwa, kuliko kwamba una watu wanakuja siku pengine watayopata nafasi wanakuja, wanaondoka lakini mtu ambaye *permanent* atakuwepo kama ni *advocate* kufanya kazi katika yale mambo ya msingi ya kusimamia sekta ya utalii, hawa wengine watendaji ni kuendesha tu ile taasisi kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ile *structure* yenyewe ilivyokusudiwa iwe namna hiyo kwa madhumuni yake, ina dhamira yake katika kuendeleza hii sekta ya utalii. Sasa leu ukisema unamuondoa maana yake unaondoa ile dhamira yamsingi na serikali baada ya kuifanyia utafiti kuona kwa utaratibu huo ndio tunavyoweza tukenda. Ndio maana nasema kwamba kama hili lilikuwa anaona libadilishwe, bila shaka kubadilisha hicho kitabadilisha na vifungu vyengine na pengine ingeipelekea serikali kufikiria hata hizo sifa kama ni mtu wa kuja na kuondoka huhitaji sifa zote hizi ambazo zimewekwa. Kwa hivyo hoja hiyo inabadili na vifungu vyengine. Mimi nasema kama ni hiyo ilikuwa ije kwa maandishi kama kanuni zinavyosema, inawezekana ina msingi. Lakini ninachosema kwa kufanya hivyo inabadili dhamira na ya ile structure yenyewe iliyokusudiwa na serikali. Yeye anataka kuwa na *structure* ambayo nahisi itakuwa hai *deal* lakini dhamira ya serikali kuwa na *structure* hii inaona ni e-*deal* zaidi.

Mimi nilifikiria kwasababu hiyo kubadilisha itakuwa inabadilisha ile dhamira yenyewe au misingi ya serikali yakuweka *structure* ya namna hiyo katika Kamisheni ya Utalii. Hiyo ilipaswa ifate Kanuni ya 83 kanuni ndogo ya 13(a) na (b) ambalo halikufanyika. Kwa hivyo nadhani kwa hoja hii kwa hapa hatuwezi kuijadili ni kinyume na utaratibu na ni kinyume na kanuni.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema mimi kwa maoni yangu sioni kama hilo linabadilisha msingi wa Mswada. Mhe. Mwanasheria Mkuu anasema kwamba tukifanya mabadiliko haya itabadilisha na vifungu vyengine vyote.

Mimi kama ningesema tuondoe kabisa Mwenyekiti, nadhani ni kweli ingebadilisha vifungu vyengine vya Mswada. Ndio maana sikusimama katika kifungu cha 5 katika suala la mwenyekiti kwa sababu kimsingi nakubali awepo

mwenyekiti na hapa nimesema haya baadhi ya mambo ambayo yametakiwa yawepo ambayo kikawaida anakuwa nayo mwenyekiti bado yaendelee kuwepo lakini nasema haya mengine ambayo yanajirejea katika makamishna na labda katika kutaka nifahamike Mhe. Mwenyekiti, naomba hata tukikisoma kijifungu kinachopendekeza cha Mswada huu cha 7(2) ambachi kipoa kipo ukurasa wa 44 kifungu kimesema

> "Uwezo wa kamisheni uliioueleza chini ya sheria hii, isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo utatekelezwa kwa makubaliano ya makamishna kupitia vikao vitakavyoitishwa kwa mujibu wa taratibu zao"

Kwa hivyo haya maamuzi kimsingi yaliyotajwa haya ni ya Kamisheni kwa pamoja Mhe. Mwenyekiti na kama suala la kusimamia baada ya hapo kama unavyotwambia ndio hapo ninavyopata wasi wasi. Kwa sababu huku anatwambia mwenyekiti atakuwa si mtendaji, huku anatwambia atakuwepo kila siku. Sasa mwenyekiti akishakuwepo kila siku itakuwaje mwenyekiti huyu halafu asiwe mtendaji, haiingii akilishi.

Nadhani tumesha *ague* sana na hili ni suala la msingi tofauti na lile la mwanzo. Kama serikali inaona kwamba ni jambo la msingi basi tuliache ipigwe kura. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nieleze mambo mawili madogo. Hii tusishindane tu kwa sababu ya kushindana lakini tutizame. Maana yake mjumbe anaposema mwenyekiti atakuwa si mtendaji halafu anakuwepo *full time* na akasema hailete *sense*, mimi simfahamu. Nina hakika Mheshimiwa Mjumbe anajua kwamba duniani na ulimwenguni kwamba kuna watu ambao si watendaji na wanakuwa ndio wakubwa kwa mfano. Kuna Rais ambao sio watendaji, halafu kuna Waziri Mkuu, ambaye ndiye mtendaji, kuna *queen* kule si mtendaji, kuna Waziri Mkuu ni mtendaji na ho ni *full time* na wanalipwa na wanapata kila kitu. Hawa ni chombo ambacho kinaongoza na kina – *direct* baadhi ya mambo.

Mhe. Mwenyekiti, unaposema kwamba huyu si mtendaji na anakuwa *full time* ni sawa, lengo letu au lengo la serikali ni kuonesha kwamba huyu anaelekeza na kuelekeza kwake kwa sababu ile *policy* ya utalii inayotaka kwenda ni kwamba lazima awepo kwa muda wote. Ndio nikasema huyu basi atakuwa si mtendaji lakini ana *advocate* mambo kuwaelekeza wale wengine. Sasa *the very fact* yeye anakuwepo *full time* wakati wote hata kama si mtendaji anaelekeza huyu ni binaadam anataka kula, anataka kuhudumia mambo yake nyumbani ni lazima alipwe mshahara, alipwe maposho yake kwa utaratibu huu, hawezi kukaa mtu siku zote ikawa halipwi, hata huyo Rais aliyekuwa si mtendaji lakini analipwa kila kitu. Hiyo ni moja Mhe. Mwenyekiti, naomba tutizame.

La pili Mhe. Mjumbe anajua yeye alikuwa Mbunge miezi kidogo tu, mtu yeyote anapotaka kubadilisha hata ile "a" katika Mswada anapeleka *showdown of amendment* mwanzo anasema mimi nina azma ya kulepelaka *showdown* amayo kwa mfano itapunguza hizi kazi alizopewa mwenyekiti katika kifungu cha sita ili ziwekwe katika kazi ambazo amepewa mjumbe. Anachosema Mwanasheria Mkuu ni kwamba hicho Mjumbe hakufanya na kwa sababu hakufanya tunafungika na Katiba Mhe. Mwenyekiti.

Kanuni za Baraza kifungu cha 83(2) kama alivyosema Mwanasheria Mkuu kinasema kwamba mtu kama hakuleta *showdown of amendment* kwa hivyo hawezi tena ku – *raise issue* katika *stage* hii. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti amefungika na hayo maelezo yake angelipeleka *showdown of amendment* hapo mwanzo basi angelisikilizwa hapo kwa sababu hii ndio *stage* ya kusikiliza ile *showdown of amendment* tunafungika na kanuni hizi. Mhe. Mwenyekiti naomba tuende kwa mijibu wa kanuni kama wajumbe wengine wote siku zote wanavyosema. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri mimi nafikiria kwa kauli yake Mhe. Ismail Jussa aliyoitoa ya mwisha ni kwamba alituruhusu tuendelee.
Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sikuruhusu tuendelee, nilisema kama ikiwa kwa kuepusha mjadala huu nilisema Kamati ya Baraza ya Kutunga Sheria ifanye kazi yake, nilitoa hoja hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa Ladhu kinavyosomeka hiki kifungu hapa hakuna haja ya kupiga kura. Hoja aliyoitoa Mwanasheria Mkuu ni kuwa ulete maombi ya kufanya *amendment*. Kwa hivyo hapa hakuna haja ya kupiga kura isipokuwa ulete hoja yako kiutaratibu, kisheria.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sijui tunakwendaje, lakini niseme alivyokuwa amesema mwanasheria mkuu mara ya mwanzo, kanuni ya 83 na naomba kwa faida ya sote. Kanuni ya 83 fasili ya 13 inasema hivi:

“Endapo wakati wa mjadala mjumbe anakusudia kupendekeza marekebisho kwenye Mswada unaojadiliwa.

(a) Ikiwa marekebisho hayo ni madogo na hayabadilishi dhamira halisi ya kifungu hicho au Mswada wenyewe anaweza kueleza mapandekezo yake wakati akichangia.

(b) Ikiwa mapendekezo hayo ni makubwa kiasi ambacho inabadilisha dhamira iliyokusudiwa atapeleka mapandekezo yake kwa katibu kabla ya mjumbe huyo hajaanza kutoa mchango wake kwenye Baraza na Katibu anaweza kuyagawa mapendekezo hayo kwa wajumbe wote, isipokuwa…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa haya ambayo tunataka kuyafanyia marekebisho ukubali kwamba ni makubwa. Kwahiyo tuendelee tutakuja kuwayafanyia marekebisho baadaye.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakiheshimu kiti chako, lakini nasema jana tu hapa tulipitisha Mswada kwa utaratibu kama huu na Spika, alikuwa akiongoza kikao hichi, lakini kiti ni chako nitaheshimu maamuzi yako.

Kifungu cha 6	Kufuta na Kuweka Kifungu cha 6 Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 7	Kufutwa na Kuandikwa Upya Kifungu cha 7 Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 8	Kufutwa na Kuandikwa Upya Kifungu cha 8.
Kifungu cha 9	Kufutwa na Kuandikwa Upya Kifungu cha 9 Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 10	Kuengezwa kwa Kifungu Kipya cha 9(a).
Kifungu cha 11	Marekebisho ya Kifungu cha 10 Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 12	Kufutwa na Kuandikwa Upya Kifungu cha 11.
Kifungu cha 13	Kuongezwa kwa Kifungu Kipya cha 11(a)
Kifungu cha 14	Marekebisho ya Kifungu cha 12 Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 15	Kufutwa kwa Kifungu cha 13.
Kifungu cha 16	Marekebisho ya Kifungu cha 14.
Kifungu cha 17	Marekebisho ya Kifungu cha 15.
Kifungu cha 18	Marekebisho ya Kifungu cha 16
Kifungu cha 19	Marekebisho ya Kifungu cha 17
Kifungu cha 20	Marekebisho ya Kifungu cha 18
Kifungu cha 21	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia niliomba ufafanuzi kuhusiana na kifungu hichi, sikumsikia Mhe. Waziri wakati akifanya majumuisho yake, alisema kifungu hiki ambacho kinaingiza kifungu kipya cha 19 A(1) “kinasema mtu aliyeruhusiwa kufanya biashara ya utalii hatofanya mabadiliko katika ofisi yake au jengo wana hisa au wakurugenzi, jina la biashara au huduma wanayoitoa paka wawasilishe kwa kamisheni maelezo, mapendekezo, mabadiliko au marekebisho yaliyokusudiwa kwa maandishi.

Nitataka ufafanuzi kwamba haya mambo yaliyotajwa hapa kwa mfano katika mabadiliko ya majengo ya ofisi sidhani kama inahusika Wizara ya Majenzi lakini zaidi nilielekeza hoja yangu katika suala la wanahisa, wakurugenzi, nilidhani kwamba nasuala haya, wanaohusika ni wale wanaofanya ya kusajili makampuni ambayo ni Ofisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali. Nikataka kujua kwamba inaingiaji katika Kamisheni. Nilikuwa naomba maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nilitoa maelezo kuhusiana na kifungu hiki ni kwamba mtu aliyeruhusiwa kufanya biashara ya utalii hatofanya mabadiliko katika ofisi yake au jengo au hisa, wakurugenzi, jina la biashara. Mhe. Mwenyekiti, tumesema Kamisheni inahitaji taarifa ya maandishi kuliko kuleta taarifa ya mdomo kwa sababu tumepata kesi nyingi kama hizo pengine wamedhulumiana halafu wanakuja kulalamika lakini baada ya kuharibika lile jambo. Kwa hivyo, atakapoleta ile taarifa ya awali kimaandishi tutakuwa tuna kumbukumbu ya kufuatia lile suala lake na hizo zimekuja nyingi tu ambazo hatuna kumbukumbu nazo, ndio tukasema lazima tuletewe hii taarifa kimaandishi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri hakunielewa suala langu hivyo namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu anisaidia katika hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Jussa atakubaliana na mimi kwamba hakika utaratibu wa usimamizi wa sheria unakuwa na *registration* lakini na pia kunakuwa na *regulator*. Kwa mfano, katika usajili wa usimamizi wa taasisi za fedha unapotaka kubadilisha mfano wakurugenzi na wakati mwengine hata *shareholders* ni lazima kwanza upate kibali cha Benki Kuu. Hii ni kwa sababu ya kulinda na kuhakikisha kwamba wale ambao wanaruhusiwa kuanzisha *financial institution* wana *integrate* fulani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya utalii uzoefu ambao umetokea ni kwamba anakuja anasajili mtu au anaanzisha kampuni ya utalii baadae unakuja linapotokezea tatizo unakuja kumtafuta *the original owner* kumbe na yeye ameshauza zamani. Mhe. Mwenyekiti, pia wakati mwengine mnajikuta mna mtu ambaye yuko katika sekta hii ambaye hana *integrate* na ana matatizo wakati mwengine ya ki-*security*, ana matatizo pengine huko alikotoka alishafanya mambo mengine na unaona kwamba wakati ule tunapoanzisha kunakuwa na *regulation* na vitu mbali mbali vya kuhakikisha kwamba unapata watu ambao wana *integrate* katika kufanyakazi.

Kwa hivyo, haya madhumuni yake sio kwamba wao ndio wanao-*regulate* hizo sekta, lakini vyote madhumuni yake ni kuhakikisha kwamba yale mabadiliko yanajuulikana ili kuhakikisha kwamba huyu anayeingia, huyu anayetoka basi ana int*e*grate ambayo inakubalika na hili ni jambo la kawaida katika sekta ambazo wenyewe katika nchi tumezichukulia kwamba ni *sensitive* ili kuwajua watu wenu ambao wana *operate* katika sekta hii. Hayo ndio madhumuni yake kwa kweli.

Mhe. Ismail Jussa Ladh: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu na nimeridhika naomba tuendelee.

Kifungu cha 21-	Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 19a pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 22-	Kuongezwa kwa vifungu vipya vya 23a na 23b

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu niligusia katika vifungu vipya vilivyoongezwa kwenye 23b (1c) nilichangia katika hii kuanzisha mfuko wa fedha wa wananchi kwa njia ya michango ya hiari ambazo zitatumika kwa maendeleo ya vijiji. Nikapendekeza kwamba hii michango isiwe ya hiari, na nikasema katika utaratibu unaojengeka katika dunia ya sasa wale watu ambao wananufaika na eneo fulani kwa mfano wenzetu wenye maadini huwa wanatoa asilimia fulani ya mapato yao kuendeleza maeneo yale. Kwa hivyo, Mhe. Waziri alipokuwa anajibu amelijibu lakini amelijibu zaidi kwa sababu kuna wajumbe wengine walichangia kwamba walidhani michango ni ya wananchi. Mhe. Mwenyekiti, mimi sikulizungumzia hivyo nilizungumzia upande wa pili, nilizungumza kwamba hawa wawekezaji badala ya kuambiwa wachangie maendeleo ya maeneo yale kwa michango ya hiari kuwe kuna asilimia angalau tatu ya mapato yao yatumike katika kusaidia maendeleo ya yale maeneo ambayo wameekeza katika sekta ya utalii. Nilikua naomba ufafanuzi wa hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo ya Mhe. Jussa tutafanya hivyo kwamba asilimia 10 itoke kwa makampuni hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea.

Kifungu cha 22 - Kuongezwa kwa vifungu vipya vya 23a

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwwenyekiti, tunatunga sheria na ni makosa kuja kuweka rekodi mbaya Mhe. Waziri ametaja asilimia 10, asilimia 10 ni kubwa sana mimi hata siwezi kupendekeza hivyo, nilivyopendekeza asilimia 3 ya mapato yao yatumike katika maeneo yale. Naomba hilo likae katika rekodi vizuri tunapopitisha hivi vifungu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa maelezo yake mazuri, lakini pia nimshukuru Mhe. Jussa kwa ushauri wake huu muhimu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuomba Mhe. Jussa na Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane kwamba asilimia 3 katika mapato ni makubwa sana ya mwekezaji na inaweza kuzua tatizo kubwa sana katika sekta yetu hii ya utalii. Kwa hivyo, naomba tukubaliane tuweke angalau asilimia 1, asilimia 3 bado ni kubwa sana.

Mhe. Ismail Jusssa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimemkubalia Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, naomba tuendelee.

Kifungu cha 22- Kuongezwa kwa vifungu vipya vya 23a na 23b pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 23 -

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia na bahati nzuri katika hili niliungwa mkono na wajumbe wengi kabla na baada yangu, nilipendekeza katika kifungu hiki cha 23 kinachorekebisha kifungu cha 24 cha sheria mama kile kijifungu cha 3 lile neno Mtanzania liondoke na badala yake iwe Mzanzibari, na hoja yangu na yetu ilikuwa ni kwamba kwa msingi wa kutunza ajira kwa Wazanzibari basi suala la *principle* liwe ajira ni kwa Wazanzibari, na wala hilo sio kosa popote ndio inavyofanyika na kama kuna *exception* kwamba Mzanzibari atakuwa hakuna basi utaratibu ulioko hapa utabakia kama atapata kibali cha waziri au kamati ilipendekeza Kamisheni na ikakubali. Kwa hivyo, naomba hili kwa moyo wote Mhe. Mwenyekiti, alijibu kwani ameliacha tusije tukapiga kura Mtanzania iondoke iingie hapa Mzanzibari kwa kulinda haki ya kikatiba ya Wazanzibari kupata ajira lakini pia kutunza haki zetu za wananchi wetu katika maeneo yetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nimesikia Mhe. Mjumbe ni kwamba tumeliona hilo, lakini kwa sababu hili suala la ajira unajua ilikuwa ipo hiyo neno Mzanzibari katika sheria ya kazi lakini ikafutwa, sasa sheria inasema uajiri itabidi iwe ni Mtanzania badala ya Mzanzibar. Kwa hivyo, labda tufute kipengele hiki cha sheria ndio turuhusu hilo, lakini kutoka naona itakuwa ni vigumu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo yake Mhe. Waziri sikubaliani naye, katiba yetu ibara ya 21 ibara ndogo ya 3 inazungumzia haki ya kila Mzanzibari inasema kila Mzanzibari ana haki ya kufanya kazi, kama ikiwa hizi nafasi za ajira katika sekta kubwa kama hizi tunashindwa kuzilinda kwa Wazanzibari, basi kweli Baraza hili litakuwa limepoteza kabisa msingi wake wa kuwatumikia Wazanzibari naomba sana hili serikali ikubali.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tunalia hapa kuna maeneo ya kazi ambayo Wazanzibari wanapaswa kuwa nazo katika Jamhuri ya Muungano hatuzipati, basi hata hizi za Zanzibar pia tunashindwa kuwalindia Wazanzibari. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, akubali Mhe. Waziri kwamba kifungu hiki tukirekebishe hapa ibakie kwamba ni Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, hata katika sheria hii tukenda katika tafsiri kule kuliingizwa neno tafsiri ya Mzanzibari katika ukurasa wa 42 kwamba Mzanzibari maana yake ni Mzanzibari kama alivyotafsiriwa katika sheria ya Mzanzibari Nam. 5 ya 1985. Kwa hivyo, madhumuni ya nini kuweka tafsiri ya Mzanzibari ikiwa tunashindwa kumpa Mzanzibari haki hii, hili Mhe. Mwenyekiti, naomba tusifikishane mbali nimuombe Mhe. Waziri akubali kama alivyonikubalia katika maeneo mengine ili serikali ikubali kubadilisha iweke Mzanzibar, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi natamani sana hili neno libakie Mzanzibari na mimi napenda sana hilo, lakini sasa kila nikiangalie hii *Act* ya*labour* ndio ambayo imenifunga. Lakini kama tutabadilisha sheria basi mimi sina pingamizi mimi napenda iwe hivyo Mzanzibari, labda wanasheria watatueleza nini tufanye. Lakini mimi kwa muono wangu nimekwenda kwa mujibu wa sheria inavyosema ya *LabourAct* ndio nikaja na hili, sio kwamba nimeweka kwa kuwa napenda, hapana mimi napenda iwe Mzanzibar lakini hali ndio imekuwa hivyo labda ufafanuzi zaidia atatoa Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nasimama hii itakuwa ni mara yangu ya tatu na ya mwisho kujibu kwa utaratibu kwa hivyo nasema kabisa sioni kama *Labour Act* imesema hivyo kwamba kwa sheria fulani ilikuwa ina *restrict* kwamba itakuwa inafanya kosa. Kama ambavyo kuna nafasi nyingi zinasema lazima awe Mzanzibari sioni kwa hapa iwe ni kosa, kwa hiyo napendekeza kwamba tubakishe hivyo na ikiwa serikali inafikiria juu ya hilo basi mimi naomba tupige kura katika hili, kabisa. Kwa sababu sidhani kama hili nitaambiwa nilete kwa maandishi kwamba linakiuka msingi mzima wa maudhui ya mswada nadhani tutakubaliwa tupige kura.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba tatizo tulilonalo ni hilo kwamba sheria ya labor itakuwa imeruhusu, lakini *actual* sheria ya *employment* sasa imeruhusu hilo, lakini huku tukiliweka hivyo tatizo tutakalokuwa nalo ni kwamba tuna sheria mbili ambazo zenyewe zinapingana. Mhe. Mwenyekiti, na jengine ambalo tunalo ni kwamba tunaingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

ambayo kuna kitu tunaita *free movement of labour*. Kwa hivyo, ndio maana tukasema kwamba kitu cha kuanza cha mwanzo na sisi tukumbuke Wazanzibari pia kwamba tuna operate pia upande wa Bara na hakuna *restriction* kinachozungumza ni Mtanzania kwa nchi nzima.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sidhani kama tutaweka *restriction* labda ya kisheria kwamba ni jambo ambalo litakuwa linatusaidia sana. Kwa sababu kama tunaweka restriction ya kisheria hapa maana yake na wenzetu nao wanaweza kutuwekea *restriction* ya kisheria na sisi *market* hizi mbili za utalii zinategemeana sisi tuna watu upande mwengine, na wao wana watu upande huu huku. Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani cha *enforce* ni namna gani ya ku-*empower* watu wetu kuweza kufanya hizi kazi wakiwa humu ndani kwa sababu wana *cooperative advantage*, wana *competitive advantage.* Lakini nadhani kwa sasa hivi tutakuwa na hiyo *conflict*, kwanza katika *level* ya huko tunakokwenda ya *East Africa Community* ambayo tumeikubali na tunakwenda nayo. Lakini la pili hata humu ndani utaratibu huo tutakuwa tunajiwekea *restriction* ambazo zinaweza zikaja zikatudhuru sisi wenyewe katika ku-*operate* kwenye soko jengine la upande wa Tanzania Bara.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, *legislative process* Mhe. Mwenyekiti, ni suala la *compromise* sidhani kama *compromise* kila mara lazima zifanywe na upande mmoja tu. Mimi nasisitiza kwamba hata kama sheria kwa jumla ya ajira imeweka kuwa ni Mtanzania bado kunaweza kukawa na sheria nyengine wala utakuwa hujakosea kusema kwa sekta hii umetunza ajira kwa Mzanzibari. Kama ambavyo hapa kwa Mwenyekiti sidhani kama tulivunja sheria ile tuliposema Mwenyekiti awe Mzanzibari na hii pia ni ajira. Kwa hivyo, nasema bado mimi sijaona mantiki ya hoja hii, na kama suala la *free movement of labour* kuna mashaka mengine mengi nadhani hata kwa sasa tusiliingie.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ya Mhe. Mwanasheria Mkuu kusema na wao watalipiza, mimi ninavyojua hakuna Mtanzania Bara wala hakuna sheria ya Mtanzania Bara kumtambua Mtanzania Bara au Mtanganyika, lakini Zanzibar iliunda serikali yake na ikaweza sheria ya Mzanzibari ili kuhakikisha kwamba kuna haki maalum ambazo wanazifaidi Wazanzibari kwa upande wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu kama walikataa kuunda Tanganyika yao na Serikali yao na kumtambua Mtanganyika hilo ni lao wao, sisi halituhusu. Lakini kwa hapa Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama nilivyosema nimeshasimama sana kama serikali ina *hard feeling* tupige kura wajumbe tupate kuamua, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, *concerns* zote mbili zina uzito. Kwanza kuna sheria ya kazi sasa hii Mhe. Mwenyekiti, ni sheria ambayo tumeitunga sisi wenyewe na sheria hii inasema kwamba ni Mtanzania. Lakini hapa Mhe. Jussa anasema kwamba *priority* zende kwa Wazanzibari katika shughuli hizi ambayo ndio kilio cha watu wetu. Mhe. Mwenyekiti, mimi ningelipendekeza na ningelimuomba Mhe. Jussa kwa sababu katika sheria hii kuna kifungu katika sheria mama inayosema kwamba waziri atatunga kanuni zinazoendeana na sheria nzima.

Mhe. Mwenyekiti, katika hizo kanuni ziwekwe kwamba *priority* ya uajiri basi itakuwa kwa Mzanzibari pale ambapo hapana itakwenda kwa Mtanzania Bara. Mhe. Mwenyekiti, ikishakuwekwa kanuni hiyo itakuwa imeshafungika au utaratibu wote wa uajiri utakuwa umeshafungwa kwamba lazima lazima *priority* iende kwa Mzanzibari halafu ndio itakwenda kwa Mtanzania. Lakini vyenginevyo kutakuwa na *conflict* ya sheria ya mbili ambazo zitakuwa ni matatizo. Sasa ku-*avoid* hiyo conflict mimi napendekeza kwamba kanuni zile zilizoko kwenye sheria niseme kwamba *priority* ya uajiri katika sekta hizi itakwenda kwa Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jussa ulishatoa ushauri kwamba tupige kura na mimi nafikiria kutokana na maelekezo ya Waziri wa Katiba na Sheria ni kwamba tunaweza kupiga kura kwamba iwe ni Mtanzania lakini kwenye kanuni ielezee kwamba ni Mzanzibari, hiyo moja au ya pili ioneshe kwamba ni Mzanzibari.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hoja ilikuwa ni yangu waziri alikuwa ana-*respond* mwenye hoja naomba ipigiwe kura kwamba awe ni Mzanzibari. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo tunapiga kura wanaokubali kwamba neno Mtanzania liondoshwe badala yake liwe Mzanzibari, wanyanyue mikono. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe ushauri umetoka kwamba kura mtu mmoja mmoja anatajwa halafu anajibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kibakie kama kilivyo nadhani haina haja ya kupiga mara mbili, isipokuwa tunachopigia kura kwa sababu marekebisho hayajakubaliwa ni kifungu kama kilivyo wanaokikubali na wanaokikataa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani kabisa hoja ya serikali kuwepo niliyetoa hoja ni mimi wa kupiga kura, hoja yangu ni kwamba kifungu hiki kibadilishwe kiwekwe Mzanzibari. Kwa hivyo, hoja inayopigiwa kura ni hiyo kwamba wanaotaka Mzanzibari waseme ndio na wanaokataa waseme hapana kwa sababu hoja niliyetoa ni mimi sio hoja ya serikali, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiria hakuna tofauti hapo mnasema kwamba hiki kifungu aidha kipitishwe kama kilivyoandikwa au neno Mtanzania kifanyiwe marekebisho neno la "Mtanzania" liwe neno "Mzanzibari". Kwa hivyo, mimi nafikiria tufanye ule ule utaratibu wanaokubali kupitisha kifungu hiki.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, madhali tunapiga kura ni muhimu ikaeleweka kabisa kwamba ingelikuwa tunapigia mswada huu nimesema niliyotoa hoja ni mimi kwamba ibadilishwe kwa hivyo hoja yangu mimi ndio ya kusema ndio kwa vile mimi ndiye niliyetoa hoja na wanaosema hapana kwani mimi ndiye niliyetoa hoja kwamba hiki kifungu kibadilishwe kiwe Mzanzibari. Kwa hivyo, tukisema tunakipigia kifungu kama kilivyo itakuwa tunapiga hoja ya serikali na mimi ndiye niliyetoa hoja, serikali haikutoa hoja kama ipigwe kura hapa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu ni kwamba hapa pana kifungu ambacho tunakizungumza Mhe. Jussa yeye anasema kifungu hiki angalipenda kirekebishwe kutoka Mtanzania kwenda Mzanzibari. Kwa hivyo, *issue* tunayozungumza ni kifungu hiki kwa hivyo suala linalokuja ni kwamba je wale wanaopenda kifungu hiki kibakie, kama kuna wale waliokuwa hawapendi kifungu hiki kibakie ndio watakuwa wale waliokuwa hawakupiga kura. Ni kwamba tunazungumzia hii sheria iliyokuwepo hapa hatuzungumzii hoja aliyoileta yeye, kama ni hoja aliyoileta yeye angelileta hoja yake binafsi. Kwa hivyo, hapa haya ni masuala yaliyokuja katika mswada huu, yeye ameleta hoja ya kubadilisha hili neno.

Mhe. Mwenyekiti, kama ameleta hoja ya kubadilishe neno kuna *issues* mbili ya kwamba kuna watu ambao wanataka kifungu hiki au kuna watu hawataki kifungu hiki. Ndio hoja yenyewe kwa hiyo wanaotaka kifungu hiki watapiga kura na waliokuwa hawataki hawatopiga kura ndio itakuwa ni ile kwamba wanataka *sugestion* aliyozungumza Mhe. Jussa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tunachouliza ni hiki hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa mimi nafikiria tufanye maamuzi kama tunapiga kura wanaotaka kifungu kibakie hivi hivi na wale ambao wanataka kifungu kibadilike neno Mtanzania liwe Mzanzibar, tutapiga kura hiyo tena kwa majina.

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe, tunaanza kuita majina kwa hiyo ambaye ataitwa jina lake atasema anakubali au anakataa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, anayetaka kibakie kama kilivyo aseme ndio nilivyokufahamu na anayetaka Mzanzibari aseme hapana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, ni kwamba anayetaka kibakie kama kilivyo atasema ndio, na anayetaka kibadilike kiwe Mzanzibari basi atasema hapana.

Katibu: Kwa hivyo, naanza kuita majina.

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Hayupo.
2.	Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa	-	Hapana

UTARATIBU

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwani kura hatujapiga hapa mimi nauliza, sasa mbona mnatuyumbisha, mimi nauliza kwa mujibu wa utaratibu sasa mbona mnaturudisha tena hapa tunatunga kitu muhimu sana katika nchi hii. Kwa hivyo, tuwe na utaratibu mzuri na wengine wanasema hawajafahamu hapa, wameniambia mimi.
Kwa hivyo, tunataka tufahamishwe nafasi ya Mzanzibari ni ipi nafasi ya Mtanzania ni ipi mpaka watu wafahamu. Lakini mnatufanya kama watoto wadogo humu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha hapa tumefanya maamuzi ya kupiga kura na tumesema tutafanya maamuzi kutokana na hoja yaliyoleta marekebisho ambayo Mhe. Jussa anayataka ama iendelee kifungu kibakie hivi hivi au kifungu neno Mtanzania libadilike na iwe Mzanzibari. Nafikiri hiyo inafahamika kabisa kwa hivyo tunapiga kura kwa sababu mjumbe kataka tupige kura. Kwa hivyo, tunafuata mjumbe anavyotaka tufanye hii ni haki yake kutaka kupiga kura. Kwa hivyo, nawaomba waheshimiwa tuendelee.

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

3. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Hapana

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa sisi ni watu wazima tuko hapa kuwawakilisha wananchi tufanye mambo ya busara, haya ni maamuzi muhimu.

Katibu: Waheshimiwa Mhe. Mwenyekiti, ameshafanya maamuzi nadhani tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe naomba ukiheshimu kiti, kiti kimeshafanya maamuzi basi.

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, naanza tena hili zoezi kwa hivyo, naomba Mheshimiwa atakaetajwa anyanyuke kama yupo aseme watu wote wasikie, tujue ni kitu gani anataka tuweze kuendelea.

Mhe. Ali Abdalla Ali - hayupo
Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa - hapana
Mhe. Mgeni Hassan Juma - ndio
Mhe. Balozi Seif Ali Iddi - hayupo
Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame - ndio
Mhe. Omar Yussuf Mzee - hayupo
Mhe. Haji Omar Kheir - hayupo
Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej - hayupo
Mhe. Moh'd Aboud Moh'd - ndio
Mhe. Abubakar Khamis Bakary - ndio
Mhe. Hamad Masoud Hamad - ndio
Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban - hayupo
Mhe. Juma Duni Haji - ndio
Mhe. Zainab Omar Moh'd - ndio
Mhe. Abdillah Jihad Hassan - ndio
Mhe. Ali Juma Shamuhuna - hayupo
Mhe. Mansour Yussuf Himid - hayupo
Mhe. Nassor Ahmed Mazrui - ndio
Mhe. Said Ali Mbarouk - ndio
Mhe. Haroun Ali Suleiman - ndio
Mhe. Suleiman Othman Nyanga - hayupo
Mhe Haji Faki Shaali - ndio
Mhe. Machano Othman Said - ndio
Mhe. Issa Haji Ussi - hayupo
Mhe.Zahra Ali Hamad - ndio
Mhe. Dr. Sira Ubwa Mwamboya - hayupo
Mhe. Bihindi Hamad Khamis - ndio

Mhe. Haji Mwadini Makame - hayupo
Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi - ndio
Mhe. Othman Masoud Othman - ndio
Mhe. Abdalla Juma Abdalla - abstain
Mhe. Abdalla Mohammed Ali - hapana
Mhe. Abdi Mosi Kombo - imeharibika
Mhe. Ali Mzee Ali - hapana
Mhe. Ali Salum Haji - hayupo
Mhe. Amina Iddi Mabrouk - hayupo
Mhe. Asaa Othman Hamad - hapana
Mhe. Asha Abdu Haji - hapana
Mhe. Asha Bakari Makame - hapana
Mhe. Ashura Sharif Ali - hapana
Mhe. Bikame Yussuf Hamad - hayupo
Mhe. Farida Amour Mohammed - hapana
Mhe. Fatma Mbarouk Said - hapana
Mhe. Hamza Hassan Juma - hapana
Mhe. Hassan Hamad Omar - hayupo
Mhe. Hija Hassan Hija - hayupo
Mhe. Ismail Jussa Ladhu - hapana
Mhe. Jaku Hashim Ayoub - hapana
Mhe. Kazija Khamis Kona - hayupo
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - hayupo
Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - hapana
Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - hayupo
Mhe. Mohammed Haji Khalid - hayupo
Mhe. Mohammedraza Hassanali - hayupo
Mhe. Mohammed Mbwana Hamad - hayupo
Mhe. Mohammed Said Mohammed - hayupo
Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - hayupo
Mhe. Mussa Ali Hassan - hapana
Mhe. Mwanaidi Kasim Mussa - ndio
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - hapana
Mhe. Nassor Salim Ali - ndio
Mhe. Omar Ali Shehe - hapana
Mhe. Panya Ali Abdalla - hapana
Mhe. Rashid Seif Suleiman - hayupo
Mhe. Rufai Said Rufai - hayupo
Mhe. Raya Suleiman Hamad - hapana
Mhe. Saleh Nassor Juma - hapana
Mhe. Salim Abdalla Hamad - hapana
Mhe. Salma Mohammed Ali - hayupo
Mhe. Salma Mussa Bilal - hayupo
Mhe. Salmin Awadh Salmin - imeharibika
Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - ndio
Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - hayupo
Mhe. Shawana Bukheti Hassan - ndio
Mhe. Subeit Khamis Faki - hayupo
Mhe. Suleiman Hemed Khamis - hayupo
Mhe. Ussi Jecha Simai - hapana
Mhe. Viwe Khamis Abdalla - ndio
Mhe. Wanu Hafidh Ameir - hayupo

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutaja waliosema ndio au tutahesabu kwa pamoja. Mhe. Mwenyekiti, naomba nitangaze matokeo ya kura tulizopiga, Waheshimiwa waliohudhuria wote ni 47, Waheshimiwa 22 wamesema ibakie

Mtanzania au wamepitisha kifungu kama kilivyo, Waheshimiwa wawili wamekataa kusema lolote na Waheshimiwa wawili wameharibu kura zao kwa makusudi. Waheshimiwa 21 wamekataa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, tulikubaliana kusema ndio au hapana na tukakubaliana kwamba. Waheshimiwa naomba tusikilizane na mbakie. Nimesema Waheshimiwa tulikubaliana hapa tuseme ndio au hapana hakuna neno jengine. Kwa hivyo, aliyesema neon jengine aliamua kuharibu kura hivyo ndivyo tulifahamu sisi. Kwa hiyo walioshinda ni wale ambao wamekubali kifungu kibakie kama kilivyo.

Kifungu cha 24 - Marekebisho ya kifungu cha 25 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 25 - Marekebisho ya kifungu cha 28.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Baraza zima imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Wanaokubali hoja, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii 2012

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii 2012 usomwe mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti: Wanaokubali hoja, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii 2012 ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe, ahsanteni sana kwa siku ndefu, ngumu, mmenipa changamoto kubwa na ninawashukuru wote kwa ushirikiano mzuri. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kuahirisha Baraza hadi tarehe 10 Aprili, 2012 saa tatu asubuhi.

(Saa 3:17 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 10/04/2012 saa 3:00 asubuhi)